# UENDELEZAJI WA LEKSIKONI YA KISWAHILI

"Tasnifu Hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya M.A. katika Chuo Kikuu cha Nairobi" 1993.

## UNGAMO

" Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika Chuo Kikuu kingine chochote".

MWARO GEORGE A. WERE
(Mtahiniwa)

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Tasnifu hii imeandikwa chini ya uongozi wetu

sisi tulioteuliwa kuisimamia

Prof. M.H. Abdulaziz

na

Ndg Kineene wa Mutiso

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146616 8

1993

KUTABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wazazi wangu
Baba Festus Were na Mama Regina O. Were,
ambao hawajachoka kunishauri kuwa:

"Muata kiwi hanacho
na chema kimpotele".

## SHUKRANI

Ama kwa hakika, masuala ya kiusomi hayakamilishwi 'vivi hivi tu' pasi na usaidizi, na mijadala ya hapa na pale. Ningependa kutoa shukrani kwa wote walionifaidi, wakanielekeza na kuniongoza na kunifikisha salama kando ya bahari hii tesi yenye mangi masi. Kwanza kabisa naona fahari kubwa kuwatolea shukrani zangu za dhati na wala si za thati wasimamizi wangu Prof. Abdulaziz M.H. na Ndg. Wa Mutiso K. kwa kuisoma, kuikosoa na kuirekebisha kazi hii. Ama kwa kweli bila ya wao, ningekwama. Siku nenda rudi nitakumbuka usaidizi wao na kujitolea kwao kuniongoza hadi mwisho wa tasnifu hii.

Pia nawashukuru Prof. Kitsao J; Dkt. Kiingi K.B, Ndg Wamitilah K.W., Gibbe A.G., Aswani F., Mutonya J.M kwa kuisoma, na kunielekeza ipasavyo. Prof. Kitsao, Dkt. Kiingi na Wamitilah walinifaa sana pia kwa kunipa vitabu chungu nzima vya kusoma.

Bila kuwasahau Dkt. Mwansoko Herman J., Yambi J. (Miss), Mgullu R., na Ndg. Habwe J.H. **kwa** kujaza hojaji yangu vizuri na kunipatia mawaidha ya busara.

Siwezi kamwe kusahau wanafunzi wenzangu Bi. F. Njeri, K. Gitare, E. Mirieri, Fred Baya, Bi A. Ogugo, B. F. Indede, Bi.G. Chepkwony, R.W. Oduori, Bosire B.M., Nkubitu P.K, Mosoti Z., Sewangi S., L. Muaka, na J. Michira Nyachae ambao tuliendesha mijadala pamoja na nikapata mawazo yaliyonifaa zaidi.

Kadhalika, sina budi kuwatolea shukrani zangu za dhati wazazi wangu Baba Festus Were O.M. na Mama Regina O. Were kwa mapenzi yao, usaidizi wao wa hali na mali na uvumilivu wao wakati wote wakipambana na masomo yangu ya uzamili. Katika kundi hili naweka jamaa na marafiki

zangu Bi. Mwaro. C. Nabwire, G.M. Lubale, Bi. Gumo S., H.P.O. Namango, Canuti Mugeri, Fred. M. Mwaro, Bi M. G Wanderwa, Bi. L. Kiura, Z.G. Wanjau, Mwambela Ken, Francis W. Mwaro, Stephen Okwero Were, B. Khalambula, Bi. Margaret Ndubi, Beneah M. Mutsotso na mwanangu mpendwa A. Mercy Mwaro kwa kunitia moyo na kunishawishi nisikate tamaa.

Mwisho nazitoa shukrani zangu kwa Bi. Agnes Kwendo kwa kuipiga chapa tasnifu hii kwa makini na uangalifu mkubwa zaidi.

Kwenu nyote nasema shukrani.

## YALIYOMO

SURA YA KWANZA — Ukurasa

Utangulizi ............ (ii)
1.1 Somo la Utafiti ............ 1
1.2 Madhumuni ya Tasnifu ............ 2
1.3 Sababu za kuchagua Mada hii ............ 2
1.4 Upeo wa Tasnifu ............ 9
1.5 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ............ 11
1.6 Haipothesia ............ 16
1.7 Msingi wa kinadharia wa Tasnifu ............ 17
1.8 Njia za utafiti ............ 24
1.9 Tanbihi ............ 25

SURA YA PILI

2.1.0 Utangulizi ............ 26
2.1.1 Maana ya ufufuaji wa msamiati wa zamani. 28
2.1.2 Sababu za 'kufa' kwa msamiati wa zamani wa Kiswahili ............ 29
2.1.3 Sababu za ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili 'uliokufa' ............ 40
2.2.1 Namna msamiati katika lahaja nyingine unavyoweza kuendeleza leksikoni ya Kiswahili ............ 57
2.2.2 Nafasi ya msamiati wa zamani wa Kiswahili 66
2.2.3 Muhtasari ............ 78

SURA YA TATU

3.1.0 Utangulizi ............ 80
3.1.1 Dosari na udhaifu katika taratibu za uundaji wa msamiati wa Kiswahili ............ 81
3.1.2 Utaratibu wa ubunaji ............ 85
3.1.3 Ukopaji/Utohoaji ............ 88
3.1.4 Kaleki ............ 98
3.1.5 Uambatanishaji ............ 100
3.1.6 Akronimu ............ 104
3.1.7 Uhuluti ............ 105

3.1.8 Ukatizaji.............................. 107
3.1.9 Unyambuaji............................ 109
3.1.10 Muhtasari............................. 111

SURA YA NNE

4.1.0 Utangulizi............................ 112
4.1.1 Mabadiliko na upoteaji wa maana katika msamiati wenye asili ya kigeni.......... 113
4.1.2 Tatizo la maneno yanayokubalika kwa watumizi na wataalamu wa lugha ya Kiswahili........................... 120
4.1.3 Suluhisho............................ 124
4.1.4 Hitimisho............................ 128
4.1.5 Tanbihi.............................. 131
4.1.6 Marejeleo............................ 134

"Kiswahili katika Kenya kinaweza kulinganishwa na tajiri mwenye nguo katika sanduku kumi chumbani, halafu akaingia katika mashindano ya uvaaji huku akiwa na kikoi kilichopasuka akishindana na maskini mwenye kanzu moja maridadi".

(Wency Cornell 'Taifa Weekly'

November 24, 1979).

UNIVE... ...OBI

## SURA YA KWANZA

### Utangulizi

Lugha hii ya Kiswahili kama historia inavyotueleza, ni ya kale sana na ilikuwa ikitumiwa na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki hata kabla ya kuja kwa Waarabu, Waajemi, na watu wa Ulaya. Izingatiwe kwamba maajilio ya wageni yalisababisha msamiati kiasili mwingi wa Kiswahili kusahaulika ama 'kufa' na pahali pake pakachukuliwa na msamiati wa kigeni na kwa namna hii kukifanya Kiswahili kichukuliwe kuwa kina upungufu wa msamiati. Iwapo matumizi ya msamiati wa kigeni ndiyo yanayofanya lugha hii ichukuliwe hivyo, basi na wakati umewadia wa wataalamu wa Kiswahili kufikiria namna ya kupunguza (ama kuepukana kabisa ikiwezekana) ukopaji mwingi wa msamiati wa kigeni ili lugha hii isilaumiwe na watu kwa sababu ya ujinga wao wenyewe. (Kitsao 1989:51)

Hata hivyo, ieleweke kwamba hakuna lawama yoyote kwa lugha yoyote kupanua na kuendeleza msamiati wake kwa kutumia msamiati kutoka lugha za mataifa ya kigeni. Jambo lisilofaa, lisilotakikana na lisilokubalika ni lile la kuifanya lugha ya Kiswahili kuonekana isiyokuwa na asili yake ama isiyoweza kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo kwa kuendelea kukopa msamiati mwingi wa kigeni. Pana haja ya kufahamu kuwa si lazima tukope na ukopaji mwingi si ubunaji. (over borrowing is not creative).

A. Sheikh Nabhany (1982) na K.B. Kiingi (1992) ni miongoni mwa wataalamu ambao wamejitokeza na njia tofauti za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili kwa kukiondolea ugeni mwingi. Nabhany

badala ya kutumia msamiati ulioazimwa katika Kiingereza au Kiarabu anaunda msamiati kwa kutafsiri maana ya viungo vidogo vya maneno vyenye maana kutokana na lahaja kadhaa za Kiswahili. Kwa mfano,

| Kiingereza | | Kiswahili/Maneno yaliyopendekezwa |
|---|---|---|
| Television (televisheni) | - | Runinga |
| Ray (rai) | - | Uka |
| University (Chuo kikuu) | - | Ndaki |
| College (Koleji) | - | Uwoti (Uwote) (yaani kwa masomo ya aina zote) |
| Retire (ritaya/staafu) | - | Tuta |
| Science (sayansi) | - | Ulimbo |
| Mathematics (Hesabu) | - | Maenga |

K.B. Kiingi badala ya kuazima msamiati wa sayansi kama vile kemia, bayolojia na fizikia kutoka kwa lugha za kigeni amependekeza msamiati huo uundwe kwa kutazama baadhi ya mofimu zinazoweza kurekebishwa ama kunyumbuliwa (extrapolated) ili zifanye kazi ya ujenzi - neno Mathalani;

| Kigeni | Kiswahili | Mifano |
|---|---|---|
| Hydro | - maji | Hydrogen = kiunda-maji |
| -Phyte | mea- | Hydrophyte = Kimeamaji |
| | | Neophyte = Kimeachanga |
| | | Palophyte = Kimeachumvi |

Photo Chemistry = Kemia-Vimea

Hapana shaka kwamba kama juhudi zote zinazofanywa na wataalamu wa TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) zitazingatia kwa kadri inayowezekana njia hizi za Nabhany na Kiingi, za kuunda msamiati, lugha ya Kiswahili, kwa maoni yetu, itakuwa na msamiati bora ambao uliangamizwa kwa sababu ya haraka za kuzifuata lugha za kigeni - Kiarabu, Kiingereza n.k.

Kazi hii kwa hivyo ni jaribio la kutazama umuhimu wa kufufua msamiati wa zamani wa Kiswahili, kama njia mojawapo ya kuendeleza leksikoni ya lugha hii kwa kutumia nadharia ya PEGITOSA. Masuala yote yatakayojadiliwa yanatokana na msingi wa hoja kwamba Kiswahili kama lugha nyingine yoyote, kina uwezo wa kujitosheleza na kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

## 1.1 SOMO LA UTAFITI

Ingawa suala la uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili limeshughulikiwa na wataalamu mbali mbali wa TUKI, na watetezi wengine wa Kiswahili kwa kutumia taratibu za uundaji wa msamiati kama vile ukopaji (borrowing), ubunaji (coinage), kaleki (calequing), akronimu, unyambuaji (derivation), uambatanishaji (compounding) n.k. kuna njia nyingine ya ufufuaji wa msamiati kiasili ama wa zamani wa Kiswahili ambayo haijatiliwa uzito na ndiyo tunataka kuiangalia. Katika kujadili suala hili tunataka pia kuchunguza namna msamiati unavyoundwa na wataalamu wa TUKI na ikiwa pana haja ya kuunda msamiati wa Kiswahili kwani Kiswahili hakikuwa na msamiati wao asilia? Je, ni kweli kwamba Kiswahili kilikuwa na pengo kubwa la kimsamiati au msamiati wa zamani tayari ulikuweko ambao wataalamu wa TUKI wangeupekuwapekuwa miongoni mwa Waswahili wenyewe na kuupata?

Je, ufufuaji wa msamiati wa zamani una umuhimu wowote katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili? Hiki hasa ndicho kiini cha kazi hii na kinatokana na sababu kwamba msamiati wa zamani mwingi sana wa Kiswahili haukufikiriwa na wataalamu wa TUKI wala katika Kiswahili sanifu, hivyo unatakikana kufufuliwa na kupewa matumizi mapya.

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

1. Kuchunguza msamiati wa zamani wa Kiswahili ambao umesahaulika na kupendekeza ufufuliwe kama hatua moja ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili.
2. Kuchunguza mada'i ya wataalamu kama Broomfield na Lyndon Harries (1964: 228) kwamba Kiswahili hakiwezi kujitosheleza kimsamiati. Izingatiwe daima kwamba kila lugha ina ukwasi wake, hivyo basi lau lugha hii ya Kiswahili haingekuwa na uwezo wa kujitosheleza, msamiati wa zamani haingekuwa nao.
3. Kutazama kwa jicho la ndani zaidi namna msamiati unavyoundwa na TUKI na iwapo kweli kulikuwa na pengo kubwa la kimsamiati au msamiati wa zamani tayari ulikuweko ambao wangeupekuwapekuwa miongoni mwa Waswahili wenyewe na kuupata.
4. Kuangalia namna PEGITOSA[1] inavyoweza kuendeleza msamiati wa Kiswahili kwa njia ifaayo zaidi.

## 1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

1. Ilhamu ya kuchagua mada hii inatokana na umuhimu wa suala tunalolishughulikia. Ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili

kama hatua ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili ni suala ambalo litatoa mchango mkubwa katika Kiswahili bali na kuonyesha kuwa lugha hii inaweza kujitosheleza kimsamiati na kujiendeleza mumo kwa mumo pasi na kuendelea kukopa msamiati wa kigeni.

2. Aidha, tumechagua mada ya uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili kwa sababu ni uwanja ambao haujatiliwa uzito. Wataalamu ambao wamewahi kutoa mchango fulani kuhusu suala la ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili kama njia moja ya kuendeleza leksikoni ya lugha hii, kulingana na uchunguzi wetu, 'hawakulitendea haki' kwa maana kwamba hawakulitazama kwa mapana na marefu yake. Kwa usemi mwingine, sisi tunataka kulipigia mbizi zaidi suala hili ambalo limekimbiwa na wataalamu wengi wa Kiswahili.

A. Baruwa (1979) anasema:

> "... neno lizaliwe katika maneno yake asili au likiwa ni jina la kitu kipya basi lizaliwe neno katika mnasaba wa kitendo chake. Kuijenga lugha ndani ya lugha yenyewe ndiko kuikuza bali kuiokotea maneno (kutoka lugha za kigeni) ni sawa na kuukata mchungwa kisha shina lake likapakatishwa matawi ya mdanzi, milimau, na ndimu. Hivyo ukubwa wa mti huo utakuwa si mchungwa tena." [2]

Maoni ya Baruwa yana uzito na tunakubaliana naye.

S.A. Nabhany (1982) ameshughulikia ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili na kwa hakika kazi yake ni muhimu kwetu. Mtaalamu huyu kwa kuzingatia usemi wa Baruwa kwamba 'neno lizaliwe katika

maneno yake kiasili' anaonelea kuwa badala ya kukopa msamiati wa Kiingereza, au Kiarabu, patumike msamiati kiasili uliopo katika lahaja mbalimbali za Kiswahili na kazi za fasihi za zamani kama vile Utenzi wa Hamziya (1749)(lugha iliyotumiwa ni Kingozi), Utenzi wa Al-Inkishaf (1810 - 1820) n.k. Kwa kuzingatia haya ameunda na kukusanya msamiati ufuatao:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| Universe | Bwaga (kiamu) |
| Space | Bwanga (Kiambu |
| Art | Ujomi |
| Blood | Ng'eu |
| Biology | Uhumbe |
| Oxygen | Mwai |
| Doctor | Hazigi |
| Institute | Mwima |
| Soldier | Joma |
| Energy | Ngosi |

Ama kwa hakika, kazi ya Sheikh Nabhany inaonyesha bayana kuwa ukwasi wa lugha ya Kiswahili ni pana sana na tunatumia sehemu ndogo tu ya msamiati wa Kiswahili. Kwa usemi mwingine, kuna msamiati kiasili mwingi wa Kiswahili ambao umesahaulika kiasi ~~cha~~ kwamba Waswahili wa zamani hizi hawawezi kuamini ya kwamba ni wa Kiswahili. Jambo hili linamaanisha kuwa hapajawahi kuweko pengo kubwa la kimsamiati katika Kiswahili na kinachohitajika, kwa upande wa TUKI, si kuunda msamiati mpya kwa ukopaji bali kubukua na kufufua msamiati wa zamani wa lugha hii na kuupanua kimaana ama kuupatia matumizi mapya.

3. Isitoshe, sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kutaka kutazama kwa macho makali udhaifu na dosari katika taratibu zinazochukuliwa na wataalamu wa TUKI katika kuunda msamiati wa Kiswahili, suala ambalo pia halijashughulikiwa vya kutosha.

4. Aidha, tunataka kuziba mwanya wa kinadharia ulioachwa wazi na wataalamu walioshughulikia suala hili bali na kutaka pia kuongesea katika hazina ya maarifa yanayohusu somo hili

Izingatiwe hapa kwamba kufikia sasa wanaleksikografia wa Kiswahili hawaelekei kujitokeza na utaratibu maalum na wenye mantiki wa kuunda msamiati au wa kuendeleza leksikoni ya Kiswahili ambao unafaa kuzingatiwa na wapenzi wa Kiswahili. Kwa mfano, wataalamu wa TUKI wamependekeza matumizi ya majina haya:-

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| antibiotic | ngoamwili |
| antibody | mzindike |
| plasmagene | utoroji |
| plasmalema | ugozimwili |
| analysis | uchambuzi |
| photolysis | uvunjikaji kimwanga |
| pyrolysis | pairolisi |
| acidolysis | asidolisi |

Ni dhahiri kutokana na mifano hii kwamba hakuna mfumo ulio sawa au mfumo maalum unaofuatya kwa maana kwamba msamiati umeundwa ' vivi hivi tu'. Umbo la dhana za 'anti-', 'plasma' na '-lysis'

halijitokezi katika msamiati wa Kiswahili. Iwapo kwa mfano, 'photolysis' ni uvunjikaji kimwanga, kwa nini 'pyrolysis' - isiwe uvunjikaji kijoto? (Kiingi 1989)

Licha ya hayo, wanaleksikografia na wataalamu kama vile C.W. Temu (1972), M.H. Abdulaziz (1987), J.S. Mdee (1986), D.P.M. Massambwa (1987), H. Akida (1971) wanasisitiza kuwa msamiati wa Kiswahili upanuliwe kwa kukopa msamiati wa kigeni kwa madai kuwa hakuna lugha ulimwenguni isiyowahi kukopa msamiati wa kigeni wala inayojitosheleza,kimsamiati. Madai haya yanahitaji uchunguzi zaidi hasa tukichukulia kwamba KICHINA na KIJERUMANI zinaelekea kujitosheleza zenyewe na zinajiendeleza mumo kwa mumo.

N.I. Sharif (1988:28) anaunga mkono mawazo ya wataalamu tuliowataja na anasema:

> "... utajiri wa lugha, nguvu zake na uwezo wake wa kudumu na kukidhi haja za wanaoitumia ni uwezo wake wa kuazima maneno ya lugha nyingine na kuyafanya yake".[3]

Naye M.H. Abdulaziz kuhusu ukopaji anasema:

> "La ajabu na hoja ya ukweli inayohusu uundaji wa istilahi mpya, ni kwamba Kiingereza ni changizi au chanzo au kisaidizi ... lugha ya dhana za kutumiwa katika Kiswahili." [4]

.../7

Mtaalamu huyu anaendelea kututolea mpango unaopaswa kuzingatiwa katika ukopaji. Anapendekeza tuanze na:

(i) Lahaja za Kiswahili

(ii) Kiarabu

(iii) Lugha za Kibantu

(iv) Kiingereza na Kigiriko - Latini

Maoni haya ya Sharif na Abdulaziz, hata hivyo, hayaafikiani na maelezo ya G.W. Broomfield (1930). Broomfield anaeleza kwamba maneno yenye asili ya Kiarabu ni maneno ya Kiswahili hivi kwamba Kiswahili hakijawahi kuwepo bila ya maneno ya Kiarabu na kwamba hakiwezi kuyaondoa. Ukweli kwamba Kiswahili kilikuwa na msamiati wake kiasili au wa zamani kabla ya kuja kwa Waarabu hauwezi kubishaniwa (Mbaabu 1991:34). Msimamo wetu ni kwamba badala ya kuazima msamiati wa Kiarabu, Kiingereza n.k. na kuuswahilisha, tupekuwepekuwe miongoni mwa lahaja za Kiswahili, - Kiamu, Kitikuu, Kimvita, n.k. na kufufua msamiati kiasili wa Kiswahili kama njia moja ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili. Aidha, pale ambapo hatupati maneno mwafaka kuhusu dhana za kisasa za Kisayansi na Kiteknolojia tufanye unyumbuaji wa mofimu za Kiswahili (we should extrapolate Kiswahili morphemes) kwa kuzingatia nadharia ya PEGITOSA. Kwa mfano,

Family ________ Kizazi (badala ya familia)

Genus ________ Ndugu (badala ya jenusi)

Species ________ Aina (badala ya spishi)

Kwa kuyumbua mofimu za Kiswahili tunapata maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| Family | Kizazi |
| Sub family | Kijizazi |
| Infrafamily | Kijijizazi |
| Genus | Ndugu |
| Subgenus | Kidugu |
| Infragenus | Kijidugu |
| Species | Aina |
| Subspecies | Kiaina |
| Infraspecies | Jiaina |

(taz. Kiingi 1989:179)

Kutokana na mfano huu ni wazi kwamba Kiswahili kinaweza kujiepusha kuazima msamiati wa kigeni moja kwa moja na kuuswahilisha. Hivyo si lazima lugha ya Kiswahili ikope msamiati wa kigeni hasa wa kisayansi na kiteknolojia kama inavyodaiwa na baadhi ya wataalamu.

G.W. Broomfield (1930) anaandika hivi:

> "Maendeleo yoyote ya kielimu huhitaji kuwa na mabadiliko na maendeleo ya lugha itakayotumika kueleza elimu hiyo. Tupende tusipende, Kiswahili kitabadilika na kuendelea kwa haraka, kwa sababu... Kiswahili cha miaka ishirini tu iliyopita hakifai siku hizi. Ni lazima lugha ibadilike na itabadilika, tupende tusipende...." [5] (msisitizo wetu)

Sisi, ingawa tunaelewa kwamba lugha hubadilika kila mara kutokana na maendeleo ya kijamii lakini ni 'udhaifu mkubwa' kudai kwamba Kiswahili

hakiwezi kujiepusha na kuazima kwa msamiati wa kigeni kama anavyodai Broomfield.

Ni kutokana na kutaka kufanyia haki masuala kama haya kwa kuonyesha kuwa msamiati wa zamani uliosahaulika katika Kiswahili sanifu unafaa kufufuliwa na kupanuliwa kimaana kinyume na madai ya Broomfield (rejelea dondoo hapo juu), na pia kutaka kuonyesha bayana dosari na udhaifu wa TUKI na BAKITA wa kuunda msamiati wa Kiswahili, ndipo tumechagua mada hii ya uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili.

## 1.4 UPEO WA TASNIFU

Haiyumkini kwa mtu kufufua wala kuunda msamiati usiokuwa na dhana za kuyakilisha. Jambo hili linamaanisha ya kuwa ufufuaji tutakaouzungumzia katika tasnifu yetu ni wa msamiati ambao dhana zake zingalipo ila tu majina yao yalisahaulika ama 'yamekufa' kwa maana kwamba hayakufikiriwa katika Kiswahili sanifu.
Kwa kuzingatia haya tutaeleza:-

(i) Maana ya ufufuaji wa msamiati wa zamani
(ii) Sababu za 'kufa' kwa msamiati wa zamani wa Kiswahili
(iii) Sababu za ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili
(iv) Namna msamiati katika lahaja nyingine unavyoweza kuendeleza leksikoni ya Kiswahili
(v) Nafasi ya msamiati wa zamani wa Kiswahili

R.W. Langacker (1966) anadai kuwa kila lugha ina uwezo wa kujitosheleza na pale ambapo haionekani kujitosheleza hufanya kila juhudi au njia ya kujitosheleza. Maoni haya yana mashiko na

UNIVERSITY OF NAIROBI

tunakubaliana naye. Katika sura hii ya pili, tutajaribu kuonyesha kuwa njia mojawapo ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili ni kuufufua msamiati wa zamani wa lugha hii na kuupatia nafasi katika maandishi ya kila siku.

(vi) Katika sura ya tatu, tutajishughulisha na dosari na udhaifu katika taratibu za uundaji wa msamiati wa Kiswahili zinazotumiwa na TUKI.

Taratibu zitakazojadiliwa na kufanyiwa uchunguzi ni:-

(a) Ubunaji (coinage/creativity)

(b) Ukopaji/utohoaji

(c) Kaleki

(d) Uambatanishaji

(e) Akronimu

(f) Uhuluti

(g) Ukatizaji

(h) Unyambuaji

Wataalamu wengi wamejadili taratibu za kuunda msamiati wa Kiswahili. Mathalani; E. Polome (1967), J.S. Mdee (1986), C. Temu (1984), M.H. Abdulaziz (1989),P.I. Likhako (1991) n.k.

Wataalamu hawa miongoni mwa wengine walijishughulisha zaidi na kutoa vijelezi na mifano mbali mbali ya mbinu za uundaji wa msamiati. Sisi, tutafanya uchunguzi mpana wa dosari na udhaifu wa msamiati wenyewe unaoundwa na wataalamu wa TUKI na BAKITA. Tutafanya uchunguzi huu kwa kutaka kuelewa iwapo ni kweli kwamba Kiswahili kilikuwa na pengo kubwa la kimsamiati na ikiwa ni lazima kuunda msamiati wa Kiswahili au msamiati kiasili tayari ulikuweko ambao

TUKI wangefaa waupekuwepekuwe miongoni mwa Waswahili wenyewe na kuupata. Ni matumaini yetu kwamba uchunguzi wa makini katika suala hili utasaidia katika kujitokeza na nia ifaayo zaidi ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili na hivyo kuimarisha lugha hii.

(vii) Mabadiliko na upoteaji wa maana katika maneno yenye asili ya kigeni

(viii) Tatizo la maneno yanayokubalika kwa watumizi na wataalam wa lugha ya kiswahili

(ix) suluhisho

Masuala yote yatakayojadiliwa yatafanywa kwa makini katika kutaka kudhihirisha na kuthibitisha kuwa Kiswahili kinaweza kujitosheleza na kujiendeleza mumo kwa mumo kwa kufufua msamiati kiasili uliosahaulika. Kazi yetu itajibana katika taaluma ya fasihi ingawa mifano fulani za msamiati wa sayansi (hasa kemia na bayolojia) utatolewa katika kuonyesha palipo udhaifu wa TUKI na BAKITA ikihitajika kufanya hivyo.

## 1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Wataalamu ambao wamewahi kushughulikia msamiati wa zamani wa Kiswahili (ama kuutumia katika kazi zao) na ni muhimu kwetu kama tutakavyoeleza baadaye ni:- S.A. Nabhany (1982), G. Miehe (1979), R. Klein-Arendt (1987), K. wa Mutiso (1985), H.M..Mbega (1976: 1984), A. Nassir (1972) M.H. Abdulaziz (1976).

Kabla hatujazungumzia kazi moja moja ya wataalamu hawa, izingatiwe kwamba katika sehemu inayohusu taratibu za uundaji wa msamiati wa Kiswahili, kazi ya wataalamu wafuatao ni muhimu sana kwetu:

C.W. Temu (1972), E. Polome (1967), M.H. Abdulaziz (1987), K.B. Kiingi (1982: 1984: 1989: 1992), A.Mukhwana (1988), H.J.M Mwansoko (1990), K. Mutahi (1986), D.W.M. Njeru (1990), P.I. Likhako (1991).

A. Mukhwana katika kuchangia suala la uundaji wa msamiati wa Kiswahili yuasema:

> "... Kiswahili ni lugha na ikiwa haina msamiati wa kutajia kifaa fulani jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua katika lahaja zote za lugha hii"[6]

Naye R. Besha (1972) anashikilia kwamba:

> "... Si lazima lugha ichukuwe maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya la kueleza. Maneno yenyewe ya lugha yanaweza kupanuliwa."7

Maoni ya wataalam hawa yana uzito na tunakubaliana nao. Kwa kuyatafuta na kuyabukua maneno kiasili katika lahaza za Kiswahili panaweza kupatikana maneno hayo bila shaka.
Kwa mfano:-

| Msamiati wa zamani | | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|
| maloleo | ———— | macho |
| wakwasi | ———— | matajiri |
| mafumo | ———— | mikuki |
| mwango | ———— | sauti |
| biramu | ———— | bendera |
| vumba | ———— | harufu |

C.W. Temu (1972), E. Polome (1967), M.H. Abdulaziz (1987), K.B. Kiingi (1982: 1984: 1989: 1992), A.Mukhwana (1988), H.J.M Mwansoko (1990), K. Mutahi (1986), D.W.M. Njeru (1990), P.I. Likhako (1991).

A. Mukhwana katika kuchangia suala la uundaji wa msamiati wa Kiswahili yuasema:

> "... Kiswahili ni lugha na ikiwa haina msamiati wa kutajia kifaa fulani jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua katika lahaja zote za lugha hii"[6]

Naye R. Besha (1972) anashikilia kwamba:

> "... Si lazima lugha ichukuwe maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya la kueleza. Maneno yenyewe ya lugha yanaweza kupanuliwa."[7]

Maoni ya wataalam hawa yana uzito na tunakubaliana nao. Kwa kuyatafuta na kuyabukua maneno kiasili katika lahaza za Kiswahili panaweza kupatikana maneno hayo bila shaka.
Kwa mfano:-

| Msamiati wa zamani | | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|
| maloleo | ——— | macho |
| wakwasi | ——— | matajiri |
| mafumo | ——— | mikuki |
| mwango | ——— | sauti |
| biramu | ——— | bendera |
| vumba | ——— | harufu |

Ni kweli usiopingika kwamba hakuna lugha isiyo na maneno ya kigeni, lakini ni ukweli pia kwamba si lazima lugha ikope maneno ya kigeni. Pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka Kiswahili chenyewe, na tubuni. Kwa namna hii Kiswahili hakitachukuliwa na baadhi ya wataalamu kuwa ni pungufu kwani chaweza kujitosheleza na kujiendeleza mumo kwa mumo. Kwa hivyo, tunashikilia mtazamo kwamba, ingawa ukopaji ni tabia mojawapo ya lugha kwa ujumla tusiyoweza kuikanusha, wala si madhumuni yetu kufanya hivyo, katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili suala la ufufuaji wa msamiati wa zamani wa lugha hii lizingatiwe na wataalamu wa Kiswahili. Jambo la kupunguza ukopaji katika Kiswahili litawabidi wanaleksikografia wa Kiswahili, kama anavyodokeza K.B. Kiingi (1992), wafikirie zaidi. Pana msamiati wa zamani mwingi uliosahaulika ambao ukifufuliwa na kupanuliwa kimaana utaendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

S.A. Nabhany (1982) amekusanya msamiati wa zamani ufuatao:

| Kiswahili/kingozi | | Kisanifu |
|---|---|---|
| kobela | ——— | dhamana |
| matayo | ——— | lawama |
| mkata | ——— | masikini |
| ng'aŋdu | ——— | dhahabu |

Mtaalamu huyu anadokeza kuwa haya ni baadhi ya maneno yawezayo kutumiwa katika Kiswahili badala ya kutumia ya Kiarabu au Kiingereza. Tunakubaliana na maoni ya mtaalamu huyu. Kwa hakika uchunguzi wa Nabhany umeonyesha kuwa uwanja wa msamiati wa zamani wa Kiswahili uliosahaulika katika Kiswahili sanifu ni

mpana sana na ukifufuliwa na kupewa matumizi mapya, bila shaka utaendeleza leksikoni ya lugha hii ya Kiswahili.

Anavyodai Nabhany mwenyewe[8] ni kwamba amechunguza lahaja za kiamu, kipate, kisiu na kitikuu pakee. Sisi uchunguzi wetu hautajifunga katika lahaja hizi tu bali utazama zaidi. Aidha, tutajishughulisha na msamiati kiasili wa Kiswahili katika sehemu ya pwani ya Kenya (na ya Tanzania wakati ukituruhusu) bila ya kujibana katika lahaja nne tu kama alivyofanya mtaalamu huyu.

Hata hivyo, kazi yake ni muhimu kwetu kwa maana kwamba ametuwekea msingi ambao tunataka kuujengea.

Kazi ya K. wa Mutiso (1985) pia ni muhimu kwetu. Mtaalamu huyu katika kushughulikia Hurafa na uyakinifu katika Hamziyyah amekusanya msamiati wa zamani wa Kiswahili. Mathalani:

| Msamiati wa zamani | Kiswahili sanifu |
|---|---|
| aga | sahau |
| ambiyai | mitume |
| arikabuti | buibui |
| nyuni | ndege |
| munyu | chumvi |
| ulili | malazi |
| nudama | majuto |

Hata hivyo, ingawa utafiti wetu pia utajibana zaidi katika taaluma ya fasihi kama alivyofanya K. wa Mutiso, lakini sisi tutachunguza

na kujishughulisha na masuala haya kwa undani zaidi kwa kuangalia namna msamiati wa zamani unavyoweza kufufuliwa na kupewa matumizi mapya kama njia mojawapo ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili.

R. Klein-Arendt (1987) aliweza kuchukua mtazamo mzuri kwa kuimulika kazi ambayo ilikuwa imekimbiliwa na wataalamu wengi. Alifanya uchunguzi wa msamiati wa zamani, na alijitokeza na msamiati ufuatao:

| Kiongozi/msamiati wa zamani | Kiingereza |
|---|---|
| mtima | heart |
| mwanzi | friend |
| ninga | eye |
| egema | ask |
| elupe | white |

(Taza a R. Klein-Arendt 1987:202)

Hata hivyo, Klein-Arendt alishughulikia zaidi Kingozi, sisi katika utafiti wetu tutazama zaidi katika Kiswahili cha kisasa kwa kuchunguza ukale wake.

Ni maoni yetu kwamba uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili kwa kufufua msamiati wa zamani uliosahaulika katika Kiswahili sanifu ni suala ambalo 'halijatendewa haki'. Sisi tunataka kwa hivyo, kulipigia mbizi zaidi.

HAIPOTHESIA

1. Njia mojawapo ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili ni ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili

2. Ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili ambao haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu ni msingi wa ukuzaji, upanuaji na uundaji wa msamiati katika Kiswahili.
3. Kiswahili kama lugha yoyote ile kinaweza kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

.7 MSINGI WA KINADHARIA WA TASNIFU

Nadharia tutakayoitumia ni ile ya PEGITOSA. Nadharia hii imeasisiwa na K.B. Kiingi (1992). Neno PEGITOSA limebuniwa na mtaalamu huyu mwenyewe na linatokana na maneno ya Kiingereza yafuatayo:-

P - Precision (udhahiri)

E - Economy (iktisadi)

G - Generativity/productivity (uzalishaji)

I - Internationality (umataifa)

T - Transparency (Uangavu)

O - Anti-Obscenity ( (si) chafu) (utusani )

S - Systemicity (utaratibu maalum)

A - Attitudanal Acceptability (ukubalifu)

Nadharia hii inasisitiza ya kwamba katika ufufuaji ama uundaji wa msamiati ni lazima mwanaleksikografia azingatie vigezo hivi vinane, hivyo inatuongoza katika kukubali au kukataa msamiati fulani wa Kiswahili.

UDHAHIRI (Precision)

Sifa moja muhimu katika ufufuaji na uundaji wa msamiati ni kwamba sharti utoe au ulenge maana ya dhana inayonuiwa kwa udhahiri bila

utata. Mfano wa msamiati ambao hauzingatii kigezo hiki ni kama vile:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| glacier | barafuto (barafu kama mto) |
| ice | barafu |
| climate | tabia ya nchi Tol. 3:26 |
| Holland | Uholanzi Tol. 2:20 |
| Netherlands | Uholanzi Tol. 2:20 |
| Engineer | Ufundimitambo (Uhandisi) |
| Mechanics | Ufundimitambo |

Hata neno Chuo Kikuu (University) halina udhahiri. Chuo Kikuu ni "kitabu kikubwa" kwa vile:-

Chuo = Kitabu au darasa (Kiarabu)

Kikuu = Kikubwa

Neno ndaki lina udhahiri kuliko Chuo Kikuu.

University = ndaki (mahali pa kusoma kwa undani zaidi)

IKTISADI (Economy)

Kigezo hiki kinamaanisha ufupishaji wa msamiati kikundi kwa kuviunga vipashio tenzi vya msamiati huo ili kupata msamiati mfupi au neno moja lenye mkato. Mfano,

UKIMWI - Ukosefu wa Kinga mwilini

SHAHATA - Shirika la habari la Tanzania

HOMOKE - Homoni ya kike

NYAMBIZI - Nyanyumi mbizi (submarine)

mfano wa msamiati wa zamani unaozingatia sifa ya iktisadi ni:

Hakiri ——— mnyenyekevu

njeo ______________ nyakati

kupeja ______________ kudharau

nzi ______________ samaki (Nswi?)

Katika kiswahili pana haja ya mkato.

UZALISHAJI (Generativity)

Mofimu/mofu inayojitokeza zaidi katika maneno mengi huchukuliwa kuwa ni zalishi. Kwa mfano, katika Kiswahili mofimu '-isha' ni zalishi. Tazama,

> Kusanifisha, kusumakisha, kuoksidisha, kuidadisha, kutaifisha, kumasikinisha, kuboresha.

Kigezo hiki cha nadharia ya PEGITOSA kinaonyesha kuwa pana haja ya kufufua mofimu zalishi za Kiswahili ambazo zilikuwa zinakaribia kufa kama '-isha'na kuzitumia katika kuunda msamiati wa Kiswahili na hivyo kurahisisha mawasiliano.

UMATAIFA (Internationality)

Inamaanisha kwamba si lazima msamiati wa kisayansi uwe ni wa Kigiriko - Latini lakini umataifa matumizi ya msamiati ni lazima ujitokeze katika alama (symbols) na ukatizaji (abbreviation). Kwa mfano,

| alama za kimataifa | msamiati usio wa kimataifa |
|---|---|
| (H) | haidrojeni |
| (O) | oksijeni (mwai) |
| (Cu) | kopa (shaba) |
| (Au) | dhahabu, uuri, ng'andu |

Ni alama tu kama vile (H), (O), (Au), ambazo zimesanifishwa kimataifa na wala si msamiati, hivyo pana haja ya kuunda ama

kufufua msamiati 'unaofaa' zaidi (na unaoweza kukubalika kimataifa) kulingana na kigezo hiki cha umataifa.

UANGAVU (Transparency)

Uangavu wa msamiati hutegemea mtumiaji wake,

Kwa mfano,

| A | B |
|---|---|
| malolea | macho (eyes) |
| tenga | kamati (committee) |
| kitenga | sabu-kamati (sub-committee) |
| fumo | mkuki (spear) |
| elimunyota | astronomia (astronomy) |

Wasomi watachukulia maneno ya kundi la A yaani malolea, tenga, kitenga, fumo, elimunyota, kuwa si ma angavu yakilinganishwa na maneno ya kundi la B. Kadhalika, 'akina yakhe' au wazungumzaji wa Kiswahili wasio wasomi wataona kamati, mkuki, astronomia kuwa hayana uangavu zaidi.

Kwa maoni yetu, msamiati wa kundi la A ni angavu zaidi kuliko wa kundi B. Kwa mfano, neno tenga latokana na 'watu waliojitenga' (wametengwa) kufanya kazi fulani. Kwa hakika neno hili ni angavu zaidi kuliko kamati au halmashauri.Kwa ujumla, msamiati unaobuniwa ama unaofufuliwa ni angavu zaidi kushinda unaotoholewa na kuswahilishwa.

(SI)-CHAFU (Anti-Obscenity)

Heshima au adabu ya lugha ya Kiswahili haina budi kuzingatiwa na wanaleksikografia. Msamiati mchafu uepukwe na pahala pake paundwe/

pafufuliwe msamiati mwingine wenye adabu au 'usiosinya' watumiaji lugha ya Kiswahili. Mfano,

| msamiati mchafu/mkali | msamiati wenye adabu zaidi |
|---|---|
| mavi | (faeces) kinyesi, makutu, majivi |
| mboo | (penis) ume, kizaliya (that which makes a woman pregnant) |
| kuma | (vagina) uke |
| mkundu | (anus) - ngoko, unyuma |
| matako | kikaliyo, mabogi |
| kinyangarika | mhalifu |

Haya ni baadhi ya maneno machafu ama makali katika Kiswahili.

UTARATIBU MAALUM (Systemicity)

Utaratibu maalum wa kufufua msamiati kiasili na kuunda msamiati mpya wa Kiswahili ni sifa inayosisitizwa na kigezo hiki. Msamiati haufai kuundwa ama kufufuliwa 'vivi hivi tu', pana haja ya kuzingatia mfumo ulio sawa wa kutekeleza suala hili. Tazama 'inconsistence' katika msamiati ufuatao na jinsi dhana ya 'hydro' imetafsiriwa na wataalamu wa TUKI.

| | | Kwa nini isiwe |
|---|---|---|
| hydrotropism | - ubadilihali | - haidrotopisimu |
| hydrophyte | - yungiyungi | - haidrofita |

kama ilivyo katika

| | |
|---|---|
| adrogen | - adrojeni |
| artery | - ateri |
| epiglottis | - epiglotisi |
| hormone | - homoni? |

UKUBALIFU (Acceptability)

Ukubalifu hutegemea jamii - tumizi - lugha yenyewe. Jamii ambazo hazioni ubaya wowote katika ukopaji hukubali msamiati uliyokopwa. Ni matumaini yetu kwamba watumiaji wa Kiswahili watakataa msamiati uliokopwa pale ambapo pana msamiati wa zamani mwafaka wa kutumiwa. Kadhalika, litakuwa jambo la busara watumiaji wa Kiswahili kuukataa msamiati ulioundwa kiholela na TUKI. Kulingana nadharia hii,'msamiati bora' ni ule unaofaulu jaribio la PEGITOSA kwa kupata alama nyingi; (12 $\leq$ P ($\bar{X}$) $\leq$ 20). Kwa mfano,

| | | P | E | G | I | T | O | S | A | (alama) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.a | Elimuviumbe | 0 | 1 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2.5 |
| 1.b | Bayolojia | 2 | 2 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5.5 |
| 2.a | Televisheni | 2 | 1 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4.5 |
| b | runinga | 4 | 3 | 0.5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 9.5 |
| 3.a | njeo | 2 | 4 | 0.5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 8.5 |
| b | wakati | 2 | 2 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5.5 |
| 4.a | liwaa | 4 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| b | sahau | 2 | 2 | 0.5 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 6 |
| 5.a | mikuki | 2 | 2 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4.5 |
| b | mafumo | 4 | 2 | 0.5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 8.5 |

Msamiati bayolojia, runinga, njeo, liwaa, na mafumo umefaulu jaribio la PEGITOSA kwa kupata alama za juu hivyo kulingana na nadharia hii ndio 'unafaa' kutumiwa.

Aidha, baadhi ya magunge wa lugha ya Kiswahili wamewahi kutatizika na msamiati kama vile adabu na fasihi kwa maana ya 'Literature' (Gibbe 1977 6:1), poligon na pembenyingi kwa maana ya 'polygon' n.k.

C.W. Temu (1983) anadai kuwa 'polygon' kutoitwa poligoni ni badiliko linalolingana na hatua ya lugha ya Kiswahili ya kutaka kujitawala na kuachana na ugeni, madai ambayo kwa maoni yetu hayana uzito wowote. Wataalamu wa TUKI wanapoulizwa ni kwa nini patumike:-

uhandisi badala ya ufundimitambo

atomu badala ya tonoradi

chuo kikuu badala ya ndaki

dhambi badala ya athima

vita badala ya kondo

Koleji (college) badala ya uwoti wao hutoasababu kwamba msamiati wa kundi la pili 'hauna mwonjo' zaidi ama hauna usayansi ndani yake, madai ambayo pia ni potovu kulingana na tunavyoonyeshwa na nadharia hii ya PEGITOSA.

Kwa ujumla, tutaitumia nadharia ya PEGITOSA kwa sababu tatu:-

Kwanza, itatusaidia kutambua msamiati wa zamani unaofaa zaidi kufufuliwa na kutumiwa katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili.
Pili, itatuelekeza katika kutambua sababu za kutaka kuchimbua au kufufua na kuupatia msamiati wa zamani matumizi mapya kama nia mojawapo ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili.
Mwisho, itatuongoza katika kutambua udhaifu wa baadhi ya msamiati unaoundwa na TUKI. Kutokana na sababu hizi hatuna budi kuitumia nadharia ya PEGITOSA.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Tutafanya utafiti wetu kwa kutumia njia kadha wa kadha

(i) Tutashirikisha kimawazo watu wenye ujuzi juu ya muda yetu kwa kuwahoji.

(ii) Tunanuia kutimia hojaji/musuala (questionnaire) Maswali yatatayarishwa ya kuwauliza wataalamu na magunge wa Kiswahili huko pwani ya Kenya, Nairobi na kuingineko. Tutawahoji wazee wa pwani ya Kenya. Tumechagua wazee kwa sababu wao ni watu ambao wamekomaa kimawazo mbali na kuwa wana tajiriba pana ya maisha na utamaduni wao.[9]

Hali kadhalika, tumechagua sehemu ya pwani ya Kenya (au na hata pwani ya Tanzania wakati ukituruhu kwa sababu ndiko 'uswahilini'[10]

(iii) Aidha, uchunguzi wa kimaktaba utafanywa. Tutasoma vitabu, magazeti, na majarida mbalimbali ya Kiswahili. Kwa kuzingatia njia hizi tatu tunatarajia kujitokeza na data itakayotusaidia katika utekelezaji na ufikiaji wa madhumuni yetu.

1.9 TANBIHI

1. Ni neno ambalo limebuniwa hivi majuzi na K.B. Kiingi mtaalamu huyu ametumia mbinu ya akronimu kuunda neno PEGITOSA. Tazama katika pendekezo lake la utafiti A. D - ILTT A Theory of Scientific Terminology (1992).

2. A. Baruwa (1979) 'Taifa weekly' Nov. 24, 1979.

3. N.I. Sharif Tungo Zetu uk. wa 28

4. Dondoo hili limetolewa katika K.B. Kiingi (1989:146) ambaye amemnukuu H.M. Abdulaziz (1985:195).

5. Tazama G.W. Broomfield (193)) katika Historia ya usanifishaji wa kiswahili Mbaabu, I (1991) uk. wa 34.

6. A. Mukhwana Tasnifu ya B.A. 1988 uk wa 61.

7. R. Besha (1972) katika Kiswahili juzuu 49/2 TUKI uk. wa 23.

8. Kulingana na maelezo ya S.A. Nabhany (1990) tulipokutana naye kule Lamu.

9. W.J. Samarin Field Linguistic (1967) ameyajadili masuala haya kwa kirefu.

10. Kama 3 hapo juu lakini uk. wa 27.

# SURA YA PILI

## 2.1.0 Utangulizi

Lugha ni chombo kilichoundwa na wanadamu kwa ajili ya matumizi yao. Kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha na binadamu. Lugha kama binadamu, ina uhai. Lugha huzaliwa, hulelewa, hukua, huzeeka, na hufa na hata hufufuka kwa wakati mwingine.

Wanaismu na wanaleksikografia wengi wamejishughulisha na kukua kwa lugha pasi na kutilia maanani kufufuliwa kwa msamiati wake mwingi wa zamani uliosahaulika, utaratibu ambao ni moja wapo wa hatua za kuendeleza lugha.

Kuhusu suala hili A. Mukhwana (1988:61) yuasema:

> "...Kiswahili ni lugha na ikiwa haina msamiati wa kutajia kifaa jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua (kufufua) katika lahaja zote za lugha hii.... ikiwa kwa bahati nzuri, mojawapo ya lahaja za kiswahili ina neno la kutajia kifaa hicho na lichukuliwe mara moja".[1]

Kutokana na kauli ya Mukhwana wanaismu na wanaleksikografia watakiri kwamba suala hili la ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili wa lahaja nyingine ambao haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu si ligeni ila tu linahitaji kupewa uzito zaidi. Njia hii ya ufufuaji ni muhimu kwa sababu inahifadhi U - Afrika wa lugha ya Kiswahili mbali na kudhihirisha kwamba ukwasi wa lugha hii ya Kiswahili ni pana sana na tunatumia sehemu ndogo tu ya msamiati wa Kiswahili.

Mukhwana anaendelea kupendekeza kwamba

> "Ikiwa lahaja za Kiswahili hazina msamiati unaotafutwa itatubidi <u>tukope</u>"[2] (msisitizo ni wetu) (1988:62).

Hapa sisi tungependa kuchukua msimamo uliotofauti na huu. Badala ya kukopa, tunapendekeza tunyambue mofimu za Kiswahili, tubuni msamiati mpya na tufufue msamiati wa zamani wa Kiswahili na kuupanua kimaana. Masuala haya matatu yaani unyambuaji wa mofimu za Kiswahili, ubunaji na ufufuaji kwa maoni yetu, yatapunguza ugeni mwingi katika Kiswahili bali na kukifanya kiswahili, kama lugha yoyote ile, kiweze kujisimamia chenyewe na kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

H.S. Olson (1972:9) yuasema "lugha inapokopa huonyesha uwezo wake wa kuweza kujimudu" [3]

Wataalamu fulani wamependekeza kwamba iwapo Kiswahili hakina msamiati unaotakikana basi tukope kutoka kwa lugha za Kibantu. Wengine wamependekeza ukopaji kutoka lugha za Kigiriko - Latin. Suala la wapi pa kukopa si lengo letu hasa. Tunalosema sisi ni kwamba ukopaji kutoka lugha za kigeni usiendelezwe kwa sababu kwanza, ukopaji huo unafanywa bila utaratibu maalum (kama tutakavyo eleza baadaye) pili, unakiondolea U - Afrika na uswahili wake.

Anavyosema R. Ohly (1987) ni kwamba ukopaji kutoka lugha za kigeni, ukubalike iwapo hakuna njia nyingine ya kuendeleza leksikoni ya lugha husika na sisi tunakubaliana na maoni haya kwa vile yana mashiko.

Ni maoni yetu kwamba ndoto ya kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya usomi barani Afrika na hatua ya kuifanya lingua franka ya bara la Afrika itafikiwa tu iwapo hazina ya lugha hii itachungiwa zaidi kwa kutumia njia zifuatato: Kwanza, kwa kutumia utaratibu unaopendekezwa na Nabhany wa kuunda msamiati kwa kutafsiri maana ya viungo vya maneno yenye maana kutokana na lahaja zingine za Kiswahili, pili kwa kutumia unyumbuaji wa mofimu za Kiswahili kama anavyopendekeza K.B. Kiingi, na tatu kwa ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili ambao haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu.Mbinu hizi ni miongoni mwa zile ambazo, kwa maoni yetu, zitasaidia katika kuikuza lugha hii katika mwelekeo mmoja badala ya ukopaji au tafsiri sisisi ambayo hujiporoja lugha ya Kiswahili.

### 2.1.1 Maana ya 'Ufufuaji' (Revival) wa msamiati wa zamani wa Kiswahili

Ili kazi yetu ieleweke barabara hatuna budi kutoa kijelezi cha 'ufufuaji'.

Dhana ya ufufuaji inaelezwa na Kamusi ya Kiswahili sanifu kwamba ni "tendo la kurudishia uhai viumbe baada ya kufa..."

> ama "utumiaji upya wa, ukubalifu au urejeshaji wa uhai katika kiumbe baada ya kufa".

Maana hii ya ufufuo au ufufuaji kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu tunaweza kuipanua kwa kusema kwamba 'ufufuaji' ni kurudisha katika matumizi msamiati ambao haukufikiriwa katika kiswahili sanifu.

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi, lugha kama binadamu ina uhai, huzaliwa, hukua, hufa na hufufuka. Ufufuaji kwa hivyo ni sifa mojawapo ya lugha. Katika kazi hii, ufufuaji kama urudishaji katika matumizi wa msamiati, ina maana kuwa msamiati huo upo, lakini hautumiki ama haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu. Msamiati huo ambao ulisahaulika, "umekufa" unapatikana katika makamusi ya zamani, kazi za kifasihi kama vile Utenzi wa Hamziyah, na katika mabuku mengi ya lugha ya kiswahili ya zamani kama ya Fumo Liyongo n.k.

Ni muhimu ifahamike, kwa manufaa ya kueleweka kwa kazi hii, kuwa 'ufufuaji' mbali na kuwa unamaanisha urudishaji katika matumizi msamiati (recycling/revival), wa zamani uliosahaulika, pia unahusu msamiati katika lahaja nyingine za Kiswahili ambao unaweza kusaidia kuendeleza leksikoni ya Kiswahili.

Kwa usemi mwingine, uchunguzi wa vipi msamiati katika lahaja nyingine za Kiswahili unavyoweza kusaidia kuendeleza Kiswahili utafanywa katika kushughulikia mada yetu.

"Kufa" kwa msamiati kuna maana ya kusahaulika ama kutofikiriwa kwa msamiati huo ambao licha ya kuwepo kwake, hautumiki katika maandishi ya kila siku. Suala hili linatuelekeza katika kueleza sababu za 'kufa' kwa msamiati wa zamani wa Kiswahili.

### 2.1.2 Sababu za "kufa" kwa msamiati wa zamani wa Kiswahili

Wanaleksikografia na wataalamu wa Kiisimu watakiri kwamba suala la 'kufa' kwa msamiati si ligeni katika maisha ya binadamu. Mwanadamu aghalabu huunda maneno mapya mara anapoona au anapobuni

dhana mpya. Maneno au msamiati unaoundwa na binadamu mara nyingi baada ya upito wa kiwakati "hufa" au husahaulika ukawa hautumiki tena. Jambo hili hutokana na sababu kadha wa kadha. Sababu mojawapo muhimu ni kwamba lugha hupanuka kila uchao kulingana na ukuaji wa mahitaji ya binadamu katika jamii. Kwa usemi mwingine, maendeleo ya haraka katika nyanja mbalimbali za maarifa ya binadamu na madadiliko ya kijamii kwa ujumla ni sababu moja ambayo imemlazimisha binadamu kutoyatumia na hivyo 'kufa' kwa msamiati wa zamani wa Kiswahili

Isitoshe, msamiati hufa kutokana na kupotea kwa dhana inayowakilishwa na msamiati huo. Kwa mfano, katika jamii ya wawindaji dhana mbali mbali zinazohusiana na mwindaji zikipotea labda kwa sababu ya kupigwa marufuku na serikali shughuli za uwindaji wa wanyama msamiati wa kuziakilisha dhana hizo bila shaka 'utakufa'.

Aidha, kuna sababu za kihistoria ambazo husababisha kusahaulika kwa msamiati wa zamani. Lugha ya Kiswahili, kama historia inavyotueleza, ni lugha ambayo imeingiliana sana la lugha zingine za ulimwenguni. Mwingiliano lugha huu ulisababishwa na uhamiaji wa kimaeneo ambapo wageni hasa Waarabu waliingiliana na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki kwa muda mrefu. Mwingiliano huu uliathiri sana leksia au msamiati wa zamani wa Kiswahili ambao ulipuuzwa labda kimaksudi au bila kujua, na kadri wakati ulipopita, ndipo msamiati huo 'ukafa'/ukasahauliwa na pahali pake pakatumika na wageni. Kwa mfano,

| <u>Kiswahili cha zamani</u> | <u>Kisanifu</u> |
|---|---|
| <u>kobela</u> | dhamana |
| <u>shokori</u> | stihizai |

| | |
|---|---|
| mweni' | damu |
| nswi | samaki |
| mwiya | wakati |
| penyenye/ngea | nafasi |
| goni | juha |
| uya | rudi |

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba msamiati mwingi wa zamani wa Kiswahili 'ulikufa' kwa sababu ya mwingiliano wa lugha hii na lugha nyinginezo za ulimwengu suala ambalo lilisababisha msamiati wa kigeni kupendelewa na msamiati wa zamani wa lugha hii 'kushushwa hadhi' kwa kutofikiriwa katika Kiswahili sanifu.

Fauka ya hayo, sababu nyingine ya kusahaulika au 'kufa' kwa msamiati wa zamani latokana na kuundwa kwa msamiati mwingine 'unaofaa' zaidi badala ya uliokuweko kabla. Msamiati uliochakaa aghalabu hupuuzwa. Kwa mfano, maneno kama vile liwaa (sahau), sede (kupatana) na mede (kukimbilia hifadhi) ni ya zamani yaliyotumiwa hasa na watoto wa sehemu za Lamu. Maneno hayo yamekufa kwa sababu mengine yaliyo 'bora' zaidi yameundwa na yametumiwa badala ya hayo ambayo inadaiwa kwamba yamechakaa.

Hoja hii inaenda sambamba na kasumba ya wanajamii fulani ambao hufikiria kwamba mambo yote ya 'maana' ni lazima yaelezwe kwa lugha ya kigeni hasa Kiingereza. Wanadai kuwa msamiati 'unaofaa' zaidi ni ule wenye asili ya kigeni na ambao umetoholewa na kuswahilishwa moja kwa moja. Watu kama hao hudai, kwa mfano kwamba:-

Viruzi 'linafaa' zaidi kuliko Viini

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| jenusi | 'linafaa' | zaidi | kuliko | ndugu |
| spishi | " | " | " | aina |
| televisheni | " | " | " | runinga |
| dhahabu | " | " | " | ng'andu |

madai ambayo, kwa maoni yetu ni potovu mno na hayana mashiko.

M.M. Mulokozi (1975) ambaye anajaribu kuonesha kuwa matumizi ya msamiati wa asili ya Kiarabu katika kuendeleza fikira fulani kwa Kiswahili (kwa sababu eti ndio 'unaofaa' zaidi) ni ukoloni unatueleza haya,

> "Fikira hizi za kikoloni, kwa hakika zinajitokeza katika lugha. Baadhi ya tenzi zilizoandikwa katika wakati huu zimejaa maneno ya Kiarabu.... Hata haimkini kwa mtu asiyejua Kiarabu kufahamu yanenwayo". [4]

Tunakubaliana na Mulokozi kwamba (hata katika ushairi) si lazima kutumia msamiati wenye asili ya kigeni tufufue na kutumia msamiati wa zamani wa Kiswahili.

Kwa usemi mwingine, kutotumika kwa msamiati kama vile:-

| | |
|---|---|
| ulili | (kitanda) |
| manza | (dhambi) |
| ganio | (neema) |

ni kwa sababu ya kuundwa kwa msamiati mwingine 'unaofaa' zaidi badala ya huo uliokuwepo mbeleni.

Aidha sababu nyingine ya kufa ama kutofukuriwa kwa msamiati wa

zamani ni kutohitajika kwa msamiati huo. Labda swali la kujiuliza hapa ni kwa nini msamiati fulani usihitajike? Kwa mfano, ni kwa nini tutumie neno <u>fasihi</u> badala ya <u>adabu</u> (literature).

Neno <u>adabu</u> lina maana ya "Literature". Baadhi ya wataalamu wa fasihi walipolileta katika lugha ya Kiswahili halikuzigusa hisia za wataalamu wengi (Amri Abeid (1957) wa lugha ya Kiswahili. Neno hili limewahi kupiganiwa sana na baadhi ya magunge wa lugha ya Kiswahili (Gibbe 1977 6:1). Neno 'fasihi' lilipoingia uwanjani, lilipokelewa mara moja na kulihinikiza ama kulifanya neno 'adabu' lisahaulike/life. Sababu mojawapo inayotolewa kwa kufa kwa neno "adabu" ni kwamba hali-kuhitajika ama halina 'mwonjo' ndani yake. Hoja kwamba msamiati hautumiki au haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu kwa sababu hauna mwonjo, am haukuhitajika, haina uzito wowote. Msimamo wetu ni kwamba msamiati unaweza 'kufa' iwapo hauzingatii baadhi ya sifa za PEGITOSA*.

Izingatiwe hapa kwamba kigezo cha <u>udhahiri</u> (Precision) ni muhimu katika kutumia ama kutotumiwa kwa msamiati wa zamani wa Kiswahili. Tukumbushane kwamba kutofikiriwa kwa msamiati mwingi wa zamani wa Kiswahili katika Kiswahili sanifu si kwamba msamiati huo haukuhitajika, ila ni kwa sababu labda haukuwa na udhahiri ndani yake yaani haukulenga wazi maana ya dhana iliyonuiwa kwa udhahiri bila utata. Kwa mfano,

> <u>munyu</u> kwa maana ya chumvi (salt)
> si dhahiri kwa vile <u>munyu</u> ni '<u>iodine</u>' kwa
> mujibu wa uchunguzi wa Kitsao J. (1992).

* rejelea sura ya kwanza kwa maelezo zaidi.

Naye Nabhany ana maoni kwamba "chuo kikuu" (University) si dhahiri kwa vile chuo ni kitabu (kiarabu),

kikuu ni kikubwa

hivyo chuo kikuu ni kitabu kikubwa. Nabhany anapendekeza patumike ndaki (mahali pa kusoma kwa undani zaidi). Mawazo ya Wataalamu hawa yanahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Mfano zaidi, neno elimumwili (anatomy) halilengi dhahiri taaluma ya 'anatomy'. Elimumwili ni neno linaloweza kusimamia uchunguzi wowote kuhusu mwili-magonjwa, viungo vya mwili n.k. hivyo ni msamiati wa jumla mno kwa sababu mwili unahusisha taaluma nyingi sana. Hivyo pana haja ya kubuni neno lingine ama patumike anatomia ambalo lina udhahiri kuliko elimumwili na katika kufanya hivyo neno elimumwili litasahaulika/litakufa. Hata hivyo hii haina maana kwamba 'elimumwili' halihitajiki, lahitajika ila halitumiki wala halifikiriki kwa sababu halina udhahiri unaohitajika na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

## Iktisadi

Lugha yoyote ile hulenga kurahisisha matamshi na mawasiliano. Kila lugha hulenga ufupi wa maneno na matamshi. Msamiati ukiwa mrefu mno hausaidii katika sifa hii au kwa hivyo si ajabu ukasahaulika. Kwa mfano neno 'nururishi' badala ya 'kipeleanguvu'

Ukimwi badala ya 'ukosefu wa kinga mwilini

(ambalo limetokana na tafsiri mkopo na kisha ufupisho)

## Uzalishi

Uwezo wa msamiati kunyambulika kwa maana ya kuongeza viambishi ili

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

kupanua maana yake ni sifa mojawapo inayoweza kusababisha 'kufa' kwa msamiati. Mfano, 'nururishi' laweza kuzalisha na kunyumbuliwa lakini 'kipeleanguvu' haliwezekani. Kunururisha, unururishaji n.k.

Umataifa

Kigezo cha kukubalika kwa msamiati kimataifa ni muhimu zaidi katika kutumika au kutotumika kwa msamiatu fulani. Aghalabu msamiati (hasa wa sayansi) umesahaulika kimataifa kwa sababu hauna misingi yake katika lugha za kigiriko-Latini. Hata hivyo, izingatiwe kwamba si lazima msamiati wa sayansi uwe wenye misingi katika lugha za Kigiriko - Latin ndipo ukubalike kimataifa. Ni alama (signs) na njia za utendaji tu ambazo zime sanifishwa kimataifa na wala si majina au msamiati unaopaswa kutumika. Hata hivyo, sifa ya ukubalifu ni muhimu sana katika uteuzi wa msamiati fulani.

Uangavu wa msamiati pia hutumiwa kama sababu mojawapo ya 'kufa' kwa msamiati. Lazima paweko uhusiano wa msamiati na maana. Msamiati usioangaza maana husahaulika. Kwa usemi mwingine msamiati mwingi wa zamani haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu kwa sababu labda haukuwa unaangaza maana. Hata hivyo, uangavu wa msamiati hutegemea mtumiaji wake. Kwa mfano,

| (1) | | (2) |
|---|---|---|
| chocheo | na | homoni (hormone) |
| ufananishi | na | analojia (analogy) |
| ndaki | na | chuo kikuu (University) |
| hama | na | nyonya (suck) |

Kuna watu wanaochukulia kuwa msamiati katika kundi la pili ni angavu zaidi kuliko wa kundi la kwanza na hivyo hawatapenda

utumike na kwa namna hii msamiati wa kundi la kwanza utasahaulika/ kufa. Ni maoni yetu kwamba msamiati unaobuniwa ni angavu zaidi kuliko unaotafsiriwa moja kwa moja kutoka lugha za kigeni.

Miiko na utamaduni

G.A. Mhina (1972) yuasema

> " Shida moja ambayo Waafrika wengi wanaelekea hawajaitambua bado ni kwamba utamaduni huenda sambamba na lugha. Kushughulikia moja bila nyingine haina maana". [5]

Tunakubaliana na Mhina kwamba kigezo cha utamaduni ni muhimu katika kushughulikia lugha. Ieleweke kwamba kwa kuwa jamii tofauti za watu zina utamaduni tofauti uliowalea, baadhi ya dhana zimekuzwa zaidi hivyo majina yao/msamiati wao umekuzwa zaidi katika lugha husika kuliko dhana ambazo hazina umuhimu wa kiutamaduni na kwa hivyo msamiati wazo umepotea/kufa.

Njia nyingine ya kueleza kigezo cha utamaduni au miiko ni kwamba msamiati wa zamani inaelekea ulisahaulika kwa sababu za miiko au aibu. Kwa kutaka kuzingatia mila au utamaduni na adabu ya lugha ya Kiswahili watumiaji lugha hii wamefanywa kukwepa kutumia msamiati mchafu.. Mfano,

| msamiati mchafu | msamiati wa adabu zaidi |
|---|---|
| mkundu | ngoko, makadi |
| mavi | mlima, kimba, makutu |
| kuma | uke |
| mboo | kizaliya, ume |
| banyani | Wahindi |

Kwa maneno mengine, msamiati mchafu huepukwa na hivyo 'hufa'. Hivyo, uchafu/ukali wa msamiati ni sababu mojawapo wa kusahaulika kwake katika lugha husika. Sababu nyingine ya kufa ama kusahaulika kwa msamiati ni ya kisiasa. Msamiati mwingi wa zamani kutofikiriwa kwake katika Kiswahili sanifu kunatokana na siasa. F.V. Nkwera (1978) kuhusu usamifishaji wa Kiswahili, yuasema:

> "....upungufu wa standard swahili unatokana na hatua ya awali kabisa ya kuichagua lugha ya kiunguja tu kushughulikiwa na kuendelezwa na kuziona lafudhi/lahaja nyingine za Kiswahili kuwa ni lahaja zisizokuwa na umuhimu mkubwa". [6]

Naye S. Chiraghdin anasema:

> "... lakini kusema kuwa hii 'standard swahili' ilivyo sasa ndiyo imetufikisha upeo wa juhudi zetu ndiko huko kujirisha vidoto tusione mbali..." [7]

Madondoo haya yanadhihirisha tu kwamba kulikuwepo upungufu mwingi wa Kiswahili sanifu uliosababishwa hasa na uchaguzi wa Kiunguja kama lugha ya pekee ya Kiswahili na kutofikiriwa kwa msamiati wa zamani upatikanao katika lahaja nyingine za Kiswahili. Upungufu huu una msingi wake katika siasa (Mkude 1989).

Kutokana na sababu za kisiasa, msamiati hubadilisha maana ama hulazimishwa kufa. Kwa mfano, maneno kama vile magendo, hayati, kachero, kunyonya, na beberu yamebadilisha kimaana.

Neno magendo ambalo latokana na'genda' maana yake asilia ni mikono ya kaa ya mbele. Kwa sasa magendo hutumiwa kwa maana ya kufanya biashara kwa njia isiyo halali. Neno kunyonya maana asilia ni

kuvuta (hasa maziwa) kinyuaji. Kwa sasa maana ambayo imetokana na siasa ni kuangamiza (exploit).

Maneno mengine ambayo yamebadilika kimaana ni masikio na kisu. Masikio katika Kiswahili cha zamani lilitumika kwa maana ya "mikono" (hands) ambayo ni ya kushikia vitu, - kusikia au kushikia yaani kukamatia vitu. Neno lililotumiwa kwa 'sikio' (ear) lilikuwa masikizi na wala sio 'masikio' kama linavyotumika sasa. Kadhalika kisu, neno asilia lilikuwa 'msu' ambacho ni kitu kama rungu (sword). Kisu chetu cha kawaida, kwa maoni ya K. wa Mutiso (1992), kilikuwa kidogo kuliko rungu, hivyo kiliitwa ki - su, 'ki' ikionyesha umbo la udogo (diminitive form) kama ilivyo katika msu - meno (saw) (rungu iliyo na meno).

Baadhi ya maneno ambayo yamechimbuka kutokana na siasa ni kama vile harambee, nyayo, kinyangarika n.k. Izingatiwe pia kwamba baadhi ya msamiati kiasili umekufa kwa sababu ya wanasiasa kutoutambua ama kuutumia vibaya hivyo kuupatia msamiati huo maana iliyo tofauti na maana yake asilia.

Temu (1983) anaziita sababu za kisiasa 'mabadiliko ya msamiati kufuatana na viongozi'. Msamiati wa Kiswahili, kwa maoni ya Temu, umekufa kufuatana na falsafa ya viongozi walioshika hatamu. Kwa mfano, kuna tofauti kati ya msamiati uliotumika kuwataja au kuwaita viongozi wa kikoloni na wale viongozi wa baada ya ukoloni. Aghalabu msamiati huathiriwa sana na falsafa ya tabaka linalotawala. Hoja hii ina mashiko na tunakubaliana naye. Ili kuipa uzito hoja hii, mtaalamu huyu anatueleza kwamba wakati wa ukoloni, tabaka lililokuwa

limeshika hatamu lilikuwa lenye madaha, kujishauna na lenye kupenda ubwana. Msamiati wao nao uliathiriwa na maringo hayo.Ona kwa mfano majina haya:

"District Commissioner" - Bwana Shauri (Mkuu wa Wilaya)

"Agricultural Officer" - Bwana Shamba (Mkuu wa kilimo au Afisa wa kilimo).

Maneno haya 'Bwana Shauri', 'Bwana Shamba' na mengine mengi kama vile boyi (mfanyikazi wa nyumbani) yamekufa kwa sababu za kisiasa bila shaka. Inafaa kueleza hapa kwamba viongozi walioshika hatamu baada ya ukoloni hawakuepuka athari na kasumba za mkoloni. Walipendelea sana waitwe 'mabwana'. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya kisiasa ya mataifa menti ya Afrika, maneno ya 'ubwana' yamekufa na nafasi yao ama imechukuliwa na maneno mengine au uwanja wake wa matumizi umetoweka.

Ama kwa hakika, ili kuendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili, panahitajika ufufuaji wa msamiati wa zamani wa lugha hii na ubunifu wa msamiati mpya wa kuwakilisha dhana mpya zinazoingia katika lugha ya Kiswahili. Wazo hili linatusukuma mbele katika kuchunguza kwa mapana na marefu sababu za ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili uliosahaulika katika kiswahili sanifu licha na kuwepo kwake katika lahaja nyingine za Kiswahili na katika kazi za kale za fasihi kama Utenzi wa Hamiziyah, Utenzi wa Al-Inkishafi n.k.

## 2.1.3 Sababu za Ufufuaji wa Msamiati wa zamani wa Kiswahili

Ili kazi hii ieleweke vyema, suala la sababu za ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili 'uliokufa' halina budi kujadiliwa hapa

R. Mukama (1989) anasema:

> "... Kiswahili kiko katika kilele cha kujikuza na kujipanua ili kumudu maendeleo ya kiuchumi, ya kisiasa na kiutamaduni. Hivyo sote bado tuko katikati ya harakati za kujiuliza maswali kama: Federal structure, anaphora, enzymology .... ni nini kwa Kiswahili"?[8]

Ni ukweli, kama anavyosema Mukama, kwamba msamiati kama 'federal structure', 'anaphora', 'enzymology' hatuwezi tukaufasiri ipasavyo kwa Kiswahili pasi na kutumia utaratibu wa kukopa kifonolojia na kimofolojia msamiati huo wa kigeni na kuuswahilisha. Utaratibu wa ubunaji wa msamiati upo na ingelikuwa bora kama wanaleksikografia wa Kiswahili wangekuwa wabunifu zaidi badala ya kuendelea kukopa na kutohoa moja kwa moja kutoka lugha za kigeni na kuchukulia

| | | |
|---|---|---|
| "federal structure" | kuwa | federali straikicha |
| "anaphora" | kuwa | anafora |
| "enzymology" | " | enzimolojia |
| "genus" | " | jenusi |
| "microphone | " | mikrofoni |
| "dynamics | " | dainamiki |

Aidha, pale ambapo mbinu ya ubunaji haitatupatia neno mwafaka, tutahitajika kutafuta miongoni mwa Waswahili wenyewe na kuupata msamiati wa zamani uliosahaulika na unaofaa kutumiwa- tuutumie. Kwa ufafanuzi zaidi, sababu mojawapo ya ufufuaji wa msamiati kiasili wa Kiswahili ni kutaka kuendeleza leksikoni ya Kiswahili. Msamiati wa zamani 'unaodhaniwa' ulikufa ukifufuliwa utatumiwa pale ambapo hapana neno mwafaka bila shaka.

J. Kitsao (1989) amegundua kwamba kuna pengo la kimsamiati katika Kiswahili na anasema:-

> "Kuhusu 'dada' na 'kaka', madhumuni yangu ni kumulika pengo lililopo katika lugha ya Kiswahili. Maana ya 'dada' ni ama ndugu mkubwa wa kike au ndugu yeyote wa kike, lakini maana ya 'kaka' katika muktadha huu ni moja tu: ndugu mkubwa wa kiume. Hii ni kuonyesha kuwa Kiswahili kina pengo linalohitaji kumezwa jino kuhusu dhana ya 'brother'...."[9](Msisitizo wetu).

Pengo la kimsamiati kama hili ambalo Kitsao analitaja, linaweza likazibwa (iwapo lipo) kwa kufufua msamiati wa zamani ambao wadhaniwa 'umekufa' ilhali bado wapatikana katika lahaja za Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, huenda pakapatikana neno 'brother' la Kiswahili. Kwa hivyo kinachohitajika,kwa upande wa TUKI, si kuunda msamiati mpya ama kutohoa neno la kigeni moja kwa moja bali kubukua na kufufua msamiati wa zamani ambao unafaa kutumiwa pale ambapo pana pengo ama hapana neno mwafaka.

.../42

F.M.V. Nkwera (1978) kuhusu suala la uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili yuasema:

> "... waandishi na wataalamu wote wa Kiswahili wana dhima kubwa ya kufanya utafiti unaostahili ili lugha hii ipanuliwe kimsamiati ..... na itosheleze haja ya kuelezea na kufundishia mitaala yote ya kisayansi na ya kijamii. Katika juhudi hizo za kukuza Kiswahili, ni bora chemchemi au chimbuko la msamiati liwe Waswahili wenyewe. Ndiko kusema: wakati wa kufanya utafiti huo mwelemeo mkubwa hasa katika kujenga na kupokea msamiati mpya uwe kwenye
>
> (a) Lugha zenzake za Kiswahili
> (b) Lugha za makabila ya kibantu, kuliko kuelekea kwenye lugha za kigeni kama inavyofanywa sana leo."[10] (Msisitizo ni wetu).

Bila shaka, dondoo hili linadhihirisha umuhimu wa ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili uliosahaulika katika Kiswahili sanifu. Tunakubaliana na Nkwera kwamba wanaleksikografia wa Kiswahili wana dhima ya kuendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili kwa kupanua msamiati wenyewe wa lugha hii. Iwapo Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) itataka kufamikiwa vizuri zaidi na kwa urahisi zaidi katika kazi zake za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, itafaa itambue kwamba kinachohitajika, kama anavyodokeza Nkwera, si uundaji wa msamiati/ustilahi tu, bali upanuaji wa msamiati wenyewe wa lugha ya Kiswahili. Kuna namna mbili za kupanua msamiati wenyewe wa lugha hii. Kwanza, ni kwa kunyumbua mofimu za maneno ya Kiswahili yaani kutazama baadhi ya vijineno vinavyoweza kurekebishwa ili vifanye kazi ya ujenzi - neno (Kiingi K.B (1992).

Pili, ni kwa kuufufua na kuupanua kimaana msamiati wa zamani 'uliokufa' na ambao unafaa kutumiwa pale ambapo hapana neno

.../43

mwafaka. Uzingatiaji wa masuala haya utathibitisha hoja kwamba Kiswahili, kama lugha nyingine yoyote kina uwezo wa kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

Aidha, ufufuaji wa msamiati wa zamani wa kiswahili ambao haukufikiriwa katika kiswahili sanifu utasaidia kama tulivyokwisha kueleza, katika kuijenga lugha hii katika misingi ya kiafrika na wala si ya kigeni. Jambo la muhimu la kuzingatia hapa ni kwamba kiswahili, kwa muda mrefu sana kimekuwa kikibezwa kwa madai kwamba ni lugha yenye upungufu wa msamiati. Ufufuaji wa msamiati kiasili uliosahaulika katika kiswahili sanifu, utathibitisha kwamba lugha hii haijawahi kuwa na pengo kubwa la kimsamiati, na kwamba ukwasi wake wa msamiati ni pana zaidi na panatumika tu sehemu ndogo ya jumla ya msamiati wake.

W. Whiteley (1969) anasema:

> "Mashina ya kiswahili ambayo yamepatikana katika 'standard swahili' hayana ukale wa lugha hii. Kwa hivyo, 'standard swahili' ambayo inatokana na Kiunguja, si lugha ya kale... kulitatua suala hili kunahitaji uchunguzi wa msamiati wa kale wa Kiswahili"...[11](Tafsiri).

Maoni ya Whiteley yana mashiko na tunakubaliana naye kwamba ukale wa lugha ya Kiswahili haupo katika kiswahili sanifu. Kwa hivyo, ufufuaji wa msamiati wa zamani wa kiswahili ambao haukufikiriwa katika 'standard swahili' unahitajika ili kuirudishia lugha hii ukale wake na kuiondolea ugeni mwingi kimsamiati.

Watetezi wa ukopaji wa msamiati wa kigeni kama vile Massamba (1988), Akida (1975), Kitsao (1989:51), Mdee (1980) wana madai kuwa hili ni jambo la kawaida kwa kila lugha ulimwenguni. Sisi hatuushuku msimamo wa wanaisimu hawa, tunawaheshimu sana, na hatuna shaka walikuwa na sababu muruwa za kuwafanya wachukue msimamo huo, lakini ijapokuwa tunaelewa kuwa kila lugha 'hukopa', ni maoni yetu kuwa Kiswahili kinaweza kujisimamia kimsamiati pasi na kuendelea kukopa msamiati wa kigeni.

H.M. Mbega (1979) anasema:

> "Maneno karakhana (karakana), zahanati, kabaila, kipuri na kadhalika ni maneno ya wapi? Hiki Kiswahili cha mpetompeto ni cha nini? Kwa nini tunakikuza Kiswahili kwa maneno ya kudondoza? Kwani tumeuchimbuza ukale wa Kiswahili na kupata kuwa hatuna hazina ya maneno? Tumegundua kuwa hiki si Kiswahili bali ni mpochongo wa maneno." [11]

Maoni ya Mbega ya uzito na tunakubaliana naye. Ili kuondoa tatizo la matumizi haya ya 'mpochongo wa maneno' suala la ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili 'uliokufa' linahitaji kutiliwa manani sana.

Watetezi wa matumizi ya msamiati wa kale katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili kama vile R.K. Ruo (1979), H.M. Mbega (1979), S.A. Nabhany (1982), wamekusanya msamiati mwingi wa zamani ambao unafaa utumiwe badala ya msamiati unaotoholewa ama unaokopwa kutoka lugha za kigeni. Wamependekeza, kwa mfano, maneno kama:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Uhazigi | badala ya | | Zahanati |
| Jasi | " | " | fedha |
| ngondo kasi | " | " | nishati |
| ndaki | " | " | chuo kikuu |
| yumbe | " | " | bunge |
| gongwa | " | " | Ikulu |
| joma | " | " | askari |
| uyoka | " | " | eksirei |
| udandi | " | " | kalamu |
| liwaa | " | " | sahau |

M.B. Mkelle (1971) anaelekea kuwaunga mkono 'wanajadi' hao kwa madai kwamba msamiati uliokopwa wa kigeni aghalabu hupoteza maana iliokusudiwa na huwa hausadifu kueleza dhana unaoziwakilisha ipasavyo.

Kunao msamiati mwingi uliokopwa na ambao umebadilika kimaana wakati ulipoingizwa katika kiswahili. Kwa mfano:-

| Kiarabu | Kiswahili |
|---|---|
| bazzaz | bazazi |
| hamak | hamaki |
| tajir | tajiri |
| kafir | kafiri |

Neno bazazi ni la Kiarabu, likimaanisha"muuzaji duka,"au (mfanyi biashara).
Kwa sasa, linatumiwa katika Kiswahili kwa maana ya mtu mjanja.

tajiri - maana asilia katika Kiarabu ni bepari (capitalist)
- katika kiswahili neno hili limebadilika kimaana na kuwa mtu mwenye mali nyingi (rich man).

Kafir - ni la Kiarabu maana asilia ni dini

- kwa sasa linatumiwa kwa maana ya 'mtu asiye mfuasi wa dini 'unreligious'

Neno husudu - maana yake asilia ilikuwa kuchukia

katika kiswahili, neno hili limepanuliwa kimaana - kupenda

Siasa - busara (maana asilia)

utawala(maana ya kisasa).

S. Falk Julia, (1973) anadokeza kwamba lugha zote hubadilika kulingana na wakati. Mabadiliko hayo, kwa maoni ya mtaalamu huyu, hutokea polepole kiasi kwamba wazungumzaji hawafahamu mabadiliko hayo hadi mpito wa kiwakati wa muda mrefu sana utokee. Mabadiliko hutokea katika nyanja zote za lugha hususa katika matamshi, sintaksia, semantiki na leksia.

Naye M.H. Abdulaziz (1989) anasema kwamba mabadiliko ya lugha ni kitambulishi ( a reflection) cha mabadiliko ya kijamii. Wataalamu hawa kwa hakika maoni yao yana mashiko, hasa tukizingatia maneno yafuatayo ambayo yamebadilika kisemantiki:-

neno Mkunga - ni la tangu jadi, likimaanisha mwanamke tu anayezalisha.

kwa sasa, ni msamiati wa mzalishaji hata awe mwanaume.

neno Mtumba - lilimaanisha furushi la nguo kukuu

kwa sasa ni kitu chochote kikukuu.

Neno "kitu kidogo" - lilimaanisha uchache wa kitu fulani
kwa sasa ni hongo au rushwa.

Mfano zaidi wa maneno ambayo yamebadilika Kidaikronia:-
M.A. Pie (1967:66) anatoa mfano wa neno nescius la Kilatini ambalo lilimaanisha silly, ignorant, kwa Kiingereza.

Neno "silly" katika Kiingereza, lilimaanisha nice
kwa sasa ni neno la kimatusi la ujinga

Idiot" maana yake asilia ilikuwa mtu adimu (a private person)
kwa sasa ni mtu mjinga

"lust" zamani likimaanisha furaha (pleasure)
sasa linamaanisha usinifu (sinfulness)

Izingatiwe kutokana na mifano hii kwamba, msamiati uliokopwa kutoka lugha za kigeni aghalabu hupoteza maana uliokusudiwa na huwa hausadifu kueleza dhana unaoziwakilisha ipasavyo. Kwa hivyo tunakubaliana na Mkelle (ibid) kuhusu suala hili. Aidha, ijapokuwa tunakubaliana na wataalamu Falk (1973), Abdullaziz (1989), Kiingi (1969), Lehmann (1962) kuwa lugha hubadilika kulingana na wakati, sisi tunachukulia msamiati bazazi, hamaki, tajiri, husudu kuwa na maana yake asilia tu, basi.

Ingawa tunaelewa pia kwamba ni vigumu kubadilisha dhana ambayo watu wameshajizoesha nayo, msimamo wetu kuhusu mabadiliko ya msamiati kimaana hauna budi kuchukuliwa hivyo ulivyo. Kwa upande mwingine lakini, maadamu 'ukopaji' wa msamiati wa kigeni unakubalika hili ni deni ambalo wataalamu wa Kiswahili hawana budi kulilipa kwa 'kulifanyia haki' kiutafiti. (Kitsao 1989:54).

Inafaa tutaje hapa kwamba, mbali na kuwa msamiati uliokopwa hubadilishwa sana kimaana, ukopaji huo, kama anavyodokeza Kiingi (1992) haufanywi kwa utaratibu maalum. Kwa mfano, hakuna mpango maalum unaofuatwa katika msamiati ufuataо:-

| Kiingereza | Bakita | Tanzania Visiwani na hapa Kenya |
|---|---|---|
| skirt | sketi | skati |
| nurse | nesi | nasi (mwaguzi) |
| blanket | blanketi (ma) | burangeti |
| bank | benki | bengi |
| dozen | dazeni | darzeni |
| exercise book | daftari | buku |

Mfano zaidi, ikiwa "cementi" ni simenti

"virus" ni virusi

"cell ni seli

Kwa nini "iris" iwe mboni badala ya irisi

"hormone" iwe kizao badala ya homoni

"mosaic" iwe chapa na wala si mosaiki

"personality" iwe haiba na wala si personality

"phenomina" iwe halia na wala si fenomena

"ovule" iwe ovule na wala si ovyulu?

(Tax. Hamad. A.K. 1989:70)

Pendekezo letu ni kwamba endapo ukopaji wa maneno ya kigeni utatumiwa amą utakubaliwa na wataalamu wa Kiswahili, na ufanywe kwa utaratibu maalum wala siyo "vivi hivi tu" kama inavyojitokeza katika mifano tuliotoa hapo juu. Hatua nyingine ambayo itafaa izingatiwe na TUKI ni ya ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili 'uliokufa' na ambao unafaa ili utumiwe pale ambapo

hapana neno mwafaka. Hapa, bila shaka umuhimu wa ufufuaji wa msamiati wa zamani na kuupanua kimaana unajitangaza wo wenyewe.

I. Mbaabu (1989) anasema:-

> "Ukubalifu wa msamiati unategemea aina ya msamiati na vile wale walioutunga msamiati huo wanavyozifahamu nyanja za msamiati wenyewe..."[13]

Anaendelea kusema:

> "Vile vile ukubalifu wa msamiati unategemea taratibu zilizotumiwa kuunda msamiati huo. Msamiati wa mila na utamaduni, kwa mfano yafaa ubuniwe na baraza la wazee likiongozwa na taratibu maalumu. Maneno mapya ya kiutamaduni yanapohitajika hayana budi kuambatanishwa na msamiati asilia kiasi iwezekanavyo" (Msisitizo ni wetu).[14]

Pendekezo la Mbaabu lina uzito na tunakubaliana naye. Kuijenga lugha ndani ya lugha ndiko kuikuzi bali kuiundia msamiati 'kiholela' pasi na kuuchimbuza ukale wake ni kuibeza lugha kwa maoni yetu. Hii haina maana kwamba msamiati mpya usiundwe wala msamiati wa kigeni uliozagaa na kuerea ubadilishwe.

Tunachosisitiza ni kwamba hapana dharura yoyote inayotushurutisha, kwa mfano, kuunda msamiati mpya ama kukopa wa kigeni pale ambapo tunahitajika tu kupekuapekua miongoni mwa waswahili wenyewe na kuupata msamiati wa zamani ambao unafaa utumiwe pale ambapo hapana msamiati mwafaka au ikiwa msamiati huo wa zamani unatosheleza haja.

Sababu nyingine muhimu ya ufufuaji wa msamiati wa zamani uliosahaulika ni kwamba msamiati huo utasaidia katika kuikuza lugha ya Kiswahili katika mwelekeo mmoja. Hazina ya msamiati wa kiswahili itachangiwa zaidi kupitia kwa njia ya ufufuaji wa msamiati wa zamani 'uliokufa' na ubunaji wa msamiati mpya wenye mantiki. Uzingatiaji wa suala hili utasaidia sana kwa maoni ya H.M Mbega, A. Baruwa, S.A. Nabhany, Akida ambao wanapendekeza 'Kiswahili kijengwe kwa misingi ya Kiswahili.'

Aidha, matumizi ya njia au utaratibu wa kufufua msamiati wa zamani uliosahaulika katika kiswahili sanifu yatadhihirisha wazi kwamba, kiswahili kama lugha yeyote ile, kinaweza kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

W.H.L. Kitumboy, (1959:227) anasema kwamba lugha ya Kiswahili inazungumzwa kwingi barani Afrika lakini kasoro yake ni kwamba msamiati wake mwingi umeundwa 'vivi hivi tu' na kila mzungumzaji huizungumza kivyake. Madai haya kwa kiasi kikubwa yana uzito kama tutakavyoyafafanua baadaye.

Kikwamizi kikubwa cha uendelezaji wa leksikoni kinatokana na wanaleksikografia wa kiswahili kuunda msamiati mpya ilhali tayari upo msamiati unaopatika katika lugha hii. Kwa mfano:-

| | |
|---|---|
| "bloodpressure" | ni presha |
| | buhari |
| | mtuto wa damu |

Wazee wa Mombasa kwa muda mrefu wamekuwa wakilitumia neno buhari

kwa maana ya "high & low bloodpressure", hivyo hapakuwa na haja yoyote Watanzania na wataalamu wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) kuunda mtuto wa damu ama hata presha iwapo hasa tunakusudia kuikuza lugha hii kwa mwelekeo mmoja.

Isitoshe, uundaji wa msamiati mpya, kama unavyofanywa na wanaleksikografia wa Kiswahili, TUKI, umeonekana kwamba haufuati mantiki yanayohitajika kama tulivyosema mbeleni. Kwa mfano:-

| | Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|---|
| neno | hydropily | kimeamaji |
| | hydrophyte | yungiyungi |
| | hydrotropism | ubadilihali |
| | hydrogen | haidrojeni |

Kutokana na mfano huu, ni kweli kama wanavyodokeza Kitumboy (1959) na Kiingi (1992) kwamba wanaleksikografia wa Kiswahili wanaunda msamiati 'vivi hivi tu' pasi na kufuata utaratibu fulani maalumu. Ile 'hydro' - ya mwanzo hairejelewi katika maneno yote yenye kiambisho hicho.

Kwa hivyo, kinachohitajika kwa upande wa TUKI si kuendelea kuunda msamiati kwa sababu ya haraka za kuzifuata lugha za kigeni, ila ni kuwa wabunifu zaidi na kuweza kuchunguza katika lahaja za kiswahili msamiati wa zamani uliosahaulika na unaotosheleza haja - waufufue na kuutumia katika maandishi ya kila siku.

Ni muhimu pia kutaja hapa kwamba msamiati mpya unapoundwa aghalabu huwakilisha dhana moja. (Maina 1989:118) Katika kutekeleza wazo

hili, msamiati mpya unaoundwa unakuwa mrefu mno na hautamkwi kwa urahisi. Kwa mfano,

neno "planstable" - kipimapembeubapa"

"triangulation" - mwimarishopembetatu

"radiation" - mpimomtawanyo

Je, haingewezekana wanaleksikografia wa Kiswahili kuwa wabunifu zaidi na kupata maneno mafupi badala ya haya marefu mno yanayowatatanisha watumiaji wa lugha hii kimatamshi? Hapana shaka, ubunifu zaidi unahitajika hapa kwa upande wa wanaleksikografia. Pamoja na haja ya kuchunguza msamiati wa zamani ambao utafaa utumiwe pale ambapo hapana msamiati mwafaka.

Izingatiwe kwamba suala la matumizi ya msamiati wa zamani uliosahaulika katika Kiswahili sanifu lakini ambao upo katika lahaja nyingine za Kiswahili kama vile Kimvita, Kiamu, Kivumba, Kimtangata na kadhalika si ligeni kamwe. Wataalamu wengi wa Kiswahili wamewahi kupendekeza kwamba msamiati wa Kilahaja utumiwe na uwekwe katika makamusi ya kiswahili lakini kwa bahati mbaya uchunguzi unaostahili haujafanywa kuhusu suala hili, ambalo kwa hakika, ni muhimu sana katika kuendeleza leksikoni ya lugha ya Kiswahili.

J.S. Mdee (1986) kuhusu jinsi msamiati katika lahaja nyingine za Kiswahili unavyoweza kuendeleza leksikoni ya lugha hii anasema:

> "... kusema kweli Kiswahili kina maneno mengi ya kuweza kueleza dhana kadha, lakini kutoyajua kwetu kumetufanya kuunda ama kutohoa maneno kwa dhana hizo. Maneno haya yatafutwe kutoka kwa wazungumzaji wa fani inayoshughulikiwa....." [15]

Kauli ya Mdee ina mashiko na tunakubaliana naye kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba ukwasi wa lugha ya Kiswahili ni pana sana. Kutopekuwapekuwa miongoni mwa Waswahili wenyewe na kudurusi kamusi za zamani za kiswahili na katika fasihi za kale kama vile Utenzi wa Mwana Kupona, Utenzi wa Tambuka, Takhmisa ya Liyongo, Al-Inkishafi na kadhalika kumewafanya wanaleksikografia wa kiswahili kuunda ama kukopa msamiati wa kigeni. Isisitizwe hapa kwamba hapajawahi kuweko pengo kubwa la kimsamiati katika kiswahili, kwa hivyo wataalamu wa kiswahili wanahitajika kuubukua na kuufufua msamiati wa zamani uliosahaulika katika kiswahili sanifu na kuupanua kimaana. Utekelezaji wa jambo hili, utachangia sana katika kuendeleza leksikoni ya kiswahili mumo kwa mumo bila shaka.

Aidha, sababu nyingine ya ufufuaji wa msamiati wa zamani 'uliokufa' wa kiswahili ni kwamba msamiati huo utasaidia kuikinga lugha ya Kiswahili na athari ya Kisheng'. Lugha ya Kisheng' imeendelea kujirutubisha kimsamiati na kuathiri sana maendeleo ya Kiswahili.

Uchunguzi uliofanywa na wataalamu kama vile M.H. Abdulaziz (1989) na K. Osinde (198 ) unaonyesha kwamba wazungumzaji wa lugha ya Kisheng' ni wale wasiojuwa vizuri Kiswahili na Kiingereza na kwa hivyo hukipendelea Kisheng'kwa sababu hakina sheria nyingi za kisarufi.

i. Mbaabu (1978:90) amezungumzia lugha ya sheng' ambayo anaita 'lahaja ya Nairobi'. Wanapozungumza vijana wanaotumia lugha ya kisheng' wao hutumia lugha kama ifuatavyo:

-(a) Niaje, mbona leo hauna story mob ya kubonga brathee?
(Ni vipi mbona leo hauna hadithi nyingi ya kutusimulia ndugu?)

(b) Wale manyanga karibu watakitoa. Tuchukulie easy na tuende tuwacheki .... acheni kusubaa.

(Wasichana warembo wale wako karibu kuondoka. Tusiogope, twende tuwaone... mwache kuogopa).

Mifano zaidi ya Kisheng': kuinjoyi - kufurahi

demu, kirenga, ndisti, manyanga - msichana mzuri

malayee, luuchi - kahaba

kutuna - kulala

tuuchi - twende

kobole - shilingi tano

ndinga - gari

Ni maoni yetu kwamba, lau Kiswahili kingeendelezwa kimsamiati kwa kufufua na kuupanua kimaana msamiati wa zamani uliosahaulika katika kiswahili sanifu, hakingeathiriwa zaidi na lugha ya Kisheng'.

Kuwepo kwa msamiati mwingi wa kigeni katika kiswahili usiotambulikana bayana kimaana, umekifanya kiwe kigumu kwa baadhi ya wazungumzaji wa lugha hii na kwa namna hii kukipa hadi Kisheng' ambacho kimeanza kunyemelea mhali mbalimbali hapa nchini Kenya. Kwa usemi mwingine, ufufuaji wa msamiati wa zamani wa Kiswahili 'uliokufa' utaweza kupunguza athari ya Kisheng', lugha ambayo ni tishio kubwa sana la maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya.

Sisi, ijapokuwa tunaelewa kuwa pana tatizo la ukubalifu linalotokana na wanajamii fulani kuyapendelea maneno fulani ambayo kwao ndiyo yaliyo na 'mwonjo' zaidi, tunapendekeza, kutokana na sababu sote zilizojadiliwa hapa, ufufuaji na upanuaji kimaana wa msamiati wa zamani wa kiswahili

uliosahaulika katika Kiswahili sanifu kama njia moja wapo ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili. Msamiati wa zamani 'uliokufa' ufufuliwe na utumiwe pale ambapo hapana neno mwafaka badala ya kuendelea kukopa kwenye lugha za kigeni kama inavyofanywa sana leo. Kwa mfano, badala ya kutumia msamiati wa kigeni, patumiwe msamiati wa zamani kama vile:

funda: Neno hili ambalo kwa sasa halitumiwi limo katika kamusi ya zamani ya F. Johnson (1939) na yaonekana liliwahi kutumika kwa wakati fulani. Tazama, fundika, fundo, mfundo, kifundo

Neno funda lina maana mbili,

1. Kumea matiti kwa msichana anayefunja ungo
2. Kufunganisha vitu fulani kwa pamoja

mfano zaidi;

| | | |
|---|---|---|
| kondo/bangu/hirabi | - | vita |
| ifuki | - | uongo |
| kidhabu | - | mwongo |

Isitoshe, sababu mojawapo muhimu ya pendekezo letu la njia hii ya ufufuaji wa msamiati wa zamani ama msamiati kiasili uliosahaulika katika kiswahili sanifu ni ya kihistoria(kutaka kuikinga lugha hii na athari za lugha sanifu). Usanifishaji wa Kiswahili, kama historia inavyotueleza na kwa maoni ya Mbaabu (1991) ulikuwa na dosari nyingi mno. Kwanza kabisa, usanifishaji wa Kiswahili mbali na kwamba wenyeji/ Waafrika hawakuhusishwa katika shughuli za hizo usanifishaji wenyewe ulifanywa kwa haraka sana. Kutokana na haraka walizokuwa nazo wageni waliosanifisha kiswahili, msamiati kiasili mwingi wa kiswahili ambao upo katika kiswahili cha kilahaja na katika fasihi za kale kama Tendi mbalimbali, haukufikiriwa kamwe katika kiswahili sanifu.

Pili, kuteuliwa kwa lahaja ya Kiunguja kulipuuza kigezo mojawapo muhimu katika usanifishaji wa lugha. Lahaja inayoteuliwa ya kusanifishwa haina budi kuwa na historia ya kimaandishi. Iwe kwa muda mrefu ni lugha ambayo imeandikiwa hasa fasihi na kadhalika.

Madan asema kwamba kiunguja hakikuwa na maandishi sanifu ukikilinga nisha na Kimvita na Kiamu ambazo zilikuwa zimesitawi sana kabla ya kuja kwa wamisheni. Ingawa si madhumuni yetu kuendeleza mjadala huu, ifahamike kwamba kigezo hiki ndicho kilimfanya Khalid (1977) kupendekeza kwamba Kiswahili kisanifishwe upya. Sisi, pendekezo letu, kinyume na Khalid, ni kwamba msamiati wa zamani ama msamiati kiasili uliosahaulika katika kiswahili sanifu ufufuliwe. Ufufuaji wa msamiati huo utasaidia kuikinga lugha hii na athari za lugha sanifu kama zinavyojitokeza katika mifano ifuatao:

| Kiswahili sanifu | Msamiati kiasili wa kiswahili |
|---|---|
| blanketi (ma) | burangeti |
| dazeni | darzen |
| majununi (jester) | mteshiteshi |
| pombe (alcohol) | kileo |
| ashiki (strong affection) | nyonda |

Kiswahili 'Kili-Arabishwa' sana na kikapunguzwa U-bantu wake kutokana na mifano hii bila shaka.
Chambilecho wenye kusema, 'kinga yashinda tiba'. Tusipokinga lugha ya kiswahili kwa kufufua na kuyapanua kimaana maneno ya zamani yaliyokufa, huenda yakafa yale maneno yaliyopo. Sasa (ingawa kufa kwa maneno ni lazima kwa kila lugha) kwa sababu ya athari ya lugha sanifu, ambayo 'usanifu wake, kama tulivyodokeza hapo mbeleni ulikuwa

na 'siasa' nyingi (Mkude 1982) na unahitaji uchunguzi zaidi.

Jinsi Msamiati katika lahaja nyingine unavyoweza kuendeleza leksikoni ya Kiswahili

Tumesema kwamba msamiati wa zamani uliosahaulika katika Kiswahili sanifu unaweza ukapatikana katika lahaja nyingine za kiswahili na katika kazi za kale za fasihi ya kiswahili.

Lahaja, tunalitumia hapa kwa maana ya lugha kwa mujibu wa pahala na ngazi ya mtu katika jamii. Lugha ni utaratibu maalum wa sauti za kusemwa na za nasibu unaotumika na binadamu katika kuwasiliana. Suala hili la matumizi ya msamiati unaopatikana katika lugha za kibantu na lahaja nyingine za kiswahili ni muhimu sana na limewahi kupendekezwa na wataalamu kama vile Mdee (1986), Mutahi (1986), Khalid (1977), Abdulaziz (1985), Kiingi (1989), Likhako (1991) na Mukhwana (1988).

Hata hivyo, kiswahili bado hakijafanyiwa uchunguzi mpana na wa kuhusiana na mambo haya. Uchunguzi wa makini katika lahaja za kiswahili, na lugha nyingine za kibantu, utasaidia sana katika kukiimarisha kiswahili kileksia bila shaka..

Matokeo ya uchunguzi mdogo uliokwishafanyika hadi sasa, kwa maoni ya Temu (1983), unaonyesha mafanikio mazuri.

A. Mukhwana (1988) kuhusu suala hili anasema:

> "... Kiswahili ni lugha na ikiwa haina msamiati wa kutajia kifaa fulani jambo la kwanza la kufanya ni kutafuta na kubukua katika lahaja zote za lugha

> hii... ikiwa kwa bahati nzuri, mojawapo ya lahaja za Kiswahili ina neno la kutajia kifaa hicho na lichukuliwe mara moja".[16]

Kutokana na dondoo hili, Mukhwana inaelekea anaunga mkono hoja kwamba majina ya Kiafrika yanapotumiwa kuijenga lugha ya Kiswahili yanazidi kuipa sura ya Kiafrika.

Mukhwana anaendelea kusema:

> "... ni kwa kufuata njia hii ndipo Kiswahili kikapata msamiati kisabeho (Kipemba), kwa maana na 'breakfast dish' yaani kifugua kinywa".[17]

Tunakubaliana na mtaalamu huyu kwamba njia hii ikitiliwa uzito zaidi huenda ikasaidia sana kuhifadhi U-Afrika wa lugha ya Kiswahili badala ya ukopaji wa msamiati kutoka lugha za kigeni. Hata hivyo neno kisabeho ingawa latumiwa Pemba lakini asili yake si ya Kibantu - linatokana kwa maoni yetu, na sabihi/sabahi la Kiarabu kwa maana ya salamu za asubuhi" (sabaoheri). Neno kuchewa ndilo la Kibantu lenye maana ya salamu za asubuhi, suala ambalo mtaalamu huyu hakulizingatia. Mukhwana (1988:62) pia anapendekeza kuwa ikiwa lahaja za Kiswahili kama vile Kiamu, Kivumba, Kimvita, Chi-jomvu, Kimtang'ata, Kipemba na kadhalika hazina msamiati unaotafutwa itatubidi tukope. Hapa sisi tungependa kuchukua msimamo ulio tofauti na huu. Tunapendekeza tubuni msamiati mpya pale ambapo hatuna msamiati mwafaka katika lahaja nyingine za Kiswahili na lugha za Kibantu. Ukopaji, kama anavyosema R. Ohly (1977) iwe ndio hatua ya mwisho kutekelezwa. Pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka katika Kiswahili chenyewe tunapendekeza tubuni msamiati mpya kwa kuzingatia misingi ya Kiisimu.

Iwapo matumizi ya msamiati wa kigeni ndio yanafanya Kiswahili kubezwa kuwa hakina 'msamiati wa kutosha', hatuna budi kuanza 'kukiboresha Kiswahili kwa kuyatumia pia maneno ya kilahaja jambo ambalo, tunastajabika kuona kuwa I.N. Shariff (1988:20), D.M.W. Njeru (1990) na wengine wengi hawaliungi mkono.

Juhudi zinazofanywa kukiendeleza Kiswahili zitapiga hatua moja mbele kwa kuchunguza zaidi na kutumia msamiati wa kilahaja ambao haukufikiriwa katika Kiswahili sanifu. Yako maneno mengi yaliyotoholewa kutoka lugha za Kiafrika (Kibantu). Kwa mfano,

| Kibantu | Kiingereza |
|---|---|
| Mlulu (Kipoare) | peat |
| koya (Kipemba) | scum |
| kianguta (Kisii) | hob |
| ng'ozi (Kimtang'ata) | leafcurl |
| mbuti (Kimaasai) | duodenum |
| yumbe (Kiha) | parliament |
| ikulu (Kisukuma) | state house |
| ngowela (Kikaguru) | antiphony |
| njeo (Kiamu) | tense (period) |

(BAKITA (1980) Tafsiri Sanifu Toleo la 4)

Mifano zaidi;

P.I. Likhako (1991) anatoa mifano zaidi ya msamiati wa kilahaja anapodokeza kwamba iwapo neno mwafaka halipo katika Kiswahili basi litoholewe kutokana na lugha zingine za Kiafrika.
Kwa mfano,

| | |
|---|---|
| rara (Kiyoruba | ballad |
| sukui (Susu Guinea) | blank verse |

<u>ngana</u> (Kinyaturu)———— accessories

<u>ngeno</u> (Kinyamwezi)———— epithaliom

<u>nduma</u> (Kikuyu)———— arrow root

<u>ulalo</u> (Ndalo)———— diagonal

<u>mbigane</u> (Kiyao)————inequality

<u>mwaro</u> (Kimara)———— coast

S.J. Maina (1989) ni mtaalamu mwingine anayetambua umuhimu wa msamiati wa kilahaja katika kukuza lugha ya Kiswahili. Anatoa mfano ufuatao wa msamiati kutoka lugha za Kibantu.

| <u>Kiingereza</u> | <u>Kiswahili</u> |
|---|---|
| Granite | Itale (Kisukuma) |
| Affluent | Kipera (Kingoni) |
| fallow | fuwele (Kizigua) |
| peneplain | hala (Kigogo) |

Msamiati kutoka katika lugha za makabila ambayo si ya Kibantu ni:

| <u>Kiingereza</u> | <u>Kiswahili</u> |
|---|---|
| kola nuts | kola (Hausa) |
| curving knife | Ngalemu (Kimasai) |
| virgin land | lweya |

Msamiati wa kilahaja, kutokana na mifano hii, una umuhimu mkubwa mno hasa pale ambapo hatuwezi kupata msamiati mwafaka katika Kiswahili chenyewe. Msamiati wa kilahaja pia unaleta dhana 'mpya' na hivyo kuipanua lugha hii.

S.A. Nabhany (1982) yuasema:

> "Maneno yatakikanayo lazima kwanza yatafutwe katika ndimi kumi na tano (15) za Kiswahili, tusitosheke na ulimi (lahaja)

mmoja, tutakosa na kusema neno hilo hapana katika Kiswahili".[18]

Nabhany, kwa wale wanaomfahamu, ni miongoni mwa wataalamu ambao msimamo wao unatetea ukale wa Kiswahili na lahaja zake. Tunakubaliana naye kwamba pana haja kubwa ya kupekuwapekuwa miongoni mwa lahaja za Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika na kupata msamiati wa kilahaja kama mojawapo ya njia za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili.

Wataalamu wa TUKI hawana budi kujishughulisha kwanza na utafutaji wa msamiati wa zamani katika Kiswahili chenyewe, na msamiati kutoka lugha/lahaja nyingine za Kiafrika kabla ya kuopa moja kwa moja msamiati wa kigeni.

Sisi, ingawa tunaelewe kwamba watetezi wa ukopaji wa maneno ya kigeni wana sababu zao za kushikilia msimamo wao, ni maoni yetu kwamba madai kuwa ukopaji unaendeleza Kiswahili sio kauli madhubuti. Kinachohitajika kwa sasa, hasa kwa upande wa wataalamu wa Kiswahili si kukipa kwa sababu "kila lugha ulimwenguni hufanya hivyo", la hasha, ni kuwa wabunifu zaidi pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka katika Kiswahili chenyewe na lahaja nyingine za Kibantu. Kwa mfano, maneno kama "gari" au "bomu". Ni kutokana na kutambua umuhimu wa kubukua na kutafuta msamiati wa zamani katika lahaja za lugha hii ndipo Nabhany amefanikiwa kukusanya msamiati ufuatao:-

| | Kiingereza | tafsiri ya moja kwa moja |
|---|---|---|
| uka | ray | (rai) |
| mangala | microscope | (mayiskroskopu) |
| uyoyozi | air-condition | (eya-kondishoni) |
| tuta | retire | (ritaya) |
| mwai | oxygen | (oksijeni) |

| | | |
|---|---|---|
| wewendu | focus | (fokasi) |
| Mwengoya | radio | (redio) |

Nabhany anadokeza kwamba:

> "haya ni baadhi ya maneno yawezayo kutumiwa katika lugha yetu ya taifa badala ya kutumiwa ya Kiingereza na hata yakitumiwa ya Kiingereza lakini na yetu yawepo ili yengeze ukwasi au msamiati kuikuza lugha hii".[19]

Sisi tunakubaliana naye. Kauli hii ina mashiko bila shaka. Izingatiwe kwamba kutojishughulisha na kutafuta msamiati wa kilahaja uliosahaulika katika Kiswahili sanifu kumewahi kuwafanya wataalamu na wapenzi fulani wa Kiswahili kujitokeza na madai yasio na uzito wowote. Tuchukue kwa mfano, L.M. Mbotela alisema katika lugha fasaha katika redio K.B.C tarehe 29/9/92 kwamba hapana neno la kiswahili kama vile tewengo. Tunakataa wazo hilo. Neno tewengo ni neno la zamani ambalo lingali latumiwa katika lahaja ya Kiamu. Limetokana na tenge tahanani na kadhalika ambayo yanatumiwa kueleza hali ya huzuni mwingi. Kwa mfano,

usinitewenge (do not harass me)
(usinichafye roho/acha kunitesa)

sitaki tewengo (I don't want nuisense)
(sitaki kusumbuliwa)

naona tenge tahanani (extreme stress)
(kuhuzunika sana)

Kutofikiriwa kwa msamiati kama huu tewengo katika Kiswahili sanifu haina maana kwamba si wa kiswahili kama alivyodai L.M. Mbotela (1992). Kinachohitajika ni kuchunguza katika lahaja za

Kiswahili na katika kazi za zamani za fasihi msamiati ambao upo lakini hautumiki sasa katika kiswahili sanifu kabla ya kutoa uamuzi wowote juu ya neno lipi ni la Kiswahili na lipi si la Kiswahili. Msamiati wa Kiswahili si tu ule unaotumiwa katika maandishi hivi sasa, pana pia na msamiati wa Kiswahili wa kilahaja ambao nao unahitajika kufufuliwa na kupanuliwa kwa kuupatia maana mpya.

Kwa usemi mwingine msamiati wa kilahaja usiokuwepo katika maandishi ya kila siku ni mwingi sana na inakuwa jambo la busara iwapo wataalamu wa TUKI watashirikiana na 'kuufanyia haki' ya kiutafiti inayohitajika badala ya kuendelea kukopa msamiati wa kigeni, na kuingiza ugeni mwingi katika lugha ya Kiswahili.

Isisitizwe hapa kwamba, matumizi ya msamiati wenye asili ya kigeni (Kiarabu, Kiajemi, Kiingereza) si sababu tosha ya madai kuwa Kiswahili hakiwezi kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo pasi na kukopa msamiati wa kigeni.

Msamiati wa zamani ambao upo katika lahaja za kiswahili na katika kazi za kale za fasihi 'uliokufa' ukifufuliwa una umuhimu usio haba katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. H.J. Mwansoko (1992) ana maoni kwamba msamiati wa zamani wa Kiswahili waweza kuhuishwa na kupewe matumizi mapya.[20] Tunakubaliana naye. Hatusemi kuwa lugha inayoingiza maneno ya kigeni ni lugha ya chini wala si madhumuni yetu kusema hivyo, ila tunapendekeza ikiwezekana ukopaji kwa wakati huu uepukwe na badala yake ubunifu wa msamiati mpya utiliwe manani pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka katika kiswahili chenyewe.

K.B. Kiingi (1992) anapendekeza kwamba badala ya kuazima msamiati wa kisayansi wa kigeni na kuuswahilisha pana haja ya kuunda msamiati mpya kwa kutazama baadhi ya mofimu na kuzirekebisha ili zifanye kazi ya ujenzi-neno. Naye S.A. Nabhany (1982) badala ya kukopa katika Kiingereza na Kiarabu anapendekeza msamiati uundwe kwa kutafsiri maana ya viungo vidogo vya maneno vyenye maana kutokana na lahaja za Kiswahili.

Hapana shaka kwamba kama wataalamu wa TUKI katika juhudi zao za kukuza lugha ya Kiswahili watazingatia kwa kadri inavyowezekana njia hizi za Kiingi na Nabhany za kuunda msamiati na watambue umuhimu wa ufufuaji wa msamiati wa zamani wa kiswahili uliokufa. (Kwa mfano, umbu umekufa badala yake inatumika dada) na watambue kwamba msamiati wa zamani waweza kuhuishwa na kupewe matumizi mapya, lugha ya Kiswahili kwa maoni yetu, itakuwa na msamiati kiasili bora ulioangamizwa kwa sababu ya kuingizwa kwa msamiati mwingi wa kigeni katika lugha hii. Jambo hili litawezekana iwapo wanaleksikografia wa Kiswahili watashirikiana ipasavyo katika kukuza lugha hii ya kiswahili.

J. Kitsao (1989) anasema:

> "Madai kuwa kiswahili ni lugha isiyoweza kujitosheleza kulingana na ulimwengu wa leo hayana wala hayawezi kuwa na msingi, na yafaa kupuuzwa. Izingatiwe, kama wanavyokubaliana wanalugha, kwamba mojawapo ya tabia za lugha ni uwezo usio mipaka wa chombo hiki cha mawasiliano miongoni mwa binadamu, kueleza tokeo au jambo lolote jipya...."[21]

.../65

Naye R. Besha (1972) yuasema:

> "Si lazima lugha ichukue maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya au dhana mpya ya kuelezwa. Maneno yenyewe ya lugha yanaweza kupanuliwa maana zake ili kueleza mawazo hayo mapya au kuto maana maalum kwa maneno ya kawaida...." [22]

Maoni ya wataalamu hawa yana mashiko na tunakubaliana nao. Tuchukue kwa mfano, katika Kiingereza cha zamani, badala ya kuchukua maneno ya Kilatini, wenyewe waliunganisha maneno mawili ya kawaida kutoa maana mpya.

Laececraeft badala ya medicine (uganga)
Scopcraeft badala ya poetry (ushairi)
Tungolcraeft badala ya astronomy (elimu ya nyota)
Boccraeft badala ya literature (fasihi)

Tunakubaliana pia na K. Mutahi (1986:65) kwamba kabla ya kuunda msamiati mpya, ni muhimu wanaleksikografia wa Kiswahili kwanza wabukue na kukusanya msamiati wa zamani au maneno asilia ya kiswahili yalipo katika lahaja za kiswahili. Hapana haja ya kukopa ama kuunda msamiati mpya pale ambapo pana msamiati kiasili unaohitajika kufufuliwa kuhuishwa na kupewa matumizi mapya.

Hapana shaka kwamba msamiati wa zamani wa kilahaja ukifufuliwa utasaidia kuziba mapengo ya msamiati maalum (J. Yambi 1993). [23]

Hivyo tunaweza kusema bila wasiwasi kuwa Kiswahili hakijawahi kuwa na pengo la kimsamiati na kwamba, kama lugha yeyote ile, Kiswahili kinaweza kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo. Ni

wazi kuwa patatokea tatizo la ukubalifu. Watetezi wa madai kwamba kila lugha ulimwenguni'hukopa' kama vile S.H. Olson (1972:9), J.S. Mdee (1986), I.N. Shariff (1988:28) itakuwa vigumu kwao kukubaliana nasi kwamba kiswahili kinaweza kujitosheleza kimsamiati na kujiendeleza mumo kwa mumo pasi na kukopa msamiati wa kigeni. Hata hivyo, kutokubaliana kwao na msimamo wetu ndiyo sifa mojawapo muhimu ya masuala ya kitaalamu. Si lazima tukubaliane. Ikiwa tutakubaliana basi usomi utaisha. Tatizo la ukubalifu lina misingi yake katika mazoea. Baadhi ya msamiati inakuwa vigumu kuzoeleka kwa kuwa yapo maneno mengine ambayo yameshazoeleka. Kwa mfano,

runinga ———— televisheni
mweni ———— damu
ng'andu ———— dhahabu
wewendu ———— fokasi

J.S. Mdee (1986 anasema:

> " Kwa hakika hakuna sababu muhimu ya kuingiza maneno ya lahaja nyingine za kiswahili katika kamusi kwani kiunguja kinajulikana karibu Afrika Mashariki nzima....." 24

Maoni ya mtaalamu huyu hayana mashiko na hatukubaliani naye kutokana na sababu zilizojadiliwa mbeleni.

## 2.2.1 Nafasi ya Msamiati wa Zamani wa Kiswahili katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili

Hali halisi ilivyo kwa sasa ni kuwa Msamiati kiasili ama msamiati wa zamani wa Kiswahili haujapatiwa nafasi kubwa katika maandishi ya kila siku ndiposa msamiati huo umebakia tu katika lahaja na kazi

za zamani za fasihi. Jambo hili linatokana na wanaleksikografia wa Kiswahili na wataalamu wa TUKI kutotilia manani ama kutotambua umuhimu wa kuzingatia ukale wa lugha hii katika harakati zao za kuendeleza na kukuza Kiswahili. Kutokana na hali kama hii ambapo msamiati wa zamani umepewa nafasi duni ndipo hatuna budi kutazama hapa umuhimu wa msamiati huo wa kale ambao'umekufa.'

Aidha, tutatumia vigezo vya PEGITOSA kuyalinganisha baadhi ya maneno kiasili ambayo kwa maoni yetu yakifufuliwa na kupanuliwa kimaana ama kupewe matumizi mapya yatasaidia sana kuziba mapengo ya msamiati maalum.

## Umuhimu wa msamiati wa zamani katika maendeleo ya leksikoni ya Kiswahili

Izingatiwe kwamba msamiati kiasili wa kiswahili umebadilishwa na wa kisasa uliokopwa na kuswahilishwa. Huku ni kuiporoja lugha kwa sababu msamiati kiasili una umuhimu wake ambao haupaswi kupuuzwa. Wanalugha ya kiswahili wanakiri kwamba msamiati wa zamani una umuhimu sana katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Ukifufuliwa, kwanza, utasaidia kuziba mapengo ya msamiati maalum.

Pili, badala ya nafasi ya msamiati wa zamani kuchukuliwa na msamiati mwingine uliokopwa kutoka lugha za kigeni, ukifufuliwa utatumiwa pale ambapo hapana msamiati/neno mwafaka.

Tatu, msamiati kiasili ukifufuliwa na kupewe matumizi mapya utawasaidia wataalamu wa TUKI kuepuka kuunda msamiati kwa dhana ambazo tayari zina msamiati kiasili wenye kuziwakilisha. Kwa mfano,

| Kiingereza | neno lililoundwa | neno la Kiswahili |
|---|---|---|
| doctor | daktari | mganga |
| hospital | hospitali | gango |
| pattern | sulubu | ruwaza |
| excretion | utoajitakamwili | nongwe |
| I have seen | nimeona | mbwene |
| x-ray | eksirei | uyoka |
| lover | mpenzi | habibi/mahabubu |
| joy | furaha | sururi |
| leave | mapumziko | sono |
| God | Mwenyezi Mungu | Qahara/Wahabu |
| Book | kitabu/buku | kijuwo |
| fish | samaki | nzi |

S.A. Nabhany (1982) anasema:-

> " haya ni maneno machache tu lakini yako mengi sana na kuyapata kwake ni kwa njia ya utafiti" [25]

Kauli hii ina uzito na tunakubaliana naye.

Mbali na msamiati wa zamani kusaidia katika kuepuka kuunda msamiati kwa dhana ambazo tayari zina msamiati kiasili wenye kuziwakilisha, pia utawasaidia wataalamu wa Kiswahili kuepuka kuuna msamiati zaidi ya moja kwa dhana moja. kwa mfano,

evolution ——— evolushoni
evolution ——— unyumbuzi

microphone ——— mayikrofoni
microphone ——— kipazasauti

| | |
|---|---|
| taperecorder | tapurekoda |
| | kinasasauti |
| epic | utendi |
| | epiki |
| intonation | lafidhi |
| | intonesheni |
| dieback | kufa |
| | kifanyuma |
| doctor | daktari |
| | hazigi |
| antibiotic | ngaomwili |
| | kiuavijasumu |
| astronomy | astronomia |
| | unajimu |
| | elimunyota |

Baadhi ya msamiati/istilahi huu unaoundwa na wataalamu wa TUKI hauwezi ukafaulu jaribio la PEGITOSA kwa maoni ya K.B. Kiingi (1992) na ndiposa hautumiwi katika maandishi ya kila siku. Tunakubaliana na mtaalamu huyu kwamba uundaji wa msamiati wa Kiswahili haujakomaa kwa sababu baadhi ya wanaoshiriki wameathiriwa sana na elimu ya kigeni na taratibu za kigeni za kuundia msamiati. Masuala haya tutayafafanua na kuyathibitisha, ikitulazimu kufanya hivyo, katika sura yetu ya tatu. Hata hivyo hatuna budi kusema kuwa kuunda msamiati zaidi ya moja kwa dhana moja ni kuwakanganya wazungumzaji wa lugha hii ya Kiswahili.

Aidha msamiati wa zamani uliokufa ukifufuliwa utasaidia katika kuitumia vya kutosha hazina ya msamiati kutoka katika Kiswahili chenyewe na kwa namna hii kudhihirisha kuwa Kiswahili, kama lugha yoyote ile kina uwezo wa kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

J.S. Mdee (1986) anasema:

> "... kusema kweli kiswahili kina maneno mengi ya kuweza kueleza dhana kadha, lakini kutoyajua kwetu kumetufanya kufikiri kuwa maneno hayo hayapo na kulazimika kuunda au kutohoa maneno kwa dhana hizo. Maneno haya yatafutwe kutoka kwa wazungumzaji wa fani inayoshughulikiwa... Waunda maneno hawana budi kudurusu kamusi za kiswahili ili wayafahamu maneno mengi ya Kiswahili wasiyoyajua ambayo wangeweza kuyatumia kueleza dhana mpya badala ya kutohoa au kuunda neno jipya." [26]

Kauli ya mtaalamu huyu ina uzito na kama itazingatiwa na wataalamu wa TUKI hatuna shaka kuwa watapiga hatua moja mbele katika harakati zao za kuendeleza Kiswahili. Isisitizwe hapa kwamba maneno kiasili au msamiati wa zamani upo siyo tu katika kamusi za zamani za Kiswahili, bali pia katika lahaja na kazi za kale za fasihi ya Kiswahili. Kuhusu suala hili,

E. Kezilahabi (1983) anasema:

> "Utenzi wa Hamziya ndio umetumia lugha ya zamani kuliko tenzi zingine. Lugha iliyotumika ni Kingozi ..... Utenzi wa Mwana Kupona (1858) ndio utenzi pekee wa zamani ulioandikwa na mwanamke na kuacha athari kubwa katika maisha ya ndoa pwani kaskazini ..... Utenzi wa Fumo Liyongo (1932) ndio utenzi pekee wa zamani wenye athari chache sana ya nje. Ni utenzi wa Kiafrika zaidi... upande wa mashairi...

mshairi aliyejulikana sana ni Muyaka bin Haji (1776 - 1840)...." [27]

Kutokana na kauli hii ya Kezilahabi ni wazi kwamba msamiati wa zamani upo katika fasihi ya zamani ya Kiswahili kama vile Utenzi wa Tambuka (1728) ulioandikwa na Bwana Mwengo, Utenzi wa Hamziya (1749) au (1652) ulioandikwa na Sayyid Abdarus, Utenzi wa Al-Inkishafi (1810 - 1820) ulioandikwa na Seyyid A Nassir, Utenzi wa Mwana kupona ulioandikwa na Mwana Kupona, na katika mashairi ya Muyaka, Fumo Liyongo, M.H. Mbega na A.N.J. Bhalo.

Aidha, msamiati wa zamani ukipewa nafasi katika maandishi ya kila siku (badala ya kufufuliwa na kupanuliwa kimaana) utasaidia katika kupunguza na kutatua tatizo la uundaji wa msamiati usioeleweka kwa urahisi. Suala hili ni muhimu sana kwa sababu msamiati kama huo huenezwa na vyombo vya habari - magazeti, runinga, na mwengoya (radio) pasi na kuwaeleza wazungumzaji maana zake. Wapenzi wa lugha hii huachwa wakiwa katika hali ya kutoelewa maana kamili ya kinachoelezwa. Kwa mfano, neno Kupe ambalo maana yake asilia ni mdudu, kwa sasa linaeleweka kama 'mnyonyaji'.

Magendo maana asilia ni mikono ya kaa ya mbele, kwa sasa linatumiwa kwa maana ya kufanya biashara kwa njia isiyo halali.
Hali kadhalika utohoaji wa neno la Kiingereza "allowance" kuwa ni alawanzi kama linavyotumika Bungeni hapa Kenya ni suala lingine ambalo huacha wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wakijaribu kudadisi maana yake bila ya kufikia uamuzi dhahiri unaohitajika.

| | P | E | G | I | T | O | S | A | Alama |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9a. Mapumziko Leave | 2 | 1 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4.5 |
| 9.b Sono | 3 | 4 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0.5 |
| 10.a Ritaya | 2 | 2 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4.5 |
| 10.b Staafu | 2 | 2 | 0.5 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| 10.c Tuta | 4 | ,2 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7.5 |
| 11.a Fokasi Focus | 1 | 2 | 0.5 | 0.5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| 11b. Wewendu | 4 | 2 | 0.5 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 9.5 |
| 12.a Mboo Penis | 0 | 1 | 0.5 | 0.5 | 2 | -2.5 | 0 | 0 | 1.5 |
| 12.b Ume | 4 | 2 | 0.5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7.5 |
| 13.a Matako | 2 | 2 | 0.5 | 0 | 1 | -3 | 0 | 0 | 2.5 |
| 13.b Mabogi | 2 | 2 | 0.5 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 7.5 |
| 13.c Makaliyo | 3 | 1 | 0.5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 6.5 |

Msamiati unyumbuzi, kipasasauti, epiki, kiuajisumu, elimunyota umefaulu jaribio la PEGITOSA kwa kupata alama za juu.

Aidha, msamiati wa zamani wote ila tu ndwele umepita jaribio la PEGITOSA. Msamiati kiasili ndwele umeanguka kwa sababu hauna uangafu. Hali kadhalika msamiati avolushoni, mayikrofoni, utendi, ngoamwili, kutofaulu kwao kunatokana na ukosefu wa sifa ya udhahiri na uangafu. Kwa usemi mwingine msamiati huu hauna 'mwonjo' ama 'ladha' ndiposa haujafaulu jaribio la vigezo vya PEGITOSA.

Isisitizwe pia kwamba neno 'astronomy' linapotoholewa na kuswahilishwa kwa maana ya astronomia, halifaulu jaribio hili kwa sababu halina uangavu jambo ambalo linatokana na kuwepo ugeni mwingi ndani yake. "Astronomy' kwa maana na unajimu pia linakataliwa kwa sababu halipigi dipo, si angavu kwa maana kwamba unajimu ni 'astrology' na wala si 'astronomia' (Kiingi (1989).

.../74

Kutofaulu kwa msamiati <u>mboo</u> kunatokana na uchafu au ukali wake. 'Mboo' ni neno ambalo halizingatii adabu ya lugha ya Kiswahili. Msamiati huu haukubaliki kutokana na sifa ya utamaduni au miiko. Hata hivyo, tunakubaliana na H.J. Mwansoko [28] kwamba kila lugha ina mbinu zake za kutotumia maneno makali. Mfano mbinu ya tasifida katika Kiswahili.

I. Mbaabu (1989) hakosei anapopendekeza kwamba:

> ".... msamiati wa mila na utamaduni, yafaa ubuniwe na baraza la wazee likiongozwa na taratibu maalum. Maneno mapya ya kiutamaduni yanapohitajika hayana budi kuambatanishwa na msamiati asilia wa kiswahili kiasi iwezekanavyo..." [29]

Maoni ya aina hii ndiyo yamewahi kutolewa na wataalamu wengi lakini kwa bahati mbaya hayajapewa uzito unaohitajika. Maoni haya yakifuatwa msamiati wote wa Kiswahili hautaenda kinyume cha utamaduni wa Waafrika.

Tumekwishadokeza hapo juu kwamba msamiati kiasili wa Kiswahili umepata alama za juu na hivyo kufaulu jaribio la sifa za PEGITOSA. Kufaulu huku kunadhihirisha wazi umuhimu wa msamiati wa zamani wa kiswahili uliokufa.

Ni kutokana na umuhimu huo ndipo tunapendekeza kwamba msamiati wa zamani utumiwe kama msingi wa kuona maneno yapi yatumike katika Kiswahili na namna ya kuunda msamiati mpya wa Kiswahili.

Isitoshe, ni kutokana na umuhimu wa msamiati kiasili ndipo tunapendekeza pia kwamba upewe nafasi kupitia kwa vikao mbalimbali, maandishi na wanafunzi shuleni na vyuoni wafundishwe maneno ya zamani. Mfano zaidi wa msamiati wa zamani uliosahaulika katika kiswahili sanifu ni:-

| | |
|---|---|
| mwele | mgonjwa |
| tobwe | mjinga |
| nyemi | furaha |
| tuhuma | wasiwasi/shaka |
| misimbo/nidhaa/nazaa | aibu |
| pujuliko | huzuni |
| kondo | vita/nguvu |
| taliba | matakwa |

(Tazama M.H. Abdulaziz (1979) katika Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry)

Hatuna budi kukumbuka kwamba maendeleo ya lugha yoyote ile hutegemea namna wataalamu wake wanavyoshirikiana na wanavyozingatia wanavyokoselewa pasi na kuvunjika moyo. Wanaleksikografia wa kiswahili watafanikiwa mno katika harakati zao za kuendeleza leksikoni ya lugha hii iwapo watafuata maoni ya watu wengine, wazee kwa vijana, na wasomi wengine kwamba waache kuziwekea uzito mkubwa lugha za kigeni. Kwa muda mrefu sana, lugha za kigeni zimeonekana kama kwamba ndilo kapu au ngala wanamochota msamiati/istilahi zinazohitajika katika Kiswahili. Jambo au tendo hili na likome ikiwezekana.

Pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka katika kiswahili chenyewe na tubuni, tusikope.

A. Khalid (1977) anasema:

> "Kihibrew kilikuwa kimekufa kwa muda wa zaidi ya miaka elfu mbili, lakini Waisraeli kwa kutokubali muundo wa Kijerumani (Yiddish) uliokuwa umechafuliwa, waliikata isiwe ndiyo lugha yao ya Taifa. Walifufua maneno yao ya zamani yaliofungamana na utamaduni wao ambayo yalikuwa yamekufa kwa karne nyingi..." [30]

Dondoo hili, linahidhirisha kuwa lugha inaweza kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo pasi na kutegemea ama kukopa msamiati kutoka lugha za kigeni. Kutotambuliwa ama kutofikiriwa kwa msamiati kiasili mwingi katika kiswahili sanifu ni mojawapo ya suala zima la kubeza lugha hii na baadhi ya wataalamu kuwa haina msamiati wa kutosha.

Kadhalika tunaweza kusema kuwa taadhima au hadhi au nafasi ya chini iliyopewa msamiati wa zamani wa kiswahili kwa wakati huu inatokana na mawazo ya baadhi ya wataalamu, hasa watetezi wa ukopaji, kwamba 'hakuna lugha ulimwenguni isiyokopa'. Sisi, ingawa tunaelewa kuwa ukopaji ni mbinu mojawapo ya kupanua lugha kimsamiati, tunapendekeza kwamba ukopaji usitiliwe uzito sana. Utumiwe tu iwapo hapana njia nyingine ya kukuza lugha ya Kiswahili. Iwapo ipo, na njia hiyo itumiwe.

Fauka ya hayo, tukizingatia nafasi ndogo iliyopewa msamiati kiasili kwa wakati huu, tunaweza kusema kuwa wengi wa wataalamu wa kiswahili wametawaliwa na kasumba za kikoloni zinazowafanya wasione uwezekano wa lugha hii wa kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

.../77

A.M. Khamisi (1985) anasema:

> "Kama ilivyo katika mambo mengine mengi, kila lilio na nia ya maendeleo haliachi kupakwa matope na kushtumiwa kwa kila hali.... Juhudi za kukikuza Kiswahili kitumikie watu haziwezi kukwepa pingamizi...." [31]

Tunafahamu kuwa pendekezo letu la kufanya msamiati wa zamani upewe nafasi kubwa baada ya kuhuishwa na kupanuliwa kimaana kama njia mojawapo ya kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, kama anavyodokeza Khamisi (ibid) halitakwepa pingamizi. Tatizo la 'ukubalifu' lipo. Hata hivyo itakuwa vizuri wanaleksikografia wa kiswahili wakiutambua na kuupa msamiati kiasili nafasi katika maandishi ya kila siku kwa ajili ya maendeleo ya lugha hii.

Yatubidi tukubali kutokana na mifano tulizotoa kwamba uwanja wa msamiati wa zamani uliokufa ni mpana sana na tunatumia sehemu ndogo tu ya msamiati wa Kiswahili.

Na ni dhahiri kuelewa kuwa msimamo na madai ya baadhi wa watetezi wa ukopaji umepotoka kwani iwapo tutayakubali itakuwa tunasema kwamba Kiswahili hakiwezi kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo pasi na kukopa msamiati wa kigeni ambalo si kweli kabisa kulingana na ulimwengu wa leo unaotuhitaji tuwe wabunifu zaidi katika kukuza lugha. Kuhusu suala hili M. Ali (1966) anasema:

> " Sehemu kubwa ya watu waliotia maneno ya Kiarabu katika kiswahili ni watu wa pwani... kwa kuwa watu hawa waliwapenda Waarabu na ustarabu wao, kama hivi leo watu wanavyopenda ustaarabu wa Wazungu... waliipenda lugha yao. Kwa kupenda lugha yao waliyachukua maneno yao na kuyatia katika Kiswahili."

.../78

Naye Y.M. Kihore (1983) anadai kuwa:

> "Hadi leo Kiswahili bado kinaendelea kuchukua maneno toka lugha za kigeni. Nafikiri litakuwa jambo la kufurahisha ikiwa uchunguzi utafanywa kuonyesha ni vipi na kwa kiasi gani kuingizwa kwa maneno ya kigeni katika Kiswahili kunavyoendelezwa na mapenzi tuliyo nayo kwa watu fulani na lugha zao.." [33]

Sisi, ijapokuwa tunafahamu kuwa kwa kawaida lugha hujikuta tu ikikopa kutoka kwa lugha zilizoingilia mazingira yake, na kwamba maneno ya kigeni yaliingia katika kiswahili kwa njia ya kawaida mno, lakini hatuna budi pia kukubaliana na Ali (ibid) kwamba ukopaji mwingi wa msamiati kutoka lugha za kigeni huenda ulitokana na wazungumzaji wa kiswahili, wasomi kuyaonea fahari maneo ya kigeni na lugha wanazokopa maneno hayo. Kwa namna hii si ajabu kwamba msamiati kiasili wa Kiswahili umepewa nafasi ndogo katika maongezi na maandishi ya kila siku na katika shughuli rasmi popote lugha hii ipoongelewa. Ukweli wa madai haya, kama anavyosema Kihore (1983) utahitaji uchunguzi na utafiti wa kina kirefu. Kwa hakika hakuna sababu muhimu ya kutoingiza msamiati kiasili/wa zamani katika maandishi ya kila siku. Kufanya hivyo kutaipanua lugha hii ya Kiswahili kileksia.

### 2.2.3 Muhtasari

Katika kutamatisha kura hii ya pili, hatuna budi kukiri kwamba mifano tuliyotoa hapo juu ya msamiati wa zamani 'uliokufa' ni ushahidi tosha kwamba upo na unapatikana katika lahaja na katika kazi za zamani za fasihi lakini hautumiki kwa sasa katika maandishi ya kila siku. Tumependekeza kwamba msamiati kiasili uliokufa, ufufuliwe. Ukifufuliwa na kupewa nafasi katika maandishi ya kila siku utasaidia kuziba

mapengo ya msamiati maalum/istilahi. Ufufuaji wa msamiati wa zamani uliokufa utawezesha wataalamu wa TUKI kuepuka kuunda msamiati kwa dhana ambazo tayari zina msamiati kiasili zenye kuziwakilisha. Haya na mengine mengi ndiyo yameshughulikiwa katika sura hii ya pili.

# SURA YA TATU

## 3.1.0 Utangulizi

Mbinu zinazotumika kuundia msamiati wa Kiswahili ni jambo ambalo hatuwezi kuepuka kulitazama na kumulika palipo udhaifu katika mbinu hizo, udhaifu ambao ndio unatuelekeza kutambua umuhimu wa njia ya ufufuaji wa msamiati wa zamani katika kuendeleza leksikoni ya kiswahili. Aidha, ni kutokana na uchunguzi wa makini wa mbinu au taratibu zinazotumiwa na wataalamu wa TUKI ndipo tutafikia uamuzi iwapo kweli pana haja ya kuunda msamiati mpya ama kinachohitajika kwa upande wa TUKI ni kupekuwapekuwa miongoni mwa Waswahili wenyewe na kuupata msamiati wa zamani ambao waweza kuhuishwa na kupewa matumizi mapya pale ambapo hapana neno mwafaka.

Izingatiwe kutokana na utangulizi huu lakini, kuwa mifano tutakazotoa ni baadhi tu ya taratibu zinazotumiwa kuunda msamiati wa Kiswahili, lengo letu hasa likiwa ni kueleza udhaifu na kutokomaa kwa uundaji wa msamiati wenyewe. Fauka ya hayo, tunanuia kupendekeza mbinu (au utaratibu) maalum ya kuunda msamiati wa Kiswahili ambayo haitakiondolea 'uswahili' wake lugha hii.

Jambo hili tutalitekeleza baada ya kuzichunguza baadhi ya mbinu zitumikazo kwa sasa kama vile, ubunaji, kaleki, uambatanishaji, akronimu, uhulutu, uradidi, unyambuaji na uambishaji na kadhalika.

### 3.1.1 Dosari na Udhaifu katika taratibu za uundaji wa msamiati

Kabla hatujajadili palipo udhaifu na dosari katika taratibu za uundaji wa msamiati wa kiswahili hatuna budi kueleza kinachofikiriwa kuwa ndicho chanzo au kisababishi cha dosari na matatizo hayo licha ya kwamba kumekuwepo na mafanikio fulani yaliyopatikana kufikia sasa.

K.B. Kiingi (1992) anadai kuwa uundaji wa msamiati/istilahi za Kiswahili haujakomaa kwa sababu mbili kuu. Kwanza, ni kwa sababu wanaoshiriki wameathiriwa sana kimawazo na mbinu za kigeni za kuunda msamiati. Pili, wataalamu wanaoshiriki katika harakati za kuunda msamiati hawashirikiani vya kutosha katika kutumia msamiati kiasili na msamiati wa kilahaja kama msingi wa kuona maneno yapi yatumike katika Kiswahili na utaratibu maalum ufaao zaidi wa kuunda msamiati mpya.

Mtaalamu huyu anadokeza pia kwamba wanaleksikografia wa Kiswahili wanachofanya hasa ni kuunda maneno kwa 'kuyaboresha' yaliyoko ya kigeni kwa kuyaswahilisha na huu, kwa maoni ya Kiingi ni udhaifu mkubwa.

Maoni ya aina hii yanamchochea kila mzungumzaji wa lugha hii kujiuliza ni kwa nini kufikia sasa hakuna utaratibu bora zaidi ambao umetambuliwa kwamba utumike katika kutunga msamiati mpya wa Kiswahili ili dhana mpya katika Kiswahili zipewe majina kwa urahisi!

Kwa kiasi kikubwa tunakubaliana na Kiingi kwamba suala la kukuza lugha linahitaji ushirikiano wa wataalamu wa Kiswahili. Lakini ukosefu wa ushirikiano tu hautoshi pana na zaidi ya - kwa mfano, ni udhaifu kwa mwanaleksikolojia kuunda msamiati mpya kabla ya kuchunguza iwapo kiswahili chenyewe kina msamiati huo ambao labda ulisahauliwa katika kiswahili sanifu, au bila ya kutafiti iwapo hakuna neno/msamiati jingine lilikokwisha kuundwa kwa ajili ya dhana hiyo.

Kuhusu udhaifu katika taratibu za uundaji wa msamiati J.S. Mdee (1986) anasema:

> "Uundaji wa maneno kwa kunyambua na kuambisha au utohoaji sio uundaji halisi wa maneno kwani tayari yapo katika lugha zinazohusika. Maneno hayo yapo katika lugha iliyolengwa ikiwa ni mnyambuliko au katika lugha chasili iwapo maneno hayo yametolewa kwa mfano dayosisi (diocese)..."[34] (Msisitizo ni wetu).

Mdee, kutokana na kauli hii, amegundua udhaifu katika taratibu za kuunda maneno za unyumbuaji na uambishaji na utohoaji. Maoni ya mtaalamu huyu yana mashiko na tunakubaliana naye kwa sababu moja muhimu. Imekuwa si rahisi kwa mzungumzaji asiyejua lugha chasili kuelewa maana ya maneno/ msamiati mapya yaliyoundwa kwa utohoaji. Kwa mfano, iwapo mzungumzaji hajui kiingereza hawezi kuelewa maana ya maneno mapya ya Kiswahili wala dhana inayowakilishwa hapa:

(utohoaji) footnote ——— futinoti (tanbihi)
godfather ——— babamungu
typewriter ——— taipreta

hansard————hanzadi (Shajara ya bunge)

shorthand————mkonomfupi (hatimkata)

atom————atomu (tonoradi)

(Unyumbuaji)

absorption————ufyonzaji

absorptively————mfyonzo

alcohol————alikoholi

alcoholic————alikoholiki (?)

Waundaji wa msamiati wa Kiswahili wameitambua njia ya ukopaji ama utohoaji wa msamiati kutoka lugha za kigeni kama njia moja muhimu sana ya kupanua leksikoni ya Kiswahili. Hatukatai wala si lengo letu kusema 'tusikope'. Lakini inafaa ieleweke kwamba ukopaji ama utohoaji si ubunaji. Kinachohitajika sana kama tulivyoeleza mbeleni, ni kuwa wabunifu. Kwa mfano tukitohoa atom - kuwa atomu tuwe na uhakika wa kueleza atomic, atomise, atomasation, atomicity na kadhalika. Madai kwamba kila lugha hukopa na hivyo Kiswahili hakina budi kukopa yameshikiliwa na wasomi na wataalamu wengi.

L.P. Imbuhila (1991) anasema:

> "... Ingawa Kiswahili kina maneno mengi ya mkopo, hili silo jambo la aibu kwani lugha nyingi duniani zimekopa msamiati kutokana na lugha zingine. Kiingereza kina asilimia 85 ya maneno ya kukopa..." 35

Naye S.H. Olson (1972) anasema:

> "Lugha inapokopa huonyesha uwezo wake wa kujimudu.... ukopaji ni sifa ya lugha zote..." 36

D.M.W. Njeru (1990) anaafikiana na Olson (ibid). Ingawa ukweli kwamba kila lugha ulimwenguni hukopa haupingiki, ni kweli pia kuwa Kiswahili kinaweza kujitegemea pasi na kuendelea kukopa maneno ya kigeni. Hata hivyo pana haja ya kusema kuwa ukopaji kwa sababu kila lugha hukopa ni madai ambayo hayana msingi katika ulimwengu wa leo kwa maoni yetu.

C.W. Temu (1972) yuasema:

> "Maoni yangu ni kuwa Kiswahili kinaweza kuunda maneno yote yanayohitajika kueleza yote kinachotaka katika nyanja zote zikiwemo za kisayansi. Kinachohitajika ni kubadilika kwa fikira... katika kuunda msamiati."[37]

Maoni haya ya Temu yana uzito na sisi tunakubaliana naye kwamba udhaifu katika taratibu za uundaji wa msamiati unatokana na fikira walizonazo wanaleksikografia wa Kiswahili. Wataalamu wa TUKI kwa mfano, wamezipendelea taratibu fulani (na msamiati) za uundaji wa msamiati kwa sababu kwao ndizo zinazopendeza masikio yao. Jambo hili la kimazoea ama kupendelea utaratibu fulani kuwa ndio ulio na 'ladha' zaidi ndilo, kwa maoni yetu limewafanya wasijitokeze na mbinu maalum ya kuunda msamiati wa Kiswahili ambayo itahifadhiwa na kuzingatiwa na mataifa yote na itakayotumika kwa urahisi kutoa majina kwa dhana mpya zinazokusudiwa kuwakilishwa. Udhaifu huu uletwao na sababu za mazoea ya kupendelea msamiati ama mbinu fulani kuundia msamiati wa Kiswahili, ukiepukwa bila shaka waundaji maneno watapiga hatua moja mbele katika shughuli zao za kukuza lugha hii ya Kiswahili.

Baada ya kueleza chanzo au visababishi vya udhaifu katika taratibu za kuunda msamiati wa kiswahili, pana haja ya kufafanua palipo udhaifu wa kuzingatia kila mojawapo ya utaratibu utumiwayo na wataalamu wa TUKI.

3.1.2 Utaratibu wa ubunaji (creativity)

Si rahisi kutoa kijelezi mwafaka cha 'ubunaji' kwa sababu ya utata wa neno hili.
S.A. Nabhany anaeleza ubunaji kama ni kujiudhi bongo na kujikera mpaka kulipata neno la kufaa. Ufafanuzi huu ni finyu mno kwa maoni yetu.

Suala la Ubunifu labda litaeleweka vizuri tukitazama mawazo ya F. de Saussure (1959) kuhusu dhana ya lugha. Izingatiwe hapa kwamba fikira ya kimsingi zaidi ya ubunaji (creativity) ilitolewa na mtaalamu huyu.

Kwa maoni ya Saussure mwanalugha anatakiwa atambue kuwa kila lugha huvua msamiati tofauti-tofauti katika tabaka la sauti zilizopo ndani ya "langage". Kutokana na sauti hizo yeye huunda msamiati au nomino katika uhusiano wa kiupekee ambao kwa upande wake huunda kwanza "parole" kisha "langue" na jinsi wakati unavyopita dhana hizi mbili hudumu katika uhusiano wa kutegemeana.


"Langage" - ni ghala la lugha zote duniani. Katika ghala hili ndipo kuna kanuni za mfumo wa lugha zote duniani. Aidha, katika

'langage' tunapata sifabia za lugha za ulimwengu wote. Kutokana na 'langage' kila jamii-tumizi-lugha hunyopoa vipande (sauti) kulingana na uwezo na mahitaji yao mbalimbali.

Mbali na jinsia nyingine za kutazamia lugha, de Saussure alibainisha kati ya lugha ikifikiriwa kama "langue" na kama "parole".

"Langue" - ni lugha dhahnia, ni mfumo imara, au lugha mahususi inayotumiwa na jamii fulani. Lugha hii haiwezi kufanyiwa mabadiliko yoyote pasi na kuwepo makubaliano ya jamii nzima. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na kadhalika.

"Parole" - ni lugha tumizi. Ni lugha katika hali ya matumizi yaani ni tabia ya matumizi ya lugha ya mtu binafsi katika maongezi na maandishi. Tazama mchoro kwa maelezo zaidi.




Ubainishi wa Saussure kwa hakika unaingiliana na ubunaji unaohitajika katika kuunda msamiati wa Kiswahili, kwa njia ya moja kwa moja. Hata ule wa Chomsky (1965) pia kati ya

"uwezo-lugha" na "utendaji"/umilisi unaelekea kuongea juu ya ubunifu. Maulana hawa Chomsky na Saussure maelezo yao yanatufaa zaidi katika kujadili suala la ubunifu. Jamii ina uwezo wa kutomruhusu mtumiaji lugha fulani kujitokeza na msamiati fulani alioubuni. Hivyo de Saussure hajakosea kwa kuihusisha lugha na "langue" (mfumo wa lugha imara wa jamii). Kadhalika Chomsky hajakosea anapoihusisha lugha na "Parole" (utendaji).

Kila binadamu ana uwezo-lugha (competence) na anautumia uwezo-lugha huo kwa kubuni majina/msamiati mpya katika hali ya 'umilisi' (performance).

Ilivyo ni kwamba neno "ubunaji" limetumika vivi hivi tu kama kwamba linajieleza lo lenyewe, ilhali uchunguzi uliofanywa unadhihirisha kuwa linawakanganya wazungumzaji wengi wa lugha ya Kiswahili. 'Ubunaji' kutokana na maelezo ya Saussure unapatikana katika "Parole Ubunifu ni uwezo wa kujitokeza na fikira za kiisimu zinazomwezesha mwanalugha kujenga msamiati mpya ambao haujawahi kutolewa hapo awali kutoka ujumla-lugha.

Uundaji wa msamiati kwa utaratibu wa ubunaji wa suala geni. J. Kitsao (1989) anasema:

> "Kuna pia na kupanua lugha kwa kuibunia maneno mapya. Hapa wanalugha, wataalamu na wajuzi wa lugha inayohusika, huunda maneno kufuatana na muundo (mofolojia) wa lugha hiyo na kuyapa maana inayohitajika ili kuziba pengo liliopo katika mawasiliano kwa lugha hiyo..." [38]

Maoni ya Kitsao yana uzito na tunakubaliana naye. Miongoni mwa wataalamu ambao wamewahi kutumia utaratibu wa ubunaji katika

UNIVERSITY ... NAIROBI

kuikuza lugha ya Kiswahili ni S. Robert (1956), M.S. Abdallah (1976).

M.S. Abdallah (1976) katika Mwana wa Yungi Hulewa anasema:

> "... na 'kupeleleza' ni kuduhusi na kudukiza jambo kwa kulidunzi pamoja na kulipekua na kulichakura...."[39]

Naye S. Robert (1956) katika Wasifu wa Sinti Binti Saad anasema:

> " kujikimu ni kujiruzuku. kujiruzuku ni kujitegemea kwa chakula, nguo na masurufu mengi katika maisha..."[40]

Jambo muhimu la kusisitiza hapa ni kuwa utaratibu wa ubunaji licha ya kwamba haujatiliwa uzito ipasavyo, ndio bora zaidi na hakuna dosari au udhaifu wowote ambao tungeweza kuutoa. Ni utaratibu muhimu sana wa kuunda msamiati wowote unaohitajika katika mwanda wa sayansi na ufundi, mwanda ambao Besha (1972:30) anadai ni vigumu kuwakilishwa kwa Kiswahili.

### 3.1.3 Ukopaji/Utohoaji

Utaratibu wa ukopaji umewavutia wanaisum kama Mdee (1986), Myachina (1981), Shariff (1988), Mukhwana (1988), Mutahi (1979), Abdulaziz (1989), Njeru (1990), Massamba (1987), Temu (1984), na Imbuhila (1991).

Katika Istilahi-Kiingereza-Kiswahili (1987) neno "mkopo" linaelezwa kama:

> "neno lililo chukuliwa kutoka lugha moja na kuingizwa katika lugha nyingine baada ya kufanyiwa marekebisho lili lilingane na muundo wa maneno ya lugha linakoingizwa" 41

Mukhwana (1988) anaeleza utohozi kama:-

> "Namna ya kuunda majina hivi kwamba maneno ya lugha changizi yanafuata muundo wa lugha pokezi". 42

Katika kazi hii tunachukulia ukopaji na utohoaji kwa maana ya uswahilishaji wa maneno ya kigeni. Sisi hatuoni sababu yoyote ya kuweza kuyatenga maneno haya mawili yaani ukopaji na utohoaji kama wanavyofanya Mdee (1986), na Mukhwana (1988).
Aghalabu lugha inapokopa msamiati kutoka lugha ya kigeni, huutohoa ili ukubaliwe na muundo wa lugha pokezi kifonolojia na kimofolojia.

M.H. Abdulaziz (1989) kuhusu ukopaji anasema:

> " Maelezo ya kiisimu ni kwamba kutokana na maingiliano kati ya Waswahili na Waarabu kwa karne nyingi, Kiarabu ni changizi cha Kiswahili kama ilivyo Kigiriko - Latini kwa lugha za Ulaya. Ukopaji wa moja kwa moja kutoka Kiingereza aghalabu unaonekana kuwa si kawaida na kwa hivyo haukubaliki. Jamii-uwili lugha katika Kiswahili na Kiingereza haitambui chanzo cha ukopaji, iwapo ukopaji wenyewe umetoka katika Kiarabu ukilinganisha na ilivyo kutoka katika Kiingereza. Wale tu ambao wanakijua Kiarabu ndio wawezao kujua ukopaji utokao katika Kiarabu, hasa iwapo neno lime swahilishwa muundo kabisa kifonolojia na kimofolojia" 43

Kutokana na kauli ya mtaalamu huyu ni dhahiri kwamba ukopaji na uswahilishaji wa msamiati kutoka lugha ya Kiarabu ni suala la kawaida muno linalotokana na maingiliano ya lugha hizi mbili ya muda mrefu. Sisi hatuna sababu yoyote ya kuushuku msimamo wa Abdulaziz.

Ana sababu zake za kumfanya atoe madai hayo. Hata hivyo, tofauti na mtaalamu huyu anaitambua kuwa ukopaji kutoka kwa Kiarabu kuwa hakutambuliki kwa urahisi, sisi tunashikilia kwamba tusikope ikiwezekana. Inafaa tueleza hapa kwamba ukopaji wa msamiati mwingi wa Kiarabu kama vile

ahera

allah

baraka

fedha

deni

sheria

elimu

sabuni

urithi - umefanya Kiswahili kichukuliwe na baadhi ya wataalamu kuwa hakina msamiati wa kutosha, madai ambayo ni potovu kwa maoni yetu. Aidha, suala la wapi pa kukopa, kama tulivyoeleza katika sura ya kwanza, si lengo letu. Tunalosema sisi ni kuwa ikiwezekana pale ambapo hapana neno mwafaka na tutumie utaratibu wa ubunaji ama tufufue na kuyapa maneno kiasili ya Kiswahili matumizi mapya.

Labda kabla hatujajadili udhaifu wa mbinu ya ukopaji itafaa zaidi tukiwarejelea wataalamu 'wanaojivunia' mbinu hii na kuelewa msimamo wao hasa.

N.I. Shariff (1988) anasema:

> "... utajiri wa lugha, nguvu zake na uwezo wake wa kudumu na kukidhi haja za wanaoitumia ni uwezo wake wa kuazima maneno ya lugha nyingine na kuyafanya yake."[44]

Naye W.C. Temu (1984) yuasema:

> "maneno yanayokopwa yaswahilishwe ili yafuate fonolojia ya Kiswahili lakini maana haina budi kubakia kama ilivyokuwa katika lugha changizi... utaratibu huu ndio kwa sasa zalishi zaidi hasa katika mwanda wa sayansi"[45] (Tafsiri yetu)

D.M.W. Njeru (1990) na P.I. Imbuhila (1991) wanaafikiana na Temu (1984) kwamba ukopaji ni mbinu zalishi zaidi (most productive) katika kuunda msamiati wa Kiswahili na wanatoa mifano ya maneno yafuatayo:

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| bicycle | baiskeli |
| mudguard | madigadi |
| democracy | demokrasia |
| speaker | spika |
| softboard | softibodi |

Maneno yaliyokopwa kutoka kwa Kihindi ni:

bajia

chokora

dawati

Kireno

gereza

bastola

bendera

meza

Kijerumani

daktari

missioni

aparati

(Taz. Myachina (1981:19)

Ingawa wataalamu hawa tuliowataja wanajivunia mbinu ya ukopaji wa Kiswahili wa maneno ya kigeni (kama vile ya Kiarabu - asante, karibu, urafiki, ufidhuli, umati) na kuyaswahilisha, sisi tunatofautiana nao kwa sababu ya udhaifu mwingi wa mbinu hii.

Kwanza kabisa ukopaji wenyewe unafanywa 'vivi hivi tu', huu ukiwa udhaifu mkubwa katika utaratibu huu wa ukopaji ama utohoaji wa kuunda msamiati. Isitoshe, baadhi ya msamiati/istilahi wa Kiswahili unaoundwa na wataalamu wa TUKI kwa kufuata mbinu ya ukopaji, unaundwa pasi na kuzingatia mfumo maalum (no systemicity). Kwa mfano, iwapo tunachukulia, kama anavyopendekeza M.H. Abdulaziz (1989: 38) ukopaji wa kotekote kwa maneno

hydrogen ——— haidrojeni

hydrate ——— haidrate

hydration ——— haidrashoni

hydrogen-oxide — haidrojeni-oxide

Basi na hydropily itakuwa haidrofilia

hydrophte haidrofita

hydrotropism haidrotropismu.

Tunatofautiana na mtaalamu huyu katika pendekezo hili. Hata hivyo ikiwa tunakubali kuwa

artery ——— ateri

glycerol ——— gliseroli

alcohol ——— alcoholi

calcium ——— kalsiamu basi hatuna budi kuafikiana na Abdulaziz katika pendekezo lake la utohoaji sisisi wa msamiati wa sayansi.

K.B. Kiingi (1992) anasisitiza kwamba msamiati wa sayansi hauna budi kufuata taratibu maalum. Kwa mfano,

| Kigeni | Kiswahili | Mifano |
|---|---|---|
| hydro | - maji | hydrogen = kiunda-maji |
| -phyte | mea | hydro-phyte = kimeamaji |
| | | palo-phyte = kimeachumvi |
| | | neo-phyte = kimeachanga |

Katika mfano huu ile 'hydro' na 'phyte' inarejelewa na kuna utaratibu maalum unaofuata jambo ambalo hatulioni likitiliwa manani na wataalamu wa TUKI katika maneno yafuataο:-

hydrophyte - yungiyungi
hydrogen - haidrojeni
hydrotropism -ubadilihali

Iwapo ukopaji, hasa kutoka kwa Kiingereza utawekwa katika hali ya chini itawabidi wataalamu wa lugha ya Kiswahili wafikirie zaidi. Kwa mfano,

iwapo
ectoderm ———— ektodemi
endoderm ———— endodemi
epidermis ———— ngozi nje
ectoplasm ———— uteseli nje

tunadadisi kuwa

derm ⇄ demi
ecto ⇄ ekto
endo ⇄ endo
epi ⇄ nje
ecto ⇄ nje
dermis ⇄ ngozi

Ikiwa hakuna tofauti za kidhana katikati ya -derm na dermis basi ukopaji umefanywa usiohitajika.

Isitoshe, iwapo wataalamu wa TUKI wanakubaliana kuwa

| | | | |
|---|---|---|---|
| neutron | - chembebatili | ) | |
| electron | - chembehasi | ) | Tol. 3.29 |
| proton | - chembehanya | ) | |

basi itakuwaje chembe - particle

batili - neutrally charged

hasi - negatively charged

hanya - positively charged?

Msamiati maalum kama huu ambao umetokana na ukopaji wa 'vivi hivi tu' hauna budi kufanyiwa usahilisho (revision) na wataalamu wa TUKI na BAKITA (Kiingi (1986:146)).

Aidha iwapo tunakubali kuwa

fuse ———— fyuzi

mudguard ———— madigadi

dynamics ———— dainamiki

photometre ———— fotometa

uterus ———— uterasi

(BAKITA) Tafsiri sanifu Toleo la 3 (1978) na Toleo la 4 (1980) itakuwaje basi

| | |
|---|---|
| glacier iwe ni | barafuto |
| plasmagene | utoroji |
| plasmalema | ugozimwili |
| plasmadesmata | kiuzichembe? |

Ni kutokana na mifano hii ndipo hatuna budi kusema kuwa utaratibu wa ukipaji, kama unavyofanywa na wataalamu wa kiswahili haufuati mfumo ulio sawa katika uundaji wa msamiati wa Kiswahili. Inabainika pia kwamba msamiati wa ngeli moja umeundwa kwa namna tofauti. Tazama kwa mfano, ile 'plasma' ya mwanzo hairejelewi katika maneno yote yenye kiambisho hicho katika mfano uliotolewa hapo juu. Dhana ya 'plasma' ambayo inakaririwa katika kila neno lililo katika seti hii haijitokezi katika maneno ya kiswahili na wala hakuna uhusiano wowote unaoonyeshwa kati ya maneno ya Kiswahili. Kila neno ni tofauti kabisa na jingine.

Inafaa tusisitizwe hapa kwamba, ingawa tunaelewa kuwa kila lugha ulimwenguni hukopa, mathalani Kiingereza kimekopa msamiati wa Kiswahili kama vile safari, sufuria, jua kali, lakini hapana haja ya kukopa na kutohoa msamiati ambao hatuuelewi ama hatuelewi dhana zinazowakilishwa na msamiati huo. Hapana shaka kuwa dhana ya fotometa/photometre kwa mfano, ingeeleweka haraka kwa Mwingereza (ama taipreta/typewriter) ambaye anafahamu ni kitu gani na kinatumiwa kufanya kazi gani. Kwa mzungumzaji wa Kiswahili asiyejua kiingereza, fotometa na taipreta yote ni kihindi. Kadhalika kwa falaki (astronomy), msubihi (aloe) au beli (gold ribbon).

Kwa hivyo badala ya kukopa na kutohoa msamiati wa kigeni tusionelewa pana haja ya kufufua msamiati wa Kiswahili uliosahaulika na kuupanua kimaana. Msamiati wa zamani ambao utaeleweka zaidi bila shaka mbali na kuipa lugha hii sura ya Kiafrika.

J.S. Mdee (1986) anasema:

> "... Inapobidi kutohoa maneno ya kigeni utohoaji huo hauna budi kufanywa kwa mfumo maalum na sio kiholela. Ni vema ukifanywa kwa utaratibu ambao utazifanya istilahi za kigeni zenye ruwaza fulani kutoholewa kwa mfumo ulio bayana. Haili halisi ilivyo kwa sasa ni kwamba waunda maneno wameshindwa kuunda sera ya utohoaji hasa jinsi ya kutohoa..." [46]

Ama kwa hakika kauli ya Mdee ina mashiko na tunakubaliana naye kwamba wanaleksikografia wa Kiswahili wanayatohoa maneno kishelabela, pasi na kufuata mfumo maalum. Mifano iliyotolewa hapo inadhihirisha madai haya. Wanaleksikografia wa Kiswahili watahitajika kuamua mfumo maalum wa kukabiliana na mbinu ya ukopaji iwapo ina umuhimu wowote kwao, umuhimu ambao labda sisi hatuuoni.

Bila shaka, kama anavyosema Mdee (1986:119), ukopaji na utohoaji unaelekea kufanywa pasi na kufuata mfumo ulio bayana, jambo ambalo wataalamu wa Kiswahili watahitajika kulifanyia uchunguzi wa undani zaidi.

Aidha, ukopaji wa msamiati wa kigeni unaelekea unafanywa kutoka lugha ambazo zo zenyewe zilikopa kutoka katika nyingine. Dosari hii imemfanya K.B. Kiingi (1989),(akianzia kwenye Luganda,)apendekeze kwamba msamiati wa sayansi kama vile bayolojia, fizikia na kemia uundwe kwa kuazima mofimu moja kwa moja kutoka Kilatini na Kigiriki. Kwa mfano, methane - methani, methene - metheni. Inafaa tutaje hapa kwamba, tayari Kiingi (1992) ameubadili msimamo wake. Anapendekeza kwamba, Kiswahili kifuate mfano wa lugha ya Kichina, ambayo haitegemei

sana Kigiriko-Latini kimsamiati. Badala ya ukopaji, wataalamu wa Kiswahili wanyambue (extrapolate) mofimu za lugha hii yenyewe. Tunaafikiana naye bila shaka kwa sababu unyambuaji wa mofimu za Kiswahili utaipunguzia ugeni na kuiwezesha lugha hii kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo.

Dosari ya utohoaji kutoka lugha kopaji inapatikana katika mifano ifuatayo:-

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| Padri | Padiri |
| focus | fokasi |
| rent | renti |

Neno Padri ni la Kigiriki "Presbiteros" ambapo maana yake ni "mtu mzee". Neno hili lilipokopwa na Kiingereza lilibadilika kimaana. Kwa sasa "Padri" ni mhubiri (Priest).

Kadhalika, neno 'focus' lina asili ya Kilatini ambapo lilimaanisha fireplace (mahali palipo moto). Kiingereza kililikopa na kulibadilisha maana. Kwa sasa 'fokasi' la Kiswahili ambalo limetoholewa kutoka Kiingereza halina maana ile asilia ya 'moto' au 'pahali pa moto' bali ni kudadisi/kutazama kwa makini sana.

Neno'rent' ambalo lina asili ya Kilatini "reddita" likimaanisha income (mapato). Katika Kiingereza maana asilia ya rent ilipunguzwa na pamoja na 'renti' la Kiswahili latumiwa kwa maana ya mapato yatolewayo na wapangaji wa nyumba au shamba. (A.M. Pei (1967:64)).

.../98

Mifano hii inadhihirisha kasoro ya utohoaji kutoka lugha kopaji ambapo hutokea hatari ya kuingiza (ama kuondoa) vipengele ambavyo sio (ni) muhimu katika msamiati uliokopwa.

Ama kwa hakika ni kutokana na dosari na udhaifu uliomo katika utaratibu wa ukopaji/utohoaji uliojadiliwa hapa ndip tuna-pendekeza kama tulivyosema mbeleni, kuwa pana haja ya kufufua na kuupanua kimaana msamiati wa zamani ili utumiwe pale ambapo hapana neno mwafaka, na ikitulazimu tubuni msamiati mpya.

### 3.1.4 Kaleki (Calqueing)

M.H. Abdulaziz (1989) anasema:

> "Kaleki au tafsiri mikopo inahusu kutafsiri istilahi na maneno kutoka lugha chasili hadi lugha pokezi." [47]

Naye D.M.W. Njeru (1990) anaeleza kaleki kuwa ni:

> " namna ya ukopaji ambapo neno lililokopwa hutafsiriwa mofimu kwa mofimu katika lugha inamoingizwa" [48] (Tafsiri yetu).

Ufafanuzi huu wa Abdulaziz na Njeru una mashiko na tunakubaliana nao. Hata hivyo, katika kazi hii tutaichukulia kaleki kuwa ni njia ya uundaji wa msamiati inayohusu tafsiri sisisi, tafsiri ya wazo au maana na tafsiri ya sauti.

Kuhusu dhana ya kaleki S. Julia Falk (1973) anasema:

> "Kila lugha ina njia nyingi za kupanua au kubadili leksikoni yake. Huku ukopaji ukitawala lugha za kiingereza na kiswahili, kwa mfano, Kijerumani

> kimetumia sana mbinu ya kaleki au tafsiri mikopo - njia ya kuunda msamiati kwa kuutafsiri katika lugha pokezi"[49] (Tafsiri yetu).

Kutokana na kauli ya Falk ni wazi kwamba kiswahili, kinyume na ilivyo Kijerumani kinatumia sana mbinu ya ukopaji. Kiswahili katika kupanua msamiati wake hakijazingatia sana utaratibu wa kaleki. Hata hivyo, kuna mifano michache ya kaleki ifuatayo:-

| Kiingereza | | Kiswahili |
|---|---|---|
| horsepower | - | nguvufarasi |
| balanced diet | - | mlo kamili |
| critical realism | - | uhalisia yakinifu |
| management committee | - | kamati ya uongozi |
| enlarging house | - | chumba cha kukuzia |
| free verse | - | ushairi huru |
| publicity section | - | sehemu ya uwenezaji |
| sick leave | - | likizo ya ugonjwa |

(Ohly 1978: 9-10)

Kutokana na mifano hii, panadhihirika kasoro katika utaratibu wa kaleki wa kuunda msamiati. Baadhi ya msamiati unaoundwa kwa kutafsiri neno kwa neno hauna uangafu. Kwa mfano, neno

"sick leave - likizo ya ugonjwa )
"public section - sehemu ya uenezaji) hayapigi dipo

Yana utata mwingi. Likizo maana ya 'leave' na 'uwenezaji' - public ni maneno ambayo yametafsirira 'vivi hivi tu' na yamepotoka.

Hata hivyo, mbinu hii, tukilinganisha na ukopaji, ina umuhimu mkubwa, umuhimu ambao utatambuliwa na wazungumzaji iwapo waunda maneno wataitumia kwa makini bila ya kutafsiri maneno ya lugha ile ngwayo kiholela.

Aghalabu kutafsiri msamiati kusipofanywa kwa makini, kama wanavyodokeza Batibo na Katingula (1980), huweza kupotosha dhana ya msingi iliyokuwa katika msamiati wa lugha changizi/chasili (kama ilivyo katika mfano hapo juu).

Mfano zaidi, "books allowance"- alawenzi ya vitabu (badala ya posho la vitabu

"motion mover" - mtangulizi wa mjadala (badala ya mwasisi wa mjadala)

"scession paper" - Karatasi ya seshoni (badala ya karatasi ya kikao)

Jambo muhimu tunalosisitiza hapa ni kwamba katika utaratibu wa kaleki pana hatari kubwa ya mwanaleksikografia kushindwa kusawiri dhana zilizokusudiwa kama ilivyokuwa katika lugha ya chasili, suala ambalo halina budi kuzingatiwa na wanaoutumia utaratibu huu kuunda msamiati wa Kiswahili.

### 3.1.5 Uambatanishaji (Compounding)

Wataalamu ambao wameujadili utaratibu wa kuambatanisha maneno ni K.B. Kiingi (1982), E. Polome (1967), M.H. Abdulaziz (1989), S.J. Falk (1973), C.W. Temu (1984), P.L. Imbuhila (1991) na M.C. Kapinga (1975) (1983).

Uambatanishaji wa msamiati/maneno ni utaratibu ambao unahusu kuteuliwa na kuchukuliwa kwa majina mawili au hata zaidi na kuyaunganisha ili kuunda jina moja lenye dhana mpya.

Utaratibu wa uambatanishaji umetumiwa sana katika Kiingereza. Mathalani,

Englishman

greenhouse

sunbathe

takeover

a highchair

gatekeeper

breakfast

Falk anasema kwamba uambanishaji ni moja wapo wa utaratibu za kimsingi za uundaji wa msamiati katika lugha yoyote ile. Maoni haya yana uzito kwa sababu na hata katika Kiswahili kuna msamiati mwingi unaoundwa kwa kutumia njia ya uambatanishaji.
Kwa mfano,

mlariba - kutokana na la + riba kwa kuongeza kiambisho cha ngeli ya 1 (m)

mwanakamati

shituamimba

njiapanda (crossroad)

elimunyota (astronomy)

utandoseli (cellmembrane)

kipimatetemeko (seismometer)

fundisanifu (technician)

elimuuyoga

ugozimwili (plasmalema)

Wataalamu ambao inaelekea wamegundua kasoro fulani katika utaratibu wa uambatanishaji ni Abdulaziz (1989), na Falk (1973).

S.J. Falk (1973) anatueleza kuwa:

> "Ingawa maneno mengi ya Kiingereza yameundwa kutokana na utaratibu wa uambatanishaji, utaratibu huu wakati fulani haupigi ndipo na hasa, maneno ambatano mengi yanafanana na 'Jazanda' kwa namna kwamba maana yao haiwezi kufasiriwa moja kwa moja kutokana na mizizi yao iliyoambatanishwa". 50 (Tafsiri yetu)

Kauli ya mtaalamu huyu ingawa inahusu zaidi lugha ya Kiingereza lakini inamulika barabara palipo dosari. Ni ukweli, na tunakubaliana na Falk (1973:36) kwamba si rahisi kuelewa moja kwa moja maana katika maneno ambatano ambapo zaidi ya mzizi mmoja hutumiwa kujenga neno moja.

Mathalani, elimuuyoga (mycology)
kidoletumbo (appendix)
ubadilihali (hydrotropism)

Maneno ambatano haya elimuuyoga, kidoletumbo, ubadilihali yanakosa sifa ya udhahiri na uangafu za PEGITOSA. Mzungumzaji wa Kiswahili wa kawaida atatatizika kufasiri maana ya elimuuyoga hasa iwapo hajui maana ya mzizi uyoga. Kadhalika maneno ambatano kidoletumbo na ubadilihali, hayana udhahiri kwa sababu hayalengi kinachomaanishwa bayana. Neno ambatano ubadilihali linatokana na ubadili wa hali "change of state".

Na kwa vile mbali na 'hydrotropism' kuna 'geotropism' 'phototropism' ambayo pia ni ubadili wa hali, basi si dhahiri

wala hakuna uangafu katika matumizi ya ubadilihali kwa maana ya'hydrotropism.'

M.H. Abdulaziz (1989:38) anadokeza kwamba lugha kama ya Kiswahili haiambatanishiki kwa urahisi. Dhana ambatano, aghalabu huelezwa kwa ujenzi endelezi (a generative construction) kwa mfano,

sodium chloride kama chloride ya sodium.

Anaendelea kudai kwamba suala hili huifanya lugha kama ya Kiswahili kukopa maneno huru kama vile "sodium" na "chloride" pamoja na umbo lao ambatano kama vile katika:

sodiumchloride - <u>sodianikloraid</u>

sodium nitrate - <u>nitratisodia</u>

chloride ion - <u>ion ya kloridi</u>

iron chloride - <u>koloridichuma</u>

hydrochlorid acid - <u>asisi hidrokloriki</u>

sodium hydrogen sulphate - <u>kiberitatihidrojeni-sodio</u>

Maoni haya ya Abdulaziz yana mashiko na tunakubaliana naye kuwa utaratibu wa uambatanishaji una dosari na unafanywa pasi na kufuata mfumo maalum kama inavyodhihirishwa katika mifano hapo juu. Wanaleksikografia wa Kiswahili watahitaji kufikia uamuzi wa mfumo maalum wa kuundia maneno ambatano ili wasiwe wanaunda maneno ambatano yanayowatatanisha wazungumzaji wa lugha hii ya Kiswahili. Maana ya kiambatanishi haiendi kila mara na maana ya sehemu zake. Kwa mfano, "blackboard" yaweza kuwa nyeupe au manjano. Kwa hivyo ni vigumu kufasiri maana inayowakilishwa katika maneno ambatano.

3.1.6 Ufupishaji

Ni njia mojawapo muhimu 'inayotumiwa katika uundaji wa msamiati wa Kiswahili. Kuna aina tatu za ufupishaji

(a) Akronimu

(b) Uhuluti (Blending)

(c) Ukatizaji (Clipping)

Akronimu

Ni aina ya ufupishaji ambapo jina linalotokana na ufupisho wa maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa kuchukua silabi ya kwanza, silabi mbili za mwanzo, silabi tenzi za kati au hata neno nzima.

Wataalamu walioshughulikia dhana ya akronimu ni Temu (1984), Yule (1985), Mukhwana (1988), Njeru (1990). Temu (1984) anadokeza kwamba akronimu ni njia ya uundaji wa maneno kwa kuunganisha silabi za mwanzo wa maneno katika kishazi. Ufafanuzi huu hauna uzito na hautofautishi bayana akronimu na uhuluti.

Njeru (1990:28) anapendekeza kwamba wataalamu wa Kiswahili wajitokeze na kijelezi mwafaka cha akronimu ndipo utaratibu huu ueleweke barabara suala ambalo halipaswi kupuuzwa na wazungumzaji na wataalamu wa lugha hii.

Mifano ya akronimu ni kama ifuatayo:

FUPAJA - mfupa wa paja

TUKI - Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

CHAKINA - Chama cha Kiswahili cha Nairobi

UKIMWI - Ukosefu wa Kinga Mwilini

MSIKWAO - Mtu asiye na Kwao

MKUI - Mkutano wa Kimataifa wa Usanifishaji wa Istilahi (za Kiswahili)

/105

CHAJIO - Chakula cha Jioni

Utaratibu wa akronimu una dosari zifuatazo. Kwanza kabisa, msamiati mwingi unaoundwa kwa utaratibu wa akronimu ni wa muda tu, 'hufa' kwa urahisi muno kama ilivyo vyama au hali mbalimbali zinazowakilishwa na msamiati huo. Hata hivyo baadhi ya akronimu huwa ni za kudumu katika leksikoni ya lugha.

Pili, hakuna mfumo ulio wazi ama kigezo maalum cha kufuatwa wala mantiki katika uundaji wa msamiati kwa utaratibu wa akronimu. Kwa mfano,

Kwa nini UKIMWI lisiwe UPUMWILI
FUPAJA lisiwe MFUPAJA
CHAJIO lisiwe CHAJIONI?

Izingatiwe hapa kwamba ili akronimu katika Kiswahili ikubalike na umuhimu wake utambuliwe na wazungumzaji, pana haja kubwa ya wataalamu wa Kiswahili kufuata mantiki fulani na mfumo maalum ulio wazi wa kuteua silabi za maneno ili kujenga neno. Kufikia sasa inaelekea kuwa utenzi wa silabi za kuunda msamiati kwa njia ya akronimu unafanya kwa unasibu tu. (Mdee 1986:123)

### 3.1.7 Uhuluti (Blending)

Uhuluti ni utaratibu wa kuunda msamiati ambapo mofimu huru mbili au zaidi huchanganywa ili kuunda msamiati/neno mpya ambao hubeba kwa pamoja maana zote za mofimu huru husika.

Utaratibu wa uhuluti unakaribiana sana na uambatanishaji na si rahisi kuzitenganisha taratibu hizi mbili za kuunda msamiati.

Polome (1967), Fromkin na Rodman (1974), ni miongoni mwa wataalamu ambao walishughulikia utaratibu wa uhuluti.

Fromkin na Rodman (1974:39) wanasema kuwa uhuluti ni uambatanishaji ambao ni 'mdogo kuliko' uambatanishaji. Wataalamu hawa wanatutolea mfano ufuatao:

Kiingereza

Smog kutokana na smoke + fog

Motel " " motor + hotel

Urinalysis " " urine + analysis

Edgar Polome (1967:82) anasema kwamba msamiati huundwa kwa kutumia uhuluti unapounganishwa na'mfanyi.' Kuunganisha "mfanyi" na vifaa aghalabu huonyesha kazi inayofanywa na wahusika. Kwa mfano,

Mfanyikazi - mfanyi + kazi

mfanyibiashara - mfanyi + biashara

Mifano zaidi ya uhuluti ni

Chumamali - kutokana na chuma + mali

Vitegauchumi - kutokana na tega + uchumi (wingi)

Mwanahewa - kutokana na mwana + hewa

Mwanamwali - kutokana na mwana + mwali

Wanachuo - kutokana na wana + chuo (wingi)

Mwanakijiji - kutokana na mwana + kijiji

Utoajitakamwili - kutokana na utoaji + takataka mwilini

Kutokana na mifano hii ya uhuluti ya kuunda msamiati wa Kiingereza na Kiswahili, ni dhahiri pia kwamba hakuna utaratibu maalum unaofuatua wa kufanya uhuluti. Maelezo ambayo yametolewa tayari

yanakanganya na hayatofautishi ipasavyo dhana ya akronimu, uambatanishaji, na uhuluti, hivyo pana haja ya kulifanyia suala hili uchunguzi zaidi.

### 3.1.8 Ukatizaji (Clipping)

Ukatizaji ni aina ya ufupishaji ambapo neno hujengwa kimkato kwa kuondoa sehemu ya mwanzoni au mwishoni ya neno hilo hilo pasi na kubadilisha maana yake.

D.M.W Njeru (1990) ametambua umuhimu wa utaratibu wa ukatizaji katika kujenga maneno ya Kiswahili na anadokeza kwamba ukatizaji hurahisisha matamshi na mawasiliano kwa jumla. Huu ni ukweli usiopingika na tunakubaliana naye.

Izingatiwe hapa kwamba 'maneno katizi (clipped words) huundwa kwa kuhifadhi sehemu fulani (hasa silabi ya kwanza) za neno asilia. Kwa mfano,

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kiingereza | | | |
| | Exam | - | Examination |
| | Co-ed | - | Co-education |
| | Lab | - | Laboratory |
| | Prof. | - | Professor |
| Kiswahili | Taz. | - | Kifupisho cha tazama |
| | agh | - | " " aghalabu |
| | wkt | - | " " wakati |
| | ktb | - | " " kitabu |
| | ktk | - | " " katika |
| | Bw | - | " " Bwana |

Bi - Bibi

Mhe - Mheshimiwa

Ndg - Ndugu

Jn - Jina

Njeru anadokeza kwamba utaratibu wa ukatizaji hautumiki sana katika kukuza msamiati wa Kiswahili. Msomi huyu hatuelezi ni kwa nini hautumiki hivyo anaacha mawazo yake yakipuayapuaya tu.

Tujuwavyo sisi ni kwamba utaratibu wa ukatizaji hauungwi mkono na wazungumzaji kwa sababu una dosari zake pia. "Maneno katizwa' mara nyingi huwakanganya wazungumzaji wa lugha hii. Kwa mfano,

K.t.b - laweza kuwa makitaba ama kitabu

Mwa - yaweza kuwa mwalimu au mwanamke n.k.

Aidha si rahisi kuelewa maana ya 'maneno katizi' Kwa mfano, agh. - kirefu chake hakiji moja kwa moja. Pana utata fulani hasa kwa mzungumzaji wa Kiswahili 'asiye-mjuzi' katika lugha hii ya Kiswahili. Isitoshe, msamiati mwingi wa Kiswahili si rahisi kuukatiza na mzungumzaji anapojaribu kufanya hivyo huambulia patupu kwa maana kwamba maana ya msamiati huo hubadilika. Kwa mfano, si rahisi kukatiza maneno yafuatayo

dada - (da)

mama - (ma)

karani - (kar)

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba ili njia hii iungwe mkono na watumiaji wa lugha ya Kiswahili, itahitajika kufanyiwa uchunguzi wa kina kirefu zaidi utakaojitokeza na utaratibu ulio bayana wa kukatiza maneno mengi ya Kiswahili.

### 3.1.9 Unyambuaji

Unyambuaji ni mojawapo ya njia muhimu sana ya kujenga msamiati kutoka katika kiswahili chenyewe. Wataalamu walioshughulikia utaratibu huu wa kuunda msamiati ni kama vile Ashton (1944), Polome (1967), Myachina (1981), Kapinga (1983), Mdee (1986) na Njeru (1990).

Mtazamo wa wasomi hawa wote, ijapokuwa Polome, kuhusu dhana ya unyumbuaji hauna uzito. Tunasema hivi kwa sababu mbili muhimu. Kwanza, kutofaulu kwao kutafautisha baina ya unyambuaji na uambishaji. Pili, kutozingatia kwao kwamba uambishaji, hauwezi ukatupa neno jipya. Wataalamu hawa hawatuonyeshi kuyajenga vipi maneno au iwapo ni kuyajenga upya maneno yale yale. Mdee (1986) anasema:

> "Kama ilivyokwishaelezwa, maneno mengi huundwa kwa kuambisha viambishi mbalimbali..." [51]

Kauli ya Mdee (ibid) haina mashiko na hatukubaliani naye. Sisi, kwa kutambua kwamba njia ya uambishaji haitupi neno jipya ila hutumiwa katika kujenga jina la kategoria ile ile, hatutajishughulisha nayo katika kazi hii. Hata hivyo, tumechukulia 'unyambuaji' kuwa ni utaratibu wa kuunda msamiati wa Kiswahili ambapo viambishi vitangulizi na viambishi vifuatilizi huongezwa kwenye

mzizi wa neno fulani ili kujenga neno/msamiati mpya.

E.N. Myachina (1981:14) maelezo yake kuhusu unyambuaji yametufaa sana hasa anapodokeza kuwa maneno yaliyonyambuliwa kudokeza mtenda jambo (binadamu) huundwa kwa kuongeza viambishi awali vya ngeli ya 1 na 2. Ukweli wa mtazamo wa mtaalamu huyu haupingiki hasa tukizingatia mifano ifuatayo:

m-sema - msema (jambo)
m-rithi - mrithi (mali)
m-chokozi - mchokozi (wa watu)
m-laji - mlaji
m-fua - mfua
m-somi - msomi
m-hakiki - mhakiki
m-chambuzi - mchambuzi

Maneno mengi ya Kiswahili yameundwa kwa njia hii. Mfano zaidi:

m-shambuliaji - mshambuliaji
m-kimbiaji - mkimbiaji
m-languzi - mlanguzi

Isitoshe, kiambishi awali cha ngeli ya 11 - U ni zalishi, na kinatumiwa katika kuunda maneno mapya kama vile:

ubaya
umoja
uzuri
urafiki
uadui
ulevi (u + lew + i) (w - v/- i)

upishi (u + pik + i) (K - S/- i)

Inafaa tusisitize hapa kwamba, pana na pia viambishi tamati vinavyotumika katika kutunga msamiati/maneno ya Kiswahili. Mathalani, (-e, -fu/-vu, -i, -ji, -o, -zi). Viambishi vifuatilizi hivi, vimejadiliwa na wataalamu waliotutangulia, letu hapa si kurudia kikasuku yaliyokwisha elezwa mbali ni kumulika palipo dosari, udhaifu ama matatizo katika njia hii ya unyambuaji.

Ama kwa hakika, hatuna budi kukubaliana na S.J. Falk (1973:41) kwamba utaratibu wa unyambuaji ni muhimu sana katika kuunda msamiati mpya, na hakuna kasoro yoyote ambayo tunaweza kuitoa.

### 3.1.10 Muhtasari

Ni baada ya kuzingatia taratibu hizo za uundaji wa msamiati wa Kiswahili na dosari zake ndipo hatuna budi KUPENDEKEZA katika sehamu hii ya Muhtasari kwamba:

- kuwe na mfumo maalum ambao ni lazima uzingatiwe na mataifa yote ambako Kiswahili kinazungumzwa wa kuunda msamiati wa Kiswahili ili msamiati isiendelee kuundwa 'vivi hivi tu'.
- kuwe na ushirikiano wa wanaleksikografia na wa wasanifishaji, katika kuunda msamiati mpya, iwapo pana haja ya kufanya hivyo, ili kuepukana na tatizo la ukubalifu wa msamiati mpya.
- kabla ya kuunda msamiati mpya, utafiti wa ndani zaidi ufanywe miongoni mwa Waswahili wenyewe ili msamiati kiasili ama msamiati wa zamani, ufufuliwe, uhuishwe na upewe matumizi mapya.

Baadhi ya mapendekezo haya labda yamekwisha tolewa na wataalamu waliotutangulia lakini hatuoni ubaya wowote kuyasisitiza hapa. Taratibu za ubunaji, unyambuaji na ufufuaji wa msamiati kiasili zikifuatwa, msamiati wote unaohitajika unaweza kupatikana mara moja.

# SURA YA NNE

## 4.1.0 Utangulizi

Ili kuweza 'kulifanyia haki' suala la ufufuaji wa msamiati wa zamani uliosahaulika katika kiswahili sanifu, itakuwa bora kueleza maswala fulani yanayofungamana nalo. Ni kutokana na kutazama mabadiliko na upoteaji wa maana katika msamiati wenye asili ya kigeni ndipo tutaweza kuelewa kinachosababisha msamiati fulani 'kufa'. Izingatiwe hapa kwamba, si tu msamiati kiasili ambao hufa, bali kuna na msamiati wenye asili ya kigeni ambao husahaulika na pahali pake pakachukuliwa na msamiati mwingine kiasili ama wa kigeni. Kwa mfano, neno shubaka - ni la Kiarabu "shubak". Neno hili lilipoingizwa katika Kiswahili lilibadilika kimaana. Maana asilia ya neno shubaka' ni dirisha (window). Kwa sasa linatumika katika Kiswahili kwa maana ya 'mahali pa kuweka vitu kama dawa'. Wazungumzaji wa Kiswahili hawasemi kwa mfano,

"Khamisi nifungulie hili shubaka"

husema: "Khamisi nifungulie hilo dirisha"

Dirisha ni neno lenye asili ya Kiajemi, na limesababisha, kufa kwa neno "shubaka" la Kiarabu (Mkele 1971:102). Michakato kama hii ya kukataliwa kwa neno moja na pahali pake pakichukuliwa na neno jingine ni suala ambalo linahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Hata hivyo, hatutajadili suala hili la mabadiliko na upoteaji wa maana katika msamiati wenye asili ya Kigeni kwa undani sana kwa sababu ya muda mfupi tulio nao.

.../113

### 4.1.1 Mabadiliko na Upoteaji wa maana katika msamiati wenye asili ya kigeni

Hatuna budi kukiri kwamba msamiati mwingi sana umeingizwa katika Kiswahili kupitia kwa lugha ya Kiingereza, lugha ambayo hadi leo ni rasmi katika mataifa mengi ya Kiafrika. Lugha hii, kama lugha nyinginezo za kileo za Ulaya, nayo imekopa msamiati mwingi kutoka lugha kongwe za Kigiriki na Kilatini.

(Mdee 1986:120) Sisi, ijapokuwa tunafahamu kwamba msamiati hubadilika kulingana na wakati, tunachukulia kwamba mabadiliko yatokeayo katika msamiati uliokopwa kutoka lugha kipaji hutokana na sababu kadha wa kadha na wala siyo tu suala la wakati. Baadhi ya sababu ni za kiisimu, kisaikolojia, kisiasa, na za kijamii, Aidha, tunaamini kuwa hatari ya utohoaji kutoka lugha kopaji haiwezi kueleweka vema pasi na kuonyesha namna mabadiliko yanavyotokea katika msamiati wenye asili ya kigeni. M.B. Mkelle (1971) alishughulikia zaidi mabadiliko katika maneno yenye asili ya Kiarabu, sisi tutajishughulisha na maneno si tu yenye asili ya Kiarabu bali pia ya Kiingereza. Kwa mfano;

Kiingereza:

neno "meter" ni la Kilatini "mittere" maana yake asilia ni kutuma (to send)

Neno hili lilipoingizwa katika Kifaranza "mettre" likapewa maana ya kuweka (to put).

Katika Kiswahili limekopwa ama limetoholewa na kuswahilishwa -mita na kupewa maana ya kisasa ya kipimio (cha umbali).

.../114

Neno nice[52] ni la asili ya Kilatini "nescius" kivumishi kilichoundwa kutokana na "ne scio" (I do not know/sijui) lilimaanisha ujinga (silly). Neno hili lilihifadhi maana yake asilia katika kifaransa "niais" lakini lilipotoka katika Kifaransa hadi Kiingereza, likawa nice si kwa maana ya mjinga/ujinga tana bali likawa latumika kumaanisha sawa, uzuri/ mzuri (fine). Leo tunazungumza juu ya:

a nice girl - msichana mzuri (badala ya msichana mjinga)

a nice guy - mvulana mzuri (mvulana mjinga).

Bila shaka kutokana na mfano huu, tunaweza tukaona dhahiri utata katika ukopaji. Je, tukope na kuswahilisha kutoka Kiingereza "nice" ama tuende kwa Kilatini "silly"? Hili ni suala ambalo Wataalamu wa Kiswahili hawana budi kulifanyia uchunguzi wa kina kirefu . Mfano zaidi wa maneno ambayo yamebadilika kimaana baada ya kutoholewa kutoka lugha kopaji ni:

(uchu) "lust" — pleasure (furaha) maana asilia
↘ sinfulness (usinifu) maana ya kisasa

"tune" — put on the right frequency - maana ya zamani
↘ seduce (tongoza) maana ya kisasa

kwa mfano, Khamisi was tuning Mary
(Khamisi alikuwa akimtongoza Mary)

"Idiot" — a private person (mtu mwadilifu) maana asilia
↘ a stupid person (mtu mjinga) maana ya sasa

"fond" — zamani likimaanisha ujinga (foolish)
↘ kwa sasa ni kupendana sana (affectionate)

"charity" ni neno la Kilatini, maana yake asilia "caritas" - upendo (dearness), lilipoingizwa katika Kiingereza linatumiwa sasa kwa maana iliyo tofauti

kabisa - tabia nzuri ndiposa yasemekana:

'charity begins at home'

(nidhamu huanzia nyumbani)

Kiarabu: Neno hamaki ni la asili ya Kiarabu, maana asilia ni ujinga sasa linatumika kwa maana ya hasira.

Safihi - maana asilia ni kutokuwa na akili timamu au ujinga.
Tazama Juma ni safihi - Juma ana kiburi/kichwa maji
Kwa sasa safihi - limepokea maana ilio tofauti kabisa baada ya kuingia katika Kiswahili - tunazungumzia safihi kidonda (man in the street).

Jambo muhimu ambalo tunalisisitiza hapa ni kwamba mabadiliko na upoteaji wa maana katika msamiati wenye asili ya kigeni hayatokei 'vivi hivi tu' pasi na sababu maalum.

F. de Saussure (1959) aliwahi kusema kuwa wakati hubadilisha vitu vyote, hakuna sababu yoyote ambayo inaweza kufanya lugha iepukane na sheria hii ya ulimwengu.
Naye Bloomfield (1933) alisema kuwa sababu za mabadiliko ya lugha hazijulikani. Wataalamu hawa wana mawazo mazito bila shaka na tunakubaliana nao. Ukweli kuwa wakati hubadilisha vitu vyote haupingiki. Kama tulivyokwisha kudokeza hapo mbeleni suala la wakati ni mojawapo ya sababu muhimu sana za mabadiliko na upoteaji wa maana katika msamiati wenye asili ya kigeni (na hata msamiati kiasili). Kwa mfano, tuseme kuna wanajamii - lugha A. Kutoka jamii hii kikachipuka kikundi - jamii B kwa kuhama. Wakati wa kuhama na hata miezi/miaka michache badaye, wakazi wa B na wa A hawatakuwa na tofauti. Wataongea sawa.

.../116

Lakini kadri wakati utakavyopita ndivyo wakazi wa B watakavyochomoza na kudumisha tofauti za kilugha za kuwatofautisha na wa A. Isisitizwe hapa kwamba mabadiliko ya kimsamiati yanapotokea katika wakazi wa B, tofauti nyingine hutokea hata miongini mwa wakazi wa A. Ingawa kimaeneo eneo la A halikugeuka, kiwakati na kimahitaji wakazi wa eneo hilo hubadilika. Kwa hivyo hata msamiati wao hubadilika kimaana. Kwa usemi mwingine kutokuwepo mfulilizo wa kukutana na watu wengine, labda kutokana na vikwazo kama vile mto mkubwa, bahari, maadui baina ya kikundi kimoja na kingine, au iwapo vyombo vya habari - magazeti, radio haviwafikii watu wote katika pembe zote walizomo, husababisha mabadiliko na upoteaji wa maana katika maneno kiasili na maneno yenye asilia ya kigeni. Kwa mfano,

> neno "masca" la Kilatini ambalo liliingizwa katika Kifaranza kama "masque" na kutoka hapo likakopwa katika Kiingereza kama 'mask' (masiki) baada ya mpito wa wakati limebeba maana ya sasa vazi tofauti na maana yake asilia ngao.

Neno telephone - ni la Kigiriki na linatokana na "tele" - far (umbali) na "phone" - sound (sauti).

S.A. Nabhany (1982) kwa kutoridhishwa na ukopaji na utohoaji wa msamiati wa kigeni na kuuswahilisha kama vile,

| | | |
|---|---|---|
| telephone | - | telefoni |
| television | - | televishoni |
| microphone | - | maikrofoni |
| earphone | - | iyafoni |

.../117

microscope - maiskroskopu

ray - rai

radio - redio, ameunda msamiati ufuatao kwa kutumia mizizi ya kibantu.

microscope - mangala

telephone - Rununu (habari za kuja bila kuletwa na mtu)

television - runinga (runu ya kenga kwa maninga/macho)

redio - mwengoya (mwengo - sauti) ya mbali

ray - uka.

Ingawa Nabhany (ibid) ametoa mchango mkubwa katika kuunda msamiati mpya, lakini inaelekea hakuzingatia historia ama asili ya msamiati fulani alioushughulikia. Kwa mfano, katika maneno mwengoya na rununu inaelekea hakuna mfumo maalum au ulio sawa anaoufuata katika kuyaunda maneno haya. Tungetaraji

neno "telephone" - "tele" - (far) = mbali - ya )
"phone" - (sound) = mwengo ) liwe mwengoya

hasa tukifuata usemi wake kuwa 'phone'/sauti ni mwengo na tele - mbali/ya (kama ilivyo katika radio hapo juu). Tungependekeza "telephone" litumiwe kwa maana ya mwengoya, na "radio" - iwe rununu.

Jambo muhimu tunalosisitiza hapa ni kwamba ili kuwepo mfumo maalum wa kuazima msamiati wa kigeni (na wa kuunda msamiati mpya) pana haja ya kuchunguza historia au asili ya msamiati huo. Hata hivyo, njia hii ya Nabhany, ingerekebishwa kwa kutumia ujuzi wa isimu ya lugha, ingefaa sana katika kuunda msamiati wa Kiswahili.

.../118

Kuhusu suala la ukale wa lugha M.B. Mkelle (1971) anasema:

> "labda suala hili - kutazama ukale wa lugha ili kuziba mapengo yaliyopo sasa huenda likawa na umuhimu zaidi katika kile kinachotendeka kwa sasa katika Kiswahili Kuhusu hatua za kuipanua lugha..."[53] (Tafsiri ni yetu).

Kutokana na dondoo hili ni dhahiri kuwa Mkelle (1971:104) ametambua umuhimu wa msamiati kiasili katika kuendeleza leksikoni ya Kiswahili. Mtaalamu huyu, anatoa mfano wa neno likizo ambalo lilikuwa linaelekea kufa lakini likaokolewa, limepata mashiko tena baada ya kuhuishwa na kupewa matumizi mapya.

likizo - linatokana na 'likizwa' ambalo zamani lilitumiwa katika shule za kufundisha korani kwa maana ya kuachiliwa waende nyumbani ,(wanafunzi) kwa mapumziko ya muda mfupi, sasa limepanuliwa kimaana na linatumiwa siyo tu kwa wanafunzi bali pia kwa wafanyikazi katika idara mbalimbali za serikali. Neno hili likizo linafaa zaidi badala ya livu ambalo latokana na utohoaji kutoka Kiingereza.

Kuna mifano chungu nzima ya maneno ya zamani ambayo, kwa maneno ya Mkelle (ibid) yanahitaji kuokolewa (rescued) kwa kuyafufua na kuyapa matumizi mapya.

Mathalani,

| Msamiati wa zamani | |
|---|---|
| ndeo | - kiburi (Kiarabu) |
| pantu | - pahali |
| nazaa | - aibu |
| nyemi | - furaha |

<u>shokori</u> - stihizai

<u>wele</u> - balaa

<u>pwiriri</u> - taabani

<u>uya</u> - rudi (ling. Kizulu - buya)

<u>mdarisi</u> - mwalimu

<u>nabihi</u> - tahadhari

<u>usindu</u> - chuki

<u>togo</u> - sifa

<u>ufyozi</u> - ufedhuli

<u>nswi</u> - samaki

(Taz. H.M. Mbega (1976 , 1984)

Haya ni baadhi tu ya maneno kiasili ama maneno ya zamani ambayo 'yamekufa' kwa maana kwamba yapo katika kazi za fasihi za zamani lakini hayatumiki katika maandishi ya kila siku. Kwa kuwa ni ukweli ulio dhahiri kwamba Kiswahili, kama lugha yoyote ile kinaweza kujiendeleza kimsamiati mumo kwa mumo, pana haja ya wataalamu wa Kiswahili kudurusu kamusi za zamani za Kiswahili, kupekuwapekuwa miongoni mwa Waswahili wenyewe na kuyapata maneno kiasili katika harakati zao za kuikuza lugha hii. Suala hili hatuna budi kulisisitiza hapa kwa sababu ya umuhimu wake. Tusije tukawa tunakimbilia tu maneno ya kigeni, kama inavyofanyika sasa, na ikaonekana kama kwamba maneno yahitajikayo hayawezi kupatikana kutoka katika Kiswahili chenyewe.

Iwapo tutazingatia haya tulioeleza hapo juu ni dhahiri kuwa tatizo la utohoaji kutoka lugha kopaji na hatari ya kuingiza vipengele ambavyo sio muhimu katika msamiati uliokopwa na kutoholewa na kuswahilishwa litatatuliwa kwa maoni yetu.

Aidha, ni kwa kuzingatia ukale wa lugha ya Kiswahili na ufufuaji wa msamiati wa zamani wa lugha hii ndipo Kiswahili kitajiendeleza kileksikoni kwa kuhuishwa na kupewa matumizi mapya msamiati uliofufuliwa ili kuziba mapengo ya msamiati maalum.

### 4.1.2 Tatizo la Meneno yanayokubalika kwa Wataalamu na Watumizi wa lugha ya Kiswahili

Uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili kwa njia ya ufufuaji wa msamiati kiasili wa Kiswahili uliosahaulika huenda usikwepe tatizo la ukubalifu. Tatizo la maneno yanayokubalika kwa Wataalamu na watumizi wa lugha ya Kiswahili si ligeni kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Pametokea tatizo la wataalamu wa Kiswahili kuyapinga maneno yaliyopendekezwa na wataalamu wengine kwa kuyachukulia kwamba 'hayana ladha' hivyo hayafai. Kwa mfano, wataalamu kama vile Bwana Mohamed Sharif Said, Sheikh A. Nabhany, wana msimamo kuwa msamiati wa zamani wa Kiswahili ambao hivi sasa umekufa, ukifufuliwa utasaidia kujaza au kuziba mapengo ya msamiati maalum (isilahi) wa kisayansi na kiteknolojia. Wataalamu hawa wamejitokeza na maneno yafuatayo:

ndisha (kwa maana ya aina fulani ya chakula cha kujenga mwili)
Neno hili linaweza kuchukua maana ya Vitamini (Vitamins)

Timea - 'Botany'

Maneno mengine yaliyopendekezwa yatumike ni:

mvunzizi/uvunzizi - 'air condition machine'

jopo - 'panel'

mwima - 'institute'

maenga - 'mathematics'

tundikana - 'vaccuum'

Mfano zaidi;

| Maneno yaliyopendekezwa | | Maneno yatumikayo Tanzania |
|---|---|---|
| Skuli ya uyezi (yaani ulezi) | - | Skuli ya vidudu ) Skuli ya chekechea ) Nursery school Skuli ya watoto wachanga) |
| Mawando au Skuli ya mawando (yaani ya kuanza) | - | Skuli ya msingi (Primary School) |
| Upili/Upilili au Skuli ya Upilini (yaani hatua ya pili) | - | Skuli ya Sekondari (Secondary school) |
| Uwoti (Uwote) (yaani kwa masomo ya aina zote) | - | Kolegi ? (College) |
| Ndaki (Kindakindaki) | - | Chuo Kikuu (University) |

(Tazama K. wa Mutiso, 1992)

Haya ni baadhi ya maneno yaliyopendekezwa yatumike na S.A. Nabhany (1982), (1992) lakini yamekataliwa na wataalamu wengine na watumizi wa Kiswahili kwa sababu 'hayana utamu' Kadhalika, msamiati wa zamani kama vile:

sururi - furaha

kwama - kunyonya

gele - kiburi

raina - harufu

.../122

| | | |
|---|---|---|
| khazaya | - | aibu |
| karii | - | mtaalamu |
| nongwa | - | balaa |
| nyuni | - | ndege |
| umbu | - | dada |
| bwege | - | mpumbavu |
| ajurali | - | kisasi na kadhalika umekataliwa kwa |

madai kwama'hauna mwonjo' .

Isitoshe, kuna nambari (numerals) za zamani zaidi za Kiswahili ambazo zimekataliwa na wataalamu wa Kiswahili. Kwa mfano;

| Nambari zitumikazo kwa sasa | Nambari za zamani za Kiswahili |
|---|---|
| 1. Mosi | Mosi |
| 2. Pili | muta |
| 3. tatu | turhanga |
| 4. nne | hagali |
| 5. tano | utumbu |
| 6. sita | ndadaru/mtandutu' |
| 7. saba | fungare/fukare/fungale |
| 8. nane | wakiya |
| 9. kenda | perekicha |
| 10. kumi | kuduo |

Waswahili walitumia gani au goyo mahali pa mia (100) la Kiarabu. Nambari ya juu inayojulikana katika Kiswahili ni kwikwi ambayo ni 'elfu moja (1000). Neno hili linapatikana katika Hamziya ambapo inaelezwa kuwa: "wenye ndala kala watu kwikwi kwa swai moja" 54

Jambo muhimu la kumulika hapa ni kwamba imekuwa si rahisi, katika ulimwengu wa sasa, kupata msamiati (au hata nambari kiasili za Kiswahili) ambao wataalamu wote wataukubali. Kwa usemi mwingine sisi, tunaelewe kuwa tatizo la ukubalifu lipo na linasababishwa na kutoelewana kati ya wataalamu na watumizi wa lugha ya Kiswahili. Watumiaji wa aina moja wamependelea taratibu fulani za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili na kutoiafiki aina nyingine pasi na kutambua kwamba baadhi ya msamiati wa kisasa haufuati nidhamu fulani na inaelekea umeundwa 'vivi hivi tu' yaani bila ya kufuata utaratibu ulio sawa. (Massamba 1989:74). Kwa sababu hii, halitakuwa jambo rahisi msamiati kiasili unaofufuliwa kuwaridhisha watumiaji wote wa lugha ya Kiswahili hasa wale wanatumia kigezo cha 'utamu wa msamiati'.

Tatizo la ukubalifu wa msamiati kiasili lina msingi wake katika mazoea. Bila shaka kuna msamiati kutoka lugha za kigeni kama vile kiarabu - wakati, laki, saliti, na staafu ambao wazungumzaji wa Kiswahili wameuzoea kiasi cha kuwa huenda msamiati wa zamani, njeo, kongwea, tongea, tuta, utayo, unyumu, mapuya (mvinyo), ngawira (mateka) na kadhalika utakataliwa kwa sababu ya mazoea. Kwa watu kama hawa, si ajabu msamiati wa zamani ukasikika masikioni mwao kama unawachachafya tu na ikawa ni shida kubwa kuukubali. Tatizo hili la mazoea ingawa ni la muda mfupi, lakini halifai kupuuzwa kwa vile limejengwa kwenye msingi wa itikadi/imani ya watumizi wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, maneno matakwa na matako

matako - mzizi wake ni -tak

Kutokana na mzizi huo tunapata -tako (need)

Katika hali ya umoja na matako (needs) katika hali ya wingi.

Neno matako nafasi yake imechukuliwa na matakwa kwa sababu za miiko ambapo matako halizingatii adabu ya lugha ya Kiswahili. Hata hivyo lingali linatumiwa kwa maana ya 'kikaliyo'. Kwa usemi mwingine maneno makali kama vile matako, mboo na kadhalika huenda yakafa kwa sababu wataalamu na watumizi wa lugha hii huyaona kuwa ni 'makali' yasiyoweza kuzoelewa na kutumiwa hadharani. Kwa hivyo, ndisha, jopo, matako ni miongoni mwa maneno mengine ambayo yamekataliwa na wataalamu na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

4.1.3 Suluhisho

Tumekwishadokeza hapo juu kwamba kuna tatizo la maneno yanayokubalika kwa wataalamu na watumizi wa lugha ya Kiswahili. Si rahisi kutoa suluhisho la moja kwa moja la tatizo la ukubalifu wa msamiati kiasili. Kwa hali kama hii hatuna budi kurejelea sababu za kukataliwa kwa msamiati mpya au msamiati kiasili. Sababu mojawapo muhimu inatokana na kasumba za kikoloni ambayo inaelekea kuwatawala wazungumzaji na wataalamu wa kuunda maneno ya Kiswahili. Kwa maoni yetu, njia ya ufufuaji wa msamiati wa zamani haiwezi ikaleta maneno kiasili kukubalika kabla ya tatizo la kikasumba la kuyaonea fahari maneno yaliyo-kopwa na kuswahilishwa moja kwa moja kutatuliwa. Hata hivyo suala la kikasumba lina mizizi mirefu na mara linapomtawala mzungumzaji lugha fulani, si rahisi kuliondoa. Linahitaji muda mrefu.

Wataalamu kama vile R. Besha (1972:24), S.A. Nabhany (1982), A. Mukhwana (1988:62) wamependekeza kuwa dhana mpya ziingiapo katika lugha ya Kiswahili ziundiwe majina mapya badala ya kukopa dhana mpya pamoja na majina yao. Mfano,

| | |
|---|---|
| botania | - <u>timea</u> |
| sayansi | - <u>ulimbo</u> |
| jenusi | - <u>ndugu</u> |
| kansa | - <u>ivi</u> |
| palasi | - <u>gongwa</u> |

Kwa sababu majina au msamiati ni mtajo tu wa kitu kinachokusudiwa. Pamoja na kuwa pendekezo hili lina uzito na tunakubaliana nao, hatuna budi kusisitiza hapa kuwa kabla ya kuunda msamiati mpya kuwakilisha dhana hizo, kwanza tupekuwapekuwa miongoni mwa Waswahili wenyewe na tukipata msamiati wa zamani wa kuwakilisha dhana hizo na uchukuliwe mara moja na kupanuliwa kimaana. Lakini pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka katika Kiswahili chenyewe, kama tulivyokwishataja mwanzoni, tubuni msamiati mpya kwa utaratibu maalum ili msamiati huo usikataliwe kwa madai kuwa ulibuniwa kiholela.

Uundaji wa msamiati mpya kwa kutumia utaratibu wa ubunaji na ufufuaji wa msamiati kiasili ukifanywa kwa mfumo ulio sawa na kwa utaratibu maalum unaoridhisha wazungumzaji wa Kiswahili, utatatua, kwa maoni yetu, tatizo la ukubalifu. Hata hivyo iwapo patatokea tatizo la kutokubaliana kwa wataalamu kuhusu msamiati wa zamani upi unaofaa kufufuliwa, kuhuishwa na kupewa matumizi mapya, hilo litakuwa ni tatizo la muda tu. Maana mara baada ya msamiati wa zamani huo kusikika tena na tena utakubalika bila shaka. Kwa mfano, baadhi ya msamiati kiasili, na msamiati ulioundwa na S.A. Nabhany (1982),baada ya mpito wa kiwakati,

/126

tayari umeanza kutumika katika shughuli rasmi na hata katika maandishi fulani ya Kiswahili ya kila siku, nao ni:

| | | |
|---|---|---|
| ngeu | - | (damu) |
| runinga | - | (televisheni) |
| ndaki | - | (chuo kikuu) |
| utayo | - | (sifa) |
| rununu | - | (radio) |

Msamiati kiasili/wa zamani ambao unaelekea umekubalika: kwa mfano,

| | | |
|---|---|---|
| ng'andu | - | (dhahabu) |
| mkwasi | - | (tajiri) |
| mkata | - | (masikini) |
| matayo | - | (lawama) |
| munyu | - | (chumvi) |

Msamiati wa zamani wa Kiswahili ambao haujakubalika na kupewa nafasi katika maandishi ya kila siku ni kama vile:

| Kingozi | | Kiingereza | | Kiswahili cha kisasa |
|---|---|---|---|---|
| ishe | - | father | - | baba |
| walangavu | - | clever | - | hodari |
| maya | - | to disappear | - | kutoweka, kupotea |
| skuli ya wawando | - | Primary school | - | shule ya msingi |
| mwasi | - | enemy | - | adui |
| tenga | - | committee | - | kamati |
| kitamsi | - | evil | - | kiovu |
| mayonjea | - | wisdom | - | busara |

(Taz. Mkelle 1976:74)

Mfano zaidi,

| | | |
|---|---|---|
| majama | - | askari |
| mwango | - | sauti |
| tama | - | aibu |
| kuamsa | - | kunyonyesha |
| mswaji | - | mke anayenyonyesha |
| pijo | - | sitihizai |
| ndwee | - | ugonjwa |
| viwi | - | muovu |
| mavi | - | maovu |
| nudama | - | majuto |

Haya ni baadhi ya maneno kiasili ya Kiswahili ambayo licha ya kwamba yapo katika lahaja za Kiswahili na fasihi za zamani za Kiswahili, hayajakubalika bado katika shughuli rasmi na maandishi ya kila siku. Ama kwa hakika, msamiati wa zamani kama huu ukifufuliwa na kupanuliwa kimaana, kama tunavyopendekeza, utaendeleza leksikoni ya Kiswahili bila shaka mbali na kuonyesha kuwa hapajakuwepo pengo kubwa la kimsamiati katika Kiswahili kama inavyofikiriwa na baadhi ya wataalamu. Lugha ya Kiswahili, kama lugha yoyote ile, imekopa msamiati wa kigeni ndiyo, lakini ukopaji wenyewe ni wa kawaida muno na wala si kwa sababu kwamba Kiswahili ni pungufu, kina uwezo wa kujitosheleza na kujiendeleza mumo kwa mumo.

Suala hili linadhihirishwa katika mifano tulizokwishazitoa hapo juu. Wataalamu na watumizi wa lugha ya Kiswahili ili waendeleze leksikoni ya lugha hii itawalazimu kujinazua, ama kuachana na kasumba za kikoloni ambazo zinawafanya baadhi

UNIVERSITY ... ROBI

yao kung'ang'ania maneno ya kigeni ilhali pana uwezekano mkubwa wa kutafiti na kuyapata maneno kiasili ya kuakilisha dhana za kigeni. Pale ambapo hatuwezi kupata msamiati kutoka katika Kiswahili chenyewe, kama tulikwishadokeza mbeleni, tubuni. Msamiati uliobuniwa usikataliwe na wataalamu kabla ya kuudadisi na kuchunguza uzito wake kwa kuongozwa na vigezo vya PEGITOSA. Hata hivyo, tatizo la ukubalifu wa msamiati wa zamani uliosahaulika katika Kiswahili sanifu lakini ambao ungali uko katika lahaja nyinginezo za Kiswahili kama Kipate, Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kimtangata na kadhalika na katika kazi za fasihi ya zamani kama Utenzi wa Tambaka, Kazi za Fumo Liyongo, Muyaka na kadhalika, na suluhisho la tatizo hili, ni masuala ambayo yanahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina kirefu na wataalamu wa Kiswahili.

### 4.1.4 Hitimisho

Katika kutamatisha kazi hii hatuna budi kukiri kwamba kuna njia kadha wa kadha za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili. Ufufuaji wa msamiati wa zamani unaodhaniwa 'umekufa' ilhali ungalipo katika lahaja nyingine za Kiswahili ni mojawapo wa njia za kuendeleza Kiswahili. Taratibu za Sheikh A. Nabhany na K.B. Kiingi zikifuatwa pia zitachangia sana katika suala la uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Hata hivyo, wana-leksikografia wa TUKI wanahitajika kuchunguza na kurekebisha taratibu za wataalamu hawa kwa kutumia ujuzi wao wa ismu ya lugha ya kuzipuuza na kukimbilia ukopaji wa maneno ya kigeni ambapo kuna maneno kiasili ya Kiswahili ya kuakilisha dhana hizo. Tumezungumzia taratibu za kuendeleza leksikoni ya

Kiswahili kama vile unyambuaji, ukopaji, kaleki, akronimu, uhuluti, ukatizaji na uambatanishaji. Katika uchunguzi wetu tumeona kwamba baadhi ya taratibu hizi zina dosari na udhaifu mkubwa licha ya kuwa hutumiwa sana na wataalamu wa TUKI kuunda msamiati wa Kiswahili. Dosari kubwa katika taratibu za kuunda msamiati ni ukosefu wa mfumo maalum ulio sawa unafaa kuzingatiwa na kufuatwa mara tu kunapotokea haja ya kuunda neno/msamiati kuwakilisha dhana mpya fulani katika Kiswahili. Aidha tumeona kwamba msamiati mwingi wa Kiswahili unaundwa 'vivi hivi tu' na hii ni sababu mojawapo ya kukataliwa kwa maneno mengi yanayoundwa na kupendekezwa na wataalamu wa TUKI na watumizi wa lugha ya Kiswahili. Isitoshe, katika uchunguzi wetu tumeona ya kwamba kabla ya kuunda msamiati mpya, pana haja ya kutafutatafuta katika Kiswahili chenyewe iwapo pana neno mwafaka na litumiwe kwa kulipanua kimaana ama kulipatia matumizi mapya. Hivyo, msamiati wa zamani uliosahaulika katika Kiswahili sanifu ukifufuliwa una umuhimu mkubwa katika uendelezaji wa leksikoni ya Kiswahili. Mathalani, msamiati wa zamani ukifufuliwa utasaidia kuziba mapengo ya msamiati maalum wa kisayansi na kiteknolojia. Hata hivyo, msamiati kiasili ama msamiati wa zamani unaofufuliwa hauna budi kuzingatia na kufaulu jaribio la PEGITOSA kabla ya kuingizwa katika matumizi rasmi au maandishi ya kila siku. Tumeona kuwa vigezo vya PEGITOSA ni muhimu sana katika suala la ukubalifu wa msamiati. Tumezungumzia kuhusu tatizo la maneno yanayokubalika kwa wataalamu na watumizi wa lugha ya Kiswahili. Mwisho na sio akali ni kuwa tumeona kwa kifupi suluhisho la tatizo la ukubalifu wa msamiati.

.../130

Kama suluhisho, imejadiliwa kuwa kuna haja ya wataalamu wa Kiswahili na wazungumzaji wa lugha hii kujikomboa kimawazo na kuachana na kasumba ya kikoloni ambayo inaelekea kuwatawala baadhi yao na inawafanya wayaonee fahari maneno yaliyokopwa na kuswahilishwa hata pale ambapo pana maneno kiasili ya Kiswahili yanayofaa kufufuliwa na kupanuliwa kimaana. Kwa kusisitiza suala hili tumeona kuwa wataalamu wa Kiswahili, wanaleksikografia, wasanifishaji na watumizi wa Kiswahili hawana budi kushirikiana katika kuendeleza leksikoni ya lugha hii. Aidha, wanapoendelea na shughuli za kuikuza lugha hii, wazingatie wanavyokosolewa lakini wasivunjike moyo - watambae baadaye watatembea. Labda itafaa sana tumalize kwa kujikumbusha maneno ya Sheikh A. Abedi:-

> "Lillahi tufanye kazi, Kiswahili tucharange,
> Njooni basi azizi, sisi na nyinyi tuchange...
> Kiswahili tukijenge, mjengo ukipasao."
> (Tazama Nkwera 1978:126)

Ama kwa hakika watumizi wa lugha ya Kiswahili wanayo dhima ya kuendeleza leksikoni ya lugha hii. Jambo hili halifai kuachiwa wataalamu wa TUKI pekee - lahitaji ushirikiano wa watu wote wanaozungumza lugha ya Kiswahili popote walipo ulimwenguni.

## TANBIHI

1. A. Mukhwana Tasnifu ya B.A. 1988 uk. wa 61.
2. Kama 1. hapo juu lakini uk. wa 62.
3. H.S. Olson (1972)"Swahili as an Educational Medium" katika Kiswahili, ju zuu 42/1 uk. wa 9.
4. M.M. Mulokozi (1975) katika Kiswahili, Dar es Salaam, tol. 45/2 September uk. wa 46 - 60.
5. G.A. Mhina (1972) katika Kiswahili juzuu 42/1 uk. wa 43.
6. F.M.V. Nkwera (1978) katika Sarufi na Fasihi na Vyuo uk. wa 122.
7. S. Chiraghdin, "Kiswahili tokea ubantu hadi Ki-"Standard Swahili" MULIKA Na. 6 (Sept, 1974) uk. 58.
8. R. Mukama (1989) katika Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili uk. wa 6.
9. J. Kitsao (1989) Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili uk. wa 59.
10. Kama 6 hapo juu lakini uk. wa 126.
11. W. Whiteley (1969) Swahili the Rise of a National Language uk. wa 98.
12. H.M. Mbega (1979) "Taifa Weekly" Agosti 11, 1979.
13. I. Mbaabu (1989) katika Usanifishaji wa Istilahi za Kiswahili uk. wa 24.
14. Kama 13 hapo juu.
15. J.S. Mdee (1986) katika Kiswahili, juzuu 53/1 & 53/2 uk. wa 125.
16. Kama 1 hapo juu lakini uk. wa 62.
17. Kama 16 hapo juu lakini uk. wa 61.
18. Sheikh A. Nabhany (1982) katika Kiswahili juzuu 49/2 uk. wa 100.
19. Kama 18 hapo juu lakini uk. wa 101.
20. H.J. Mwansoko ni mtaalamu wa TUKI ambaye alitufaa sana kwa maoni aliyoyatoa alipokuwa akijibu maswali yetu ya hojaji tuliompatia kule Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Mai 1993.
21. Kama 9 hapo juu lakini uk. wa 50.

.../132

22. R. Besha (1972) "Lugha ya Kiswahili hivi leo, hasa katika siasa" katika Kiswahili juzuu 42/1 uk. wa 23.

23. J. Yambi alitoa wazo hili katika hojaji yetu aliyoijaza katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

24. Kama 15 hapo juu lakini uk. wa 90.

25. Kama 18 hapo juu lakini uk. wa 102.

26. Kama 15 hapo juu.

27. E. Kezilahabi (1983) "Uchunguzi katika ushairi wa Kiswahili" katika Fasihi TUKI uk. wa 148.

28. Kulingana na maoni yake tulipokutana kule Tanzania - Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

29. Kama 13 hapo juu.

30. Abdallah Khalid (1977) The Liberation of Swahili.. uk. wa 212.

31. A.M. Khamisi (1985) katika Tasnifu yake ya Ph.D haijachapishwa bado.

32. M. Ali (1966) katika Kiswahili, juzuu 36/2, TUKI uk. wa 16.

33. Y.M. Kihore (1983) "Maandishi ya Kiarabu yaliyo na umuhimu kwa Kiswahili" katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Fasihi uk. wa 170

34. Kama 15. hapo juu lakini uk. wa 120. Pia tazama maelezo anayoyatoa katika Kiswahili Muundo na Matumizi

35. Likhako P. Imbuhila (1991) Tasnifu ya M.A. uk. wa 33.

36. Kama 3. hapo juu.

37. C.W. Temu (1972) katika Kiswahili, juzuu 42/1 uk. wa 1.

38. Kama 9. hapo juu lakini uk. wa 52.

39. M.S. Abdalla (1976) Mwana wa Yungi Hulewa uk. wa 7.

40. S. Robert (1956) Wasifu wa Sinti Binti Saad uk. wa 57.

41. TUKI (1987) Istilahi-Kiingereza-Kiswahili Ripoti ya Warsha ya Kanda ya Utayarishaji uk. 62.

42. Kama 1. hapo juu lakini uk. 62.

43. Dondoo hili limenukuliwa na K.B. Kiingi (1989) " A critical Examination of Swahili Expressional Modernisation in the Formal & Natural Sciences" uk. 146. Amemnukuu M.H. Abdulaziz(1989) Tafsiri yetu.

44. I.N. Shariff (1988) Tungo zetu uk. wa 28.

45. C.W. Temu (1984) katika Kiswahili juzuu 51/2 & 51/2 uk. 117.

46. Kama 15 hapo juu lakini uk. 119.

47. M.H. Abulaziz (1989) katika Kiswahili juzuu 56/1 uk. 35.

48. D.M.W. Njeru (1990) Tasnifu ya M.A. uk. wa 22.

49. S.J. Falk (1973) Linguistics & Language uk. 41.

50. Kama 49. hapo juu lakini uk. wa 40.

51. J.S. Mdee (1986) Kiswahili Muundo na Matumizi yake uk.

52. Neno hili nice na mengine kama vile 'idiot', na 'lust' tumeyarudia kimaksudi ili kusisitiza hoja yetu na kwa kutaka kuyafafanua zaidi maneno hayo.

53. M.B. Mkelle (1971) katika Kiswahili, juzuu 41/1 uk. 104.

54. Kulingana na uchunguzi uliofanywa na wa Mutiso (1992) katika sehemu ya kaskazini ya pwani ya Kenya juu ya "Ushairi wa Kiswahili na maneno ya kizamani."

## MAREJELEO


Abdulaziz, M.H. (1979): Muyaka 19th C. Swahili Popular Poetry. K.L.B. Nairobi

(1985): "Aspects of Lexical and Semantic Elaboration in the process of Modernisation of Swahili". In Swahili Language and Society. Edited by J. Maw and D. Parkin. Beitrage Zur Afrikanistik Vol. 23. Vienna.

(1989): "Development of Scientific and Technical Terminology in African Languages". In proceedings of The International Seminar on Terminology. (The Academy of Ethiopia Languages and Terminology Terms Translation Project).

Adams, V. (1973): An Introduction to Modern English Word Formation. London. Longman Group Ltd.

Aitchison, J. (1981): The Language Change: Progress or Decay? Fontana Press. London.

Akida, H. (1975): Kamusi ya Maneno ya Sayansi ya Elimu-viumbe (Biolojia) TUKI. Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Ali, M. (1966): "Maendeleo ya Maandishi ya Kiswahili" katika Kiswahili, juzuu 36/2, TUKI. Dar es Salaam.

Ashton, E.O. (1947): Swahili Grammar. London. Longman, Green & Co. Ltd.

BAKITA (1974, 1976, 1978, 1980): Tafsiri Sanifu Tol. la 1,2,3,4 Dar es Salaam.

Baruwa, A (1979): "Taifa Weekly" Nov. 24, 1979.

Besha, R (1972): "Lugha ya Kiswahili hivi leo hasa katika siasa". katika Kiswahili, juzuu 42/1 Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Uchunguzi wa Kiswahili.

Chao, Yuen R. (1968): Language and Symbolic Systems Cambridge Eng. & N. York. Cambridge University Press.

Chiraghdin, S. na Wenzie (1975): "Tarehe ya Ushairi" Mulika Toleo la 7 DSM

Chiraghdin S. na Mnyampala (1977): Historia ya Kiswahili Oxford University Press.


UNIVERSITY ... OBI LIBR...

Crystal, D. (ed)(1982): A first Dictionary of Linguistics & Phonetics uk. Cambridge University Press.

D'Agostino, F. (1986): Chomsky's System of Ideas Clarendon Press - Oxford.

Falk Julia, S. (1973): Linguistics & Language Xerox College Pub. Toronto.

Ferguson, Charles A.(1968): Language Development. katika Fishmann J.A & Ferguson C.A. Language Problems of Developing Nations. John Wiley & Sons. N. York.

Fulass, H. (1971): "Problems of Terminology" In W.H. Whiteley (ed). Language use and Social change. Oxford University Press. London.

Gibbe, A.G. (1983): "Maendeleo ya Istilahi za Kiswahili". Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili . TUKI Dar es Salaam.

Godman, A. & Payne E.M.W. (1979): Longman Dictionary of Scientific Usage. London. The scientific Book Guild.

Hartmann, R.R.K & Stock (1972): A Dictionary of Language & Linguistics. Applied Science Publishers Ltd. London.

Hogben, L. (1969): The Vocabulary of Science. London. Heinmann.

Johnson, F. (1939): A Standard Swahili - English Dictionary. Nairobi. Oxford University Press D.S.M.

Kezilahabi, E. (1983): "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili" Makala ya semina ya Kimataifa... III Fasihi TUKI. D.S.M.

Khalid, A. (1977): The Liberation of Swahili from European Appropriation. E.A.L.B. Kenya. Nairobi.

Kiingi, Kibuuka B.(1982): "Maneno ya kukopa na tafsiri ya kukopa katika Kiswahili cha kisayansi na kiteknolojia. Mwanko 1. Chakina.

(1984): "Some obstacles to the Vocabulary Expansion of Scientific Swahili" Mwanko 2. Chakina

(1985): A systematic modernisation of a bantu language: Luganda. Published by Organisation of African Unity - Inter African Bureau of Languages. Kampala.

(1989): A systematic approach to the problems of the expressional modernisation in the formal and natural science; The case of Luganda. University of Bielefeld.

(1992): A Theory of Scientific Terminology A.D. LITT Research Proposal. Kenyatta University.

Kitsao, J. (1989): "Ukubalifu wa msamiati/Istilahi: Mifano kutoka Kenya" TUKI. Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Klein-Arendt, R.(1987): Spache und Geschichte in Africa. Helmut Buske Verlag Hamburg.

Langacker, R.W. (1968): Language and Its structure-some Fundamental Linguistic concepts, Harcourt, Brace & World Inc. U.S.A.

Likhako, P.I. (1991): Ufaaji wa Kiswahili kama lugha ya kisomo Tasnifu ya M.A. University of Nairobi. Haijachapishwa.

Massamba, D.P.B.(1987): "Dhana ya Polisemia na sulubu zake katika Kiswahili". Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Research. Dar es Salaam

(1988): "Sababu za kubadilika kwa maana za maneno: Mifano kutoka Kiswahili" Kiswahili Juzuu 55/1 & 55/2. TUKI. Chuo Kikuu cha DSM.

Mbaabu, I. (1989): "Ukubalifu wa Msamiati: Mifano kutoka Kenya" katika TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(1991): Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili - Longman Kenya Ltd.

Mbega, H.M. (1979): "Taifa Weekly" Agosti 11, 1979.

(1984): Dafina ya Umalenga Longman Kenya Ltd.

Mdee, J.S. (1980): The Degree of Acceptability of the New Swahili words: Speakers' response analysis. Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

(1984): "Matatizo ya Kuunda Msamiati wa Kiswahili" katika Kiswahili, juzuu 53/1. TUKI Dar es Salaam.

(1986): Kiswahili Muundo na Matumizi yake Intercontinental Publishers Ltd. Nairobi.

(1986): "Matatizo ya kuunda istilahi..." katika Kiswahili juzuu 53/1 & 53/2 TUKI DSM

.../137

Mfaume, G.E. (1989): Misingi ya Isimu na lugha ya Kiswahili. Dar es Salaam. Utamaduni Publishers.

Miche, Gudrum (1979): Marburgen Studien Zur Afrika. Asienkunde Verlag Von Dietrich Reimer Berlin.

Mkelle, M.B. (1971): "Change in content & meaning of words" katika Kiswahili juzuu 41/1 TUKI. DSM.

Mukhwana, A. (1988): Ukuzaji wa Kiswahili. Tasnifu ya B.A. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi, M.M. (1975): "Revolution and Reaction in Swahili Poetry" Kiswahili, Toleo la 45/2 Dar es Salaam

Munguti, E. (1989): Uundaji wa Nomino katika Kiswahili. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutahi, K. (1986): "Swahili lexical expansion - prospects and problems". katika Kiswahili. juzuu 53/1 TUKI Dar es salaam.

Mwangomwango, J.S (1972): "Kiswahili Karne ya Ishirini" katika Kiswahili, juzuu 42/1 TUKI. Dar es salaam.

(1969): Lugha yetu. Baraza la Kiswahili DSM.

Mwaro, G.A. (1991): Uundaji wa majina ya Kiswahili. Tasnifu ya B.Ed. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Myachina, E.N. (1981): The Swahili Language - A descriptive Grammar. London. Kegan Paul, Boston & Henley.

Nabhany, S.A. (1982): Barua, Maoni, Mapitio, Mashairi n.k. 'Kiswahili', juzuu 49/2 jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Nassir, S.A. (1972): Al-Inkishafi. Oxford University Press. Nairobi.

Nicholson, R.A. (1969): Literary History of the Arabs. Cambridge, University Press.

Njeru, D.W.M. (1990): Lexical Expansion in Kiswahili. A study of strategies in corpus Development. Unpublished M.A. Dessertation. University of Nairobi.

Nkwera, F.M.V (1978): Sarufi na Fasihi na Vyuo. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Ohly, R. (1977): "The Problems of Scientific Terminology in Swahili" katika Kiswahili juzuu 47/1 (Wahariri Gibbe, Kiango na Mbughuni). JISR Dar-es-Salaam.

(1981): A short Mannual of Coinage in Swahili. Unpublished manuscript, Institute of swahili research, University of Dar es Salaam.

Olson, Howard S. (1972): "Swahili as an Educational Medium" katika Kiswahili, juzuu 42/1 TUKI. DSM.

Omari, C.K. (1969): "Towards the Development of Swahili Theological Terms" KISWAHILI(JISR) Dar es salaam.

Pei, Mario A. (1967): Language Today A survey of current linguistic thought. Funk & Wagnalls N.York

Polome, E. (1969): Swahili Language Handbook

Quine, W.O. (196)): London. Kegan Paul. Word and Object Cambridge, Mass; M. I.T. Press.

Ruo, K.R. (1979): "Taifa Weekly" Disemba 1, 1979.

Shariff, N.I. (1988): Tungo zetu Msingi wa Mashairi na tungo nyinginezo. The Red sea Press Inc.

Temu, C.W. (1972): "Swahili Vocabulary Expansion: A Preliminary Observation" katika Kiswahili juzuu 42/1 TUKI. Dar es Salaam.

(1984): "Kiswahili Terminology: Principles adopted for the enrichment of the Kiswahili language" katika Kiswahili juzuu 51/1 na 51/2 Dar es salaam.

TUKI (1981): Kamusi ya Kiswahili Sanifu Oxford University Press.

(1990): Kamusi Sanifu ya Ismu na Lugha Chuo Kikuu, Dar es Salaam

(1990): Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia. Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Wa Mutiso K. (1985): Hurafa na Uyakinifu katika Hamziyah Unpublished M.A. Dissertation, U.O.N.

(1992): Kamusi ya Kwanza ya Ushairi wa Kiswahili na maneno ya Kizamani, (Mswada ambao haujachapishwa bado) U.O.N.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

.../139

Weber, H. (1985): Longman Dictionary of Applied Linguistics Hongkong: Longman Group.

Weston, W. (1965): "Law in Swahili - Problems in Developing the National Language" katika Swahili juzuu 35/2 TUKI Dar es salaam.

Whiteley, W. (1969): Swahili The Rise of a National Language Methuen & Co. Ltd. London.

Whitney, W.D. (1895): The life & growth of language NewYork D. Appleton Ams Press.

Williams, G.G (1935): Creative Writing, Harper & Row Publishers.

Zawawi, S.M. (1979): Loan-words and Their effects on the Classification of Swahili Nominals Leiden: E.J.Brill.

Ziman, J. (1976): The Force of Knowledge Cambridge University Press.

Zgusta, L. (1971): Manual of Lexicography Monton, The Hague.